
# Stadi za Kazi

## Kitabu cha Mwanafunzi

### Darasa la Sita







Taasisi ya Elimu Tanzania

FOR ONLINE USE ONLY
DO NOT DUPLICATE

# Stadi za Kazi

## Kitabu cha Mwanafunzi

### Darasa la Sita



JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA
WIZARA YA ELIMU, SAYANSI
NA TEKNOLOJIA

*Cheti cha Ithibati*

Na. 222

Jina la Chapisho: Stadi za Kazi Kitabu cha Mwanafunzi Darasa la Sita

Mchapishaji: Taasisi ya Elimu Tanzania

Mwandishi: Taasisi ya Elimu Tanzania

ISBN: 978-9987-09-039-6

Kitabu hiki kimeidhinishwa na Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia tarehe 20 Septemba, 2019 kuwa Kitabu cha Kiada kwa ajili ya Mwanafunzi wa Darasa la Sita katika ngazi ya elimu ya Msingi nchini Tanzania kulingana na Muhtasari wa Mwaka 2016.

Dkt. Lyabwene M. Mtahabwa
Kaimu Kamishna wa Elimu.

FOR ONLINE USE ONLY

Taasisi ya Elimu Tanzania

Stadi za Kazi darasa la 6.indd 1 23/07/2021 15:11

FOR ONLINE USE ONLY
DO NOT DUPLICATE

© Taasisi ya Elimu Tanzania 2019

Toleo la Kwanza 2019
Chapa ya Pili 2021

ISBN: 978 – 9987 – 09 – 039 – 6

Taasisi ya Elimu Tanzania
S.L.P 35094
Dar-es-Salaam.

Simu: +255 735 041 170/ 735 041 168
Baruapepe: director.general@tie.go.tz
Tovuti: www.tie.go.tz

FOR ONLINE USE ONLY

Haki zote zimehifadhiwa. Hairuhusiwi kunakili, kurudufu, kuchapisha, kutafsiri wala kukitoa kitabu hiki kwa namna yoyote ile bila idhini ya maandishi kutoka Taasisi ya Elimu Tanzania.



Stadi za Kazi darasa la 6.indd 2 23/07/2021 15:11

FOR ONLINE USE ONLY
DO NOT DUPLICATE

# Yaliyomo

**Utangulizi**.........................................................................v

**Shukurani**.........................................................................vi

**Sura ya Kwanza**

Unadhifu.........................................................................1

**Sura ya Pili**

Utunzaji wa mazingira..........................................................20

**Sura ya Tatu**

Upishi.........................................................................37

**Sura ya Nne**

Ala za muziki ..........................................................60

**Sura ya Tano**

Kumudu misingi ya uigizaji..........................................................68

**Sura ya Sita**

Picha, vichezeo na uchapaji..........................................................84

FOR ONLINE USE ONLY



Stadi za Kazi darasa la 6.indd 3 23/07/2021 15:11

FOR ONLINE USE ONLY
DO NOT DUPLICATE

## Sura ya Saba

Ufinyanzi, ususi na vifani........................................................110

## Sura ya Nane

Stadi za ujasiriamali..............................................................124

## Sura ya Tisa

Usimamizi wa fedha................................................................141

FOR ONLINE USE ONLY



Stadi za Kazi darasa la 6.indd 4 23/07/2021 15:11

FOR ONLINE USE ONLY
DO NOT DUPLICATE

# Utangulizi

Kitabu hiki ni cha pili katika mfululizo wa vitabu vya Stadi za Kazi ambacho kimeandaliwa mahususi kwa mwanafunzi wa Darasa la Sita. Kitabu hiki kimelenga kukuza umahiri wa stadi za uchunguzi, ugunduzi, udadisi, ubunifu, kusoma, kuandika na kuhesabu. Aidha, kitabu hiki kina sura tisa zilizoandaliwa kukidhi mahitaji ya muhtasari wa somo linalohusika. Sura hizo ni: Unadhifu; Utunzaji wa mazingira; Upishi; Ala za muziki; Kumudu misingi ya uigizaji; Picha, vichezeo na uchapaji; Ufinyanzi, ususi na vifani; Stadi za ujasiriamali na Usimamizi wa fedha. Kitabu hiki kinawasilisha maudhui kwa njia ya habari, picha, kazi za vitendo na mazoezi.

FOR ONLINE USE ONLY



Stadi za Kazi darasa la 6.indd 5 23/07/2021 15:11

FOR ONLINE USE ONLY
DO NOT DUPLICATE

# Shukurani

Taasisi ya Elimu Tanzania (TET) inatambua na kuthamini mchango muhimu wa washiriki waliofanikisha uandishi wa kitabu hiki cha mwanafunzi.

TET inatoa shukurani za dhati kwa mchango uliotolewa na wataalamu wafuatao walioshiriki kutayarisha kitabu hiki:

**Waandishi:** Mwl. Zena H. Amiri, Mwl. Gaitani F. Romwald, Mwl. Revocutus Kundy, Dkt. Martha W. Tesha na Mwl. Kalistus Chonya.

**Wahariri:** Dkt. George D. Nahimian (Sanaa za ufundi), Dkt. Kassomo Mkallya (Muziki) Mwl. Juma M. Masine (Sanaa za maonesho), Mwl. Zahra S. Majili na Mwl. Caroline J. Sobayi (Upishi na lishe) , Mwl. Peter W. Haule (Sanaa za ufundi), Mwl. Richard A. Nguma (Sanaa za ufundi) na Bi. Wema L. Msigwa (Lugha-BAKITA)

**Msanifu:** Bw. Jerome K. Ndubusa

**Wachoraji:** Alama Art and Media Production Limited

**Mpiga picha:** Bw. Chrisant Ignas

**Mratibu:** Mwl. Zena H. Amiri

Pia, TET inatoa shukurani kwa walimu wote walioshiriki katika ujaribishaji wa kitabu hiki. Vilevile, Taasisi inatoa shukurani za pekee kwa shirika la “Global Partinership for Education (GPE)” kupitia mradi wa Kukuza Stadi za Kusoma, Kuandika na Kuhesabu (KKK) uitwao “Literacy and Numeracy Education Support (LANES II)” kwa ufadhili wao uliofanikisha kazi ya kuchapisha kitabu hiki.

Aidha, Taasisi inatoa shukurani za pekee kwa Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia kwa kutoa rasilimali fedha iliyofanikisha uandishi wa kitabu hiki cha mwanafunzi.

Dkt. Aneth A. Komba
Mkurugenzi Mkuu
Taasisi ya Elimu Tanzania

FOR ONLINE USE ONLY

FOR ONLINE USE ONLY
DO NOT DUPLICATE

# Sura ya Kwanza

## Unadhifu

### Utangulizi

*Ulipokuwa Darasa la Tano, ulijifunza kuhusu usafi wa mwili, usafi wa mavazi, utunzaji wa mavazi na usafi wa makazi. Katika sura hii utajifunza kuhusu ufuaji wa nguo, upigaji pasi kwa kutumia pasi ya umeme na pasi ya mkaa pamoja na usafi wa viatu. Usafi wa nguo, upigaji pasi pamoja na usafi wa viatu huchangia mtu kuonekana nadhifu. Unadhifu humwezesha mtu kuwa na furaha, kujiamini, kupendeza na kukubalika katika jamii. Hivyo maudhui ya sura hii yatakuwezesha kuwa nadhifu siku zote ukiwa shuleni na nyumbani.*

### Utunzaji wa mavazi



Fikiri

1. Je, ni kwa nini nguo huchafuka?
2. Kitu gani kitatokea iwapo hutafuata hatua za ufuaji nguo ulizojifunza ulipokuwa Darasa la Tano?

Katika Darasa la Tano ulijifunza kuwa nguo huchafuka kutokana na jasho, vumbi na uchafu mwingine kama vile matope, mkaa, girisi na mafuta. Nguo zilizochafuka huweza kutoa harufu mbaya na kuvutia wadudu na vimelea vya magonjwa. Vilevile, ulijifunza kuwa nguo zilizochafuka sana huchakaa haraka kwa kuwa zinahitaji kusuguliwa sana wakati wa kufua. Ni muhimu kuhakikisha kuwa unafua nguo zako mara zinapochafuka. Hakikisha nguo zako za ndani pamoja na soksi zinafuliwa na kubadilishwa mara kwa mara. Ukifuata utaratibu huu utaepuka kutoa harufu mbaya na kupata magonjwa ya ngozi kama fangasi. Hivyo, nguo zinahitaji kutunzwa vizuri ili ziweze kuwa na mwonekano mzuri na kudumu kwa muda mrefu.



Stadi za Kazi darasa la 6.indd 1 23/07/2021 15:11

FOR ONLINE USE ONLY
DO NOT DUPLICATE

## Kuondoa madoa kwenye nguo

Madoa yanapoingia kwenye nguo husababisha nguo kuwa na mwonekano mbaya. Ni vema madoa yaondolewe mara tu yanapoingia kwenye nguo ili kurahisisha utoaji wake. Doa likiachwa kwenye nguo kwa muda mrefu huendelea kupenya katika nyuzi za nguo. Utoaji wa madoa hutegemea aina ya doa na rangi ya nguo pamoja na aina ya kitambaa. Madoa katika nguo za pamba huweza kutolewa kwa kutumia vitoa madoa vya aina mbalimbali kama ifuatavyo:

(i) Madoa yanayotokana na vyakula kama matunda na michuzi huweza kutolewa kwa kutumia chumvi, maji ya moto, maji ya limau, magadi au mionzi ya jua;

(ii) Madoa yenye asili ya wanyama kama damu huweza kuondolewa kwa kutumia maji baridi yaliyochanganywa na chumvi. Maji ya moto sio mazuri kutumia kwa kuwa huweza kusababisha doa hilo kupenya zaidi kwenye nyuzi za nguo; na

(iii) Madoa yenye asili ya kemikali kama wino huweza kuondolewa kwa kutumia maji ya limau au nyanya au maziwa ya mgando. Baada ya hapo mimina maji ya uvuguvugu katika doa na uache kwa muda wa dakika 10-15. Sugua sehemu yenye doa kwa kufikicha mpaka doa lote litoke kisha fua nguo yako kwa kufuata utaratibu unaotakiwa.

***Ufuaji wa nguo:*** Ufuaji wa nguo ni muhimu kwa afya njema na mwonekano nadhifu wa mvaaji. Ulipokuwa Darasa la Tano ulijifunza jinsi ya kufua sare za shule zikiwemo shati, kaptura na sketi. Ulijifunza mambo muhimu ya kuzingatia katika kufua nguo hizo. Hakikisha unafuata utaratibu huo unapofua nguo ili zipendeze na zidumu kwa muda mrefu. Hata hivyo, zipo nguo nyingine ambazo huhitaji umakini zaidi wakati wa kufua ili kutoharibu mwonekano wake. Nguo hizi ni kama fulana na sweta ambazo zinatabia ya kuvutika iwapo hazitafuliwa kwa uangalifu. Wakati wa kufua nguo hizi ni muhimu kufuata hatua zote za ufuaji ukizingatia usahihi wa usuguaji, ukamuaji na uanikaji wa nguo hizi. Zingatia mambo yafuatayo wakati wa kufua nguo za aina hii:

FOR ONLINE USE ONLY



Stadi za Kazi darasa la 6.indd 2 23/07/2021 15:11

FOR ONLINE USE ONLY
DO NOT DUPLICATE

i. Andaa vifaa kwa ajili ya kufua nguo kama ulivyojifunza ulipokuwa Darasa la Tano.

ii. Tenganisha nguo kulingana na rangi zake kabla ya kuziloweka kuepusha kuchujiana rangi. Nguo zilizochujiana rangi husababisha kutokuwa na mwonekano mzuri. Vilevile, tenganisha nguo kulingana na kiwango cha uchafu wa nguo zinazofuliwa.

iii. Kagua nguo zote ili kuhakikisha hakuna kitu kama pesa au kifaa hatarishi kama pini au wembe ulioachwa kwenye nguo.

iv. Rekebisha nguo iliyochanika au iliyofumuka kabla ya kufua kwani zinaweza kuchanika zaidi wakati wa kuzisugua au kuzifikicha.

v. Iwapo nguo inayofuliwa ni sweta au fulana, hakikisha unafinyanga bila ya kusugua kwa nguvu. Kusugua au kufikicha kwa nguvu kunaweza kuharibu mwonekano wa umbo la nguo hizo.

vi. Baada ya kufua nguo, suuza kwa maji safi ili kuondoa sabuni yote.

vii. Iwapo nguo inayofuliwa ni sweta au fulana, punguza maji kwenye nguo iliyosuuzwa kwa kuiminyaminya tayari kwa kuanikwa. Ukamuaji wa nguo za aina hii, kunachangia kuharibu mwonekano wake hususani kuongezeka ukubwa kwenye mikono, mabega na eneo la shingo. Pia huweza kudhoofisha uimara wa nyuzi zilizotumika kufuma nguo za aina hii.

viii. Anika nguo kwa kuzingatia utaratibu sahihi wa uanikaji. Wakati wa kuanika sweta au fulana epuka kuzivuta kwani huweza kuharibu mwonekano wake au kuongezeka ukubwa.

ix. Iwapo fulana au sweta limetengenezwa kwa nyuzi za sufi, hakikisha unalitandaza kwenye ubao, meza au mkeka kisha lipime au chora kulizunguka na tunza vipimo vyake kabla ya kufua. Baada ya kufua nguo hiyo, litandaze tena kwa kufuata vipimo vya awali ili kuliweka katika mwonekano wake wa awali kabla halijafuliwa. Acha likauke vizuri.

x. Epuka kuacha nguo kwenye jua kali kwa muda mrefu kwa kuwa jua kali huharibu nyuzi zilizotengeneza nguo hizo na hupausha rangi ya nguo.

FOR ONLINE USE ONLY

FOR ONLINE USE ONLY
DO NOT DUPLICATE

xi. Nguo zikauke vizuri kisha zihifadhiwe sehemu yenye hewa ya kutosha kuepuka kupata ukungu. Nguo zikipata ukungu mwonekano wake huharibika na pia huchakaa mapema. Unaweza kuzitunza nguo zilizofuliwa na kukauka vizuri katika kabati, boksi, tenga, sanduku au begi.

### Kazi ya kufanya namba 1

1. Ondoa doa la wino lilioingia katika kitambaa cheupe cha pamba.
2. Fua nguo aina ya sweta au fulana ukizingatia hatua zote za ufuaji.

### Zoezi la kwanza

1. Eleza sababu tatu za kufua nguo mara tu zinapochafuka.
2. Kwa nini tunashauriwa kufanya mambo yafuatayo wakati wa kufua nguo?
   (a) Kutenganisha nguo kabla ya kuziloweka.
   (b) Kufanya marekebisho ya nguo kabla ya kuzifua.
3. Kitu gani kitatokea iwapo utaacha nguo zenye unyevunyevu katika ndoo ya chuma?
4. Eleza mambo matatu yanayoweza kuharibu mwonekano wa nguo kama sweta au fulana.

FOR ONLINE USE ONLY



Stadi za Kazi darasa la 6.indd 4 23/07/2021 15:11

FOR ONLINE USE ONLY
DO NOT DUPLICATE

## Upigaji pasi nguo



Fikiri
Je, ni kwa nini unapaswa kupiga pasi nguo?

Nguo ikishafuliwa huwa na mikunjokunjo ambayo huondolewa kwa kupigwa pasi. Nguo iliyopigwa pasi huwa na mwonekano mzuri. Kitendo hicho hufanyika kwa kutumia pasi. Zipo aina tatu za pasi ambazo ni pasi inayotumia nishati ya mkaa, umeme na mafuta ya taa kama inavyoonekana katika Kielelezo namba 1.



Pasi kavu ya umeme



Pasi ya umeme ya mvuke



Pasi ya mkaa



Pasi ya mafuta ya taa

**Kielelezo namba 1:** *Aina za pasi*
***Chanzo:*** *https://victoriancollections.net.au* tarehe 27/07/2019

FOR ONLINE USE ONLY

FOR ONLINE USE ONLY
DO NOT DUPLICATE

Ni muhimu kupiga pasi nguo kwa sababu zifuatazo:

(a) Kuzikausha vyema ili kuondoa unyevunyevu kwa sababu kuvaa nguo zisizokauka vizuri huweza kusababisha magonjwa kama mafua, kikohozi, baridi yabisi na fangasi;

(b) Huondoa mikunjokunjo na hivyo kufanya nguo zionekane nadhifu;

(c) Kuua wadudu na vimelea vya magonjwa; na

(d) Humuwezesha mvaaji kujisikia vizuri na kujiamini.

***Matayarisho ya kupiga pasi nguo:*** Fanya maandalizi ya vifaa utakavyotumia wakati wa kupiga pasi nguo. Vifaa vinavyotumika wakati wa kupiga pasi nguo ni kama: meza, blanketi, shuka, chombo chenye maji, farasi, pasi na kitundikio cha nguo. Tumia meza iliyotengenezwa kwa ubao usiong'arishwa ili kuepuka kuharibu mwonekano wa meza kutokana na joto la pasi. Iwapo hakuna meza unaweza kutumia mkeka uliotandazwa kwenye sakafu safi pamoja na nguo nzito. Aidha, unaweza kutumia ubao maalumu wa kupigia pasi kama inavyoonekana katika Kielelezo namba 2.



**Kielelezo namba 2:** *Matayarisho ya kupiga pasi nguo*
***Chanzo:*** *https://www.ravvie.com tarehe* 27/07/2019

***Mambo ya kuzingatia wakati wa kupiga pasi:*** Baadhi ya mambo ya kuzingatia wakati wa kupiga pasi ni kama ifuatavyo:

(a) Iwapo nguo ni za rangi, piga pasi upande wa ndani ya nguo tu kuepuka nguo kupauka;

FOR ONLINE USE ONLY

FOR ONLINE USE ONLY
DO NOT DUPLICATE

(b) Unapopiga pasi unapaswa kukandamiza nguo kiasi ili iweze kunyooka vema. Kandamiza pasi kutegemea aina ya kitambaa cha nguo yenyewe. Mathalani, nguo iliyotengenezwa kwa kitambaa kizito kama kaptura au sketi, kandamiza pasi kwa nguvu zaidi ili inyooke vizuri. Kama nguo imetengenezwa kwa kitambaa laini kama shati la shule la tetironi kandamiza pasi kidogo tu;

(c) Kiasi cha joto la pasi hutegemea aina ya kitambaa cha nguo inayohusika. Baadhi ya nguo zinahitaji pasi yenye joto kali na nyingine zinahitaji pasi yenye joto la kadiri. Mfano nguo za pamba huhitaji joto kali ukilinganisha na nguo za polista au nailoni ambazo huhitaji joto kiasi kidogo; na

(d) Kiasi kinachohitajika cha unyevunyevu katika nguo hutegemea aina ya kitambaa cha nguo inayopigwa pasi. Baadhi ya nguo zinapopigwa pasi lazima ziwe na unyevunyevu ili ziweze kunyooka vizuri kama nguo za pamba na kitani.

**Tanbihi**: Endapo nguo unazohitaji kupiga pasi zitakuwa zimekauka sana nyunyizia maji kiasi ili ziweze kuwa na unyevunyevu wa kutosha. Hii itasaidia kuondoa mikunjokunjo ya nguo kwa urahisi wakati wa kupiga pasi na kuonekana maridadi. Brashi laini au chupa yenye mfuniko uliofungwa sawasawa ambao umetobolewa vitundu hufaa kwa kunyunyizia maji. Kunja na viringisha vizuri kila nguo baada ya kunyunyiza maji ili ziweze kufyonza maji vizuri. Unaweza pia kutumia pasi ya umeme ya mvuke.

FOR ONLINE USE ONLY

## Utumiaji wa pasi ya mkaa

Iwapo unatumia pasi ya mkaa zingatia mambo yafuatayo:

(a) Pangusa pasi ili kuondoa vumbi au uchafu mwingine;

(b) Washa mkaa mpaka uwake kabisa. Mkaa unaweza kuwashwa katika pasi moja kwa moja au kwenye jiko la mkaa na kisha kuwekwa katika pasi;

(c) Tandika vizuri blanketi na shuka kwenye meza iliyoandaliwa kwa ajili ya kupigia pasi;

FOR ONLINE USE ONLY
DO NOT DUPLICATE

(e) Juu ya meza hiyo, weka farasi ya pasi, pia weka kitambaa cha kujaribisha joto la pasi;

(f) Ni muhimu kupima joto la pasi kabla ya kuanza kuitumia. Pasi ya mkaa haina chombo maalumu cha kurekebishia kiwango cha joto. Hivyo ni vema kujaribisha joto la pasi kwa kutumia kitambaa kinachoendana na nguo unayotaka kupiga pasi. Iwapo kitambaa kitaungua au kubadilika rangi, ujue kuwa pasi ina joto kali sana linaloweza kuunguza nguo inayopigwa pasi. Punguza joto la pasi kwa kutumia kitambaa chenye unyevunyevu kisha safisha kitako cha pasi. Iwapo kitambaa hakitapata alama yoyote ya kuungua, endelea kupiga pasi nguo; na

(g) Ukishamaliza kupiga pasi nguo, hakikisha unamwaga mkaa sehemu sahihi. Hifadhi pasi katika eneo safi na kavu. Hewa yenye unyevunyevu huweza kusababisha kutu kwenye kitako cha pasi na hatimaye kusababisha madoa katika nguo inayopigwa pasi.

.

### Utumiaji wa pasi ya umeme

Hii ni aina ya pasi inayotumia nishati ya umeme. Aina hii ya pasi inaweza kuwa pasi kavu au ya mvuke. Pasi ya umeme ni rahisi kutumia kwani kiasi cha joto kinaweza kupunguzwa au kuongezwa na mtumiaji kulingana na aina ya kitambaa. Kiasi cha joto katika pasi kimeoneshwa katika makundi matatu: joto dogo, joto la wastani na joto kali. Hakikisha unazima pasi mara baada ya kumaliza kupiga pasi kuepuka madhara na kupunguza gharama ya umeme. Chomoa pasi kwenye soketi ya umeme kwa ajili ya usalama.

### Pasi ya mafuta ya taa

Hii ni aina ya pasi inayotumia mafuta ya taa ambayo huwekwa kwenye kitanki kidogo kilichoambatishwa kwenye pasi. Hutumika zaidi kwenye maeneo ambayo hayana umeme japokuwa haitumiki sana kama pasi ya mkaa. Aina hii ya pasi ina kifaa cha kupunguza au kuongeza joto la pasi kulingana na aina ya kitambaa cha nguo inayopigwa pasi. Hakikisha unazima pasi baada ya kutumia na kuitunza sehemu safi na kavu ili kuepuka kupata kutu.

FOR ONLINE USE ONLY

FOR ONLINE USE ONLY
DO NOT DUPLICATE

## Usafishaji wa pasi

Kitako cha pasi huweza kuchafuka kutokana na kuyeyuka kwa nyuzi katika nguo. Hali hii husababisha uchafu kuganda kwenye kitako cha pasi. Uchafu huu usiposafishwa huchafua nguo zinazonyooshwa kwa kutumia pasi hiyo. Unaweza kutumia mojawapo ya njia zifuatazo kusafisha kitako cha pasi:

**(a) Kusafisha pasi kwa kutumia magadi soda**

i. Iwapo unatumia pasi ya umeme, hakikisha kuwa pasi imechomolewa kutoka kwenye soketi ya umeme. Iwapo pasi ni ya mvuke, hakikisha unamwaga maji yaliyomo kwenye pasi. Iwapo unatumia pasi ya mkaa hakikisha pasi haina mkaa ndani. Vilevile, hakikisha kuwa kitako cha pasi ambacho hutumika kupiga nguo pasi hakina joto.

ii. Changanya vijiko viwili vya chai vya magadi soda na maji robo kikombe kutengeneza uji mzito.

iii. Tumia kitambaa safi kupaka mchanganyiko wa magadi soda na maji kwenye maeneo machafu ya kitako cha pasi. Sugua taratibu kuondoa uchafu uliogandia.

iv. Futa pasi kwa kutumia kitambaa safi au brashi laini mpaka uchafu wote utoke.

v. Acha pasi ikauke kabla ya kuitumia.

**(b) Kusafisha pasi kwa kutumia makaratasi**

Pasha pasi moto mpaka iwe na joto kali kisha tumia karatasi kama vile magazeti kusugua uchafu mpaka uondoke. Njia hii si salama kutumiwa na watoto. Hakikisha unavaa glovu maalumu kuzuia joto lisikuunguze mikono.

**(c) Kusafisha pasi kwa kutumia siki au maji ya limau**

Tumbukiza kitambaa katika siki au maji ya limau kisha futa kitako cha pasi chenye uchafu kwa kutumia kitambaa hicho. Iwapo uchafu utabaki, tumbukiza kitambaa tena kwenye siki au maji ya limau kwa dakika 15-30 kisha tumia kitambaa hicho kusafishia pasi. Hakikisha pasi imekauka kabla ya kuitumia.

FOR ONLINE USE ONLY



Stadi za Kazi darasa la 6.indd 9 23/07/2021 15:11

FOR ONLINE USE ONLY
DO NOT DUPLICATE

**(d) Kusafisha pasi kwa kutumia chumvi**

Nyunyiza chumvi kwenye kipande cha karatasi. Chomeka pasi kwenye soketi ya umeme au koleza pasi ya mkaa kisha iache ipate joto kiasi. Pitisha pasi yenye joto juu ya kipande cha karatasi chenye chumvi mpaka uchafu wote utoke. Chomoa pasi kutoka kwenye soketi au mwaga mkaa kisha acha pasi ipoe. Safisha kitako cha pasi kwa kutumia kitambaa laini ambacho ni kikavu kuondoa uchafu uliosalia.

## Taratibu za upigaji nguo pasi

Upigaji pasi nguo unaweza kufuata taratibu zifuatazo:

(a) Anza kupiga pasi nguo nyepesi ambazo hazihitaji joto kali ili kutopoteza nishati inayotumika;

(b) Ikiwa ni nguo yenye mng’ao, piga pasi kwa upande wa ndani na kama haina mng’ao piga pasi kwa upande wa nje kwanza;

(c) Unapopiga pasi nguo, anza na sehemu zote zilizo maradufu kama vile sijafu, majongo, yoki na pindo isipokuwa ukosi;

(d) Piga pasi ukosi baada ya kumaliza kupiga pasi nguo yote;

(e) Piga nguo pasi sehemu zilizodariziwa au zenye picha kwa upande wa ndani. Hii itasaidia kuepuka kupauka kwa nyuzi zilizodarizia nguo au kuharibika kwa rangi zilizotumika kuchorea picha;

(f) Geuza nguo na piga pasi nguo yote kwa upande wake wa nje;

(g) Piga kwa kufuata nyuzi za mtande; na

(h) Ikiwa nguo ina marinda ya kupanga piga pasi yalale bapa.

## Kutundika nguo baada ya kupiga pasi



Fikiri
Ni kwa nini unashauriwa kutundika nguo mara baada ya kupiga pasi?



Stadi za Kazi darasa la 6.indd 10 23/07/2021 15:11

FOR ONLINE USE ONLY

FOR ONLINE USE ONLY
DO NOT DUPLICATE

Nguo zilizonyunyizwa maji wakati wa kupiga pasi huonekana zimekauka na kunyooka vizuri. Hata hivyo, ni muhimu nguo zitundikwe mahali penye hewa ya kutosha ili zikauke vizuri kwani wakati mwingine nyuzi za kitambaa zinakuwa bado zina unyevunyevu. Vilevile, joto la pasi likipoa husababisha unyevunyevu katika nyuzi za kitambaa. Hivyo, mara baada ya kupiga pasi nguo zitundike mahali penye hewa ya kutosha ili zikauke vizuri. Unaweza pia kutandaza nguo katika meza au sehemu safi ili zipate hewa. Iwapo utakunja nguo mara tu baada ya kupiga pasi, unyevunyevu uliobakia katika nguo huweza kusababisha mikunjokunjo na kuonekana kama hazikupigwa pasi vizuri. Vilevile, zinaweza zikawa na harufu ya uvundo au kupata madoa ya kuvu.

## Kukunja nguo



Jadiliana katika kikundi na wenzako

Kuna umuhimu gani wa kukunja nguo baada ya kupiga pasi?

Kukunja nguo husaidia kuepusha kukunjamana wakati zinapokuwa sandukuni au kabatini. Nguo zilizokunjwa na kuhifadhiwa vizuri huweza kuvaliwa bila kuhitaji kupigwa pasi tena. Baada ya kukamilisha kazi ya kunyoosha nguo unaweza kufanya yafuatayo:

(a) Kunja nguo na weka vizuri sandukuni au kabatini;

(b) Iwapo una kabati maalumu la kuweka nguo zikiwa zimetundikwa, acha nguo katika vitundikio, kisha zitundike vizuri kabatini; na

(c) Iwapo huna kabati la aina hiyo unaweza kutundika nguo mahali maalumu kwa mpangilio mzuri.

***Utaratibu wa kukunja nguo:*** Yafuatayo ni baadhi ya mambo muhimu unayopaswa kuzingatia wakati wa kukunja nguo:

i. Anza kukunja nguo kwa kufuata marefu yake kisha ikunje kwa mapana yake kama inavyoonekana katika Kielelezo namba 3. Kunja nguo kutegemeana na aina ya nguo mfano shati, suruali, gauni au sketi; na


FOR ONLINE USE ONLY



Stadi za Kazi darasa la 6.indd 11 23/07/2021 15:11

FOR ONLINE USE ONLY
DO NOT DUPLICATE

ii. Iwapo kuna sehemu fulani ya nguo ina marinda kwa mfano mikononi, tumboni au kifuani yatengeneze vizuri ili yalale bapa mithili ya marinda ya kupanga.



**Kielelezo namba 3:** *Ukunjaji wa nguo*
*http://rcmodels-hmao.ru/uyut/315-kak-slozhit-rubashku-chtoby-ona-ne-pomyalas-poleznye-sovety.html*

### Kazi ya kufanya namba 2

Katika vikundi, andaeni eneo la kupigia nguo pasi kisha mpige pasi sare za shule kwa kufuata utaratibu mliojifunza.

FOR ONLINE USE ONLY



Stadi za Kazi darasa la 6.indd 12 23/07/2021 15:11

FOR ONLINE USE ONLY
DO NOT DUPLICATE

**Zoezi la pili**

**Jibu maswali yafuatayo**

1. Utapata madhara gani iwapo utavaa nguo ambazo hazijakauka vizuri?
2. Taja sehemu tano zilizo maradufu katika nguo.
3. Kwa nini ni muhimu kunyunyiza nguo maji kabla ya kuzipiga pasi?
4. Kwa nini nguo zilizonyunyiziwa maji zinatundikwa baada ya kupiga pasi? Taja sababu mbili.
5. Eleza sababu tatu za kupiga nguo pasi.

## Utunzaji wa viatu

Viatu ni mojawapo ya vazi muhimu kwa binadamu. Viatu vina umuhimu mkubwa katika kulinda miguu kutokana na matope, baridi, wadudu hatarishi, kuumia kwa kuchomwa na vitu vyenye ncha kali kama vile pini. Uvaaji wa viatu unaweza pia kuepusha miguu kupasuka. Hali kadhalika ukivaa viatu safi unaonekana nadhifu na mwenye kujiamini. Viatu hutengenezwa kutokana na makunzi ya aina mbalimbali kama vile mpira, plastiki, ngozi na turubali. Hivyo, usafishaji na uhifadhi wa viatu hutegemea aina ya makunzi yaliyotumika kutengeneza viatu. Ni vema ukazingatia utaratibu wa usafishaji, uanikaji na uhifadhi wa viatu kulingana na makunzi yaliyotumika kutengeneza viatu.

## Uchaguzi wa viatu

Unapochagua viatu hakikisha unachagua viatu vinavyokutosha vizuri kwa kuwa viatu vinavyobana vinaweza kuzuia mzunguko mzuri wa damu mwilini. Nunua viatu imara ambavyo vitadumu kwa muda mrefu.Chagua viatu kulingana na matumizi yaliyokusudiwa, mfano viatu vya ngozi kwa matumizi ya kila siku kama kwenda ofisini, shuleni na michezo. Viatu vigumu na vyenye kisigino kirefu sio sahihi kwa matumizi ya kila siku. Uvaaji wa viatu hivi huweza kusababisha misuli kujivuta, hivyo kujisikia kuchoka au

FOR ONLINE USE ONLY



Stadi za Kazi darasa la 6.indd 13 23/07/2021 15:11

FOR ONLINE USE ONLY
DO NOT DUPLICATE

kuhisi maumivu ya misuli ya miguu na mgongo. Aidha, unashauriwa kuvaa viatu pamoja na soksi zilizotengenezwa kwa pamba ili kusaidia kufyonza jasho linalotoka kwenye miguu na hivyo kuwa mikavu.

**Usafishaji wa viatu:** Ni muhimu kusafisha viatu mara kwa mara kwa kuzingatia aina ya makunzi yaliyotumika kutengenezea viatu hivyo ili viweze kudumu kwa muda mrefu. Safisha viatu mara vinapochafuka kwa kuwa vikichafuka sana utatumia nguvu kuvisugua hivyo huweza kuchanika au kuharibu mwonekano wake. Vilevile, ni muhimu kusafisha viatu ili kuondoa uchafu unaoweza kusababisha harufu mbaya na magonjwa ya ngozi kama fangasi kwenye miguu.

***(a) Kusafisha viatu vya turubali:*** Fuata hatua zifuatazo kusafisha viatu vya turubali:

(i) Ondoa bitana na gidamu kisha zisafishe tofauti na viatu ili zitakate vizuri kama inavyoonekana katika Kielelezo namba 4;

(ii) Safisha viatu kwa kutumia brashi ya kusafishia viatu na sabuni kuondoa uchafu. Iwapo hakuna brashi unaweza kutumia gunzi;

(iii) Suuza viatu vizuri kwa kutumia maji safi;

(iv) Iwapo viatu hivyo ni vyeupe, paka rangi nyeupe ili ving’ae;

(v) Anika viatu sehemu ya wazi yenye hewa ya kutosha ili vikauke. Rudisha bitana na gidamu; na

(v) Tunza viatu vilivyokauka vizuri katika sehemu au eneo ambalo ni kavu.



**Kielelezo namba 4**: *Bitana na gidamu zilizotenganishwa na viatu*

FOR ONLINE USE ONLY

FOR ONLINE USE ONLY
DO NOT DUPLICATE

*(b)* ***Kusafisha viatu vya plastiki***: Usafishaji wa viatu vya plastiki ni rahisi ukilinganisha na viatu vilivyotengenezwa kwa turubali au ngozi. Kung'uta uchafu, vumbi na ondoa tope kama lipo kwenye viatu. Osha kwa kutumia maji yenye sabuni hadi viatu viwe safi. Tumia brashi kusugua uchafu uliong'ang'ania, kisha suuza kwa maji safi kuhakikisha uchafu wote umetoka. Anika viatu katika eneo ambalo halina jua kali kuepuka kuharibu mwonekano wake.

*(c)* ***Kusafisha viatu vya ngozi***: Viatu vya ngozi visafishwe mara kwa mara ili vionekane vinang'aa na kupendeza. Viatu vya ngozi husafishwa kwa kufuta vumbi au matope, kupaka rangi kisha kung'arishwa. Epuka kuweka viatu vya ngozi kwenye maji kwani vitaharibika mwonekano wake. Vifaa vinavyoweza kutumika kusafisha viatu ni pamoja na: brashi ya kupakia rangi na brashi ya kung'arisha viatu, maji, kitambaa na kipande cha sponji na rangi ya viatu.

***Hatua za kusafisha viatu vya ngozi:*** Viatu vilivyong'arishwa vinapendeza na vinadumu kwa muda mrefu vikiwa na mwonekano mzuri. Hakikisha unazingatia hatua zifuatazo wakati wa kusafisha viatu vya ngozi:

(i) Ondoa bitana ya viatu iwapo inawezekana kufanya hivyo;

(ii) Ondoa matope kama yapo kwa kutumia kitambaa chenye unyevunyevu;

(iii) Pangusa viatu kwa kitambaa kuondoa vumbi;

(iv) Tumia brashi laini kuondoa vumbi lote lililobaki kwenye viatu;

(v) Paka viatu rangi kwa kutumia brashi. Hakikisha unapaka rangi kwenye ngozi na sehemu za pembeni mwa soli ya kiatu;

(vi) Anika viatu sehemu ya wazi yenye hewa ya kutosha ili mwonekano wake usiharibike;

(vii) Ng'arisha viatu kwa kutumia brashi laini zaidi ambayo hutumika kwa ajili ya kung'arisha viatu;

(viii) Tumia kipande cha sponji kisichokuwa na unyevunyevu kung'arisha viatu; na

(ix) Ingiza kwa kusokomeza vitambaa au magazeti kwenye viatu kisha tunza sehemu sahihi isiyokuwa na majimaji au unyevunyevu.

FOR ONLINE USE ONLY



Stadi za Kazi darasa la 6.indd 15 23/07/2021 15:11

FOR ONLINE USE ONLY
DO NOT DUPLICATE

## Kazi ya kufanya namba 3

Safisha viatu ukifuata hatua ulizojifunza kulingana na makunzi yaliyotumika kutengeneza viatu hivyo.

## Zoezi la 3

**A. Jibu maswali yafuatayo kwa kujaza nafasi zilizoachwa wazi ukitumia daftari lako la mazoezi**

1. Pasi ni kifaa kinachotumika ........................................................................
2. Makunzi yanayotumika kutengeneza viatu ni.................................
3. Viatu vyeupe kung’arishwa kwa kutumia rangi..............................
4. Nguo huweza kuchafuliwa na................, ................ na ..............
5. Bitana ya viatu ni...........................................................................
6. Farasi ni.......................................................................................

**B. Chagua jibu sahihi na uandike herufi yake katika daftari lako la mazoezi**

1. Maji yaliyochanganywa na chumvi yanafaa kuondoa madoa yenye:
   (a) Asili ya wanyama mfano damu
   (b) Asili ya matope
   (c) Asili ya kemikali mfano wino
   (d) Asili ya vyakula

2. Mwonekano mbaya wa rangi ya nguo unaweza kusababishwa na
   (a) Kuzitenganisha wakati wa kuziloweka
   (b) Kutozitenganisha wakati wa kuziloweka
   (c) Kuzikamua nguo
   (d) Kuzifua usiku na mchana

FOR ONLINE USE ONLY



Stadi za Kazi darasa la 6.indd 16 23/07/2021 15:11

FOR ONLINE USE ONLY
DO NOT DUPLICATE

3. Ni nguo zipi huhitaji joto kali wakati wa kupiga pasi?
   (a) Polista na kitani
   (b) Nailoni na pamba
   (c) Kitani na nailoni
   (d) Pamba na kitani

4. Ni aina gani ya pasi huonesha kiasi cha joto katika makundi matatu, joto dogo, joto la wastani na joto kali.
   (a) Pasi ya mkaa
   (b) Pasi yoyote
   (c) Pasi ya mafuta ya taa
   (d) Pasi ya umeme

5. Kwa nini unashauriwa kupiga pasi kwanza nguo ndogondogo kama vile leso wakati pasi haijawa na joto kali?
   (a) Kuepuka kuunguza nguo kwa urahisi
   (b) Leso ni bora kuliko nguo zingine
   (c) Nguo hizo hazihitaji joto kali
   (d) Hutumika kama kipozeo cha pasi

6. Viatu vyenye kisigino kirefu huweza kusababisha
   (a) Maumivu ya kichwa
   (b) Maumivu ya magoti
   (c) Maumivu ya misuli
   (d) Maumivu ya tumbo

7. Uvaaji wa soksi za pamba husaidia
   (a) Kunyonya jasho la miguu
   (b) Kupunguza joto la miguu
   (c) Kutembea vizuri
   (d) Kuzuia kuteleza

FOR ONLINE USE ONLY

FOR ONLINE USE ONLY
DO NOT DUPLICATE

8. Kwa nini unashauriwa kutundika nguo zilizonyunyiziwa maji baada ya kupiga pasi?
   (a) Nyuzi ziweze kukauka vizuri
   (b) Kuzifanya nguo zipendeze
   (c) Kuondoa harufu mbaya
   (d) Kuzinyoosha vizuri zaidi

9. Kuna umuhimu gani kuzima pasi baada ya kutumia?
   (a) Kuepuka kuunguza nguo
   (b) Kuzuia kutu kwenye uso wa pasi
   (c) Kuiwezesha kudumu kwa muda mrefu
   (d) Kuepuka madhara na gharama

10. Kwa nini hairuhusiwi kuweka viatu vya ngozi katika maji?
   (a) Vinaweza kupauka
   (b) Vitaharibika mwonekano wake
   (c) Vitayeyuka kwa urahisi
   (d) Vitatoa harufu mbaya

**C. Jibu maswali yafuatayo kwa kuandika majibu yake katika daftari lako la mazoezi**

1. Taja njia tatu unazoweza kutumia kunyunyiza maji kwenye nguo kavu wakati wa kupiga pasi.
2. Eleza hatua unazopaswa kufuata unaposafisha viatu vilivyotengenezwa kwa makunzi ya ngozi.
3. Ainisha sababu tatu za kuvaa viatu.
4. Ni madhara gani yanayoweza kutokea iwapo viatu havitasafishwa?
5. Eleza mambo unayopaswa kuzingatia ili kuhakikisha kuwa viatu vinadumu kwa muda mrefu.

FOR ONLINE USE ONLY



Stadi za Kazi darasa la 6.indd 18 23/07/2021 15:11

FOR ONLINE USE ONLY
DO NOT DUPLICATE

6. Eleza namna ya kutoa madoa ya aina zifuatazo katika nguo
   (a) Madoa yatokanayo na vyakula
   (b) Madoa yenye asili ya kemikali
7. Taja njia tano zinazotumika kusafisha kitako cha pasi iliyochafuka.
8. Eleza sababu ya kusafisha bitana na gidamu tofauti na viatu.

## Msamiati

| | |
|---|---|
| **Bitana** | Kifaa kinachowekwa ndani ya kiatu sehemu ya unyayo |
| **Farasi** | Kifaa kinachotumika kuwekea pasi wakati wa kupiga pasi nguo |
| **Gidamu** | Kamba za kufungia viatu |
| **Kitani** | Nyuzi zinazotokana na gome la mti wenye asili ya India ambazo hutumika kutengeneza vitu kama magunia, nguo mazulia na kamba. Zina tabia zinazofanana na nyuzi za pamba. |
| **Majongo** | Sehemu inayotokea baada ya kuunganisha vitambaa viwili kwa uzi na sindano |
| **Sijafu** | Pindo katika mkono wa shati au koti linaloshonewa kwa nje. |
| **Yoki** | Sehemu ya nguo eneo la kifua au mabega ambalo huwa linashonwa kwa kutumia vitambaa maradufu. Mara nyingi huwa katika nguo za watoto. |

FOR ONLINE USE ONLY



Stadi za Kazi darasa la 6.indd 19 23/07/2021 15:11

FOR ONLINE USE ONLY
DO NOT DUPLICATE

# Sura ya Pili

## Utunzaji wa mazingira

### Utangulizi

*Ulipokuwa Darasa la Tano, ulijifunza kuhusu usafi wa makazi na namna ya kusafisha aina mbalimbali za sakafu. Vilevile, ulijifunza namna ya kufanya usafi sehemu ya kulala na namna ya kuhifadhi taka. Katika sura hii, utajifunza namna ya kutunza viunga vya nyasi pamoja na bustani za maua na mboga. Pia, utajifunza jinsi ya kudhibiti taka zenye asili ya kuoza mapema, matumizi mbadala ya taka, urejelezaji na usalama katika kuhifadhi taka hizo. Aidha, utajifunza namna ya kuhifadhi taka zisizofaa kutumika hasa taka za sumu. Kujifunza kutunza mazingira, kutakuwezesha kulinda afya yako na ya jamii kwa ujumla. Shughuli za utunzaji wa mazingira utakazojifunza utaweza pia kuzitumia kama fursa za biashara na kupata kipato chenye faida.*

FOR ONLINE USE ONLY

### Umuhimu wa kutunza nyasi, maua na mboga katika mazingira



Fikiri
Je, nyasi, maua na mboga zina umuhimu gani katika mazingira yetu?

Mazingira ni jumla ya vitu vyote vinavyomzunguka binadamu, mfano milima, mabonde, mito, bahari, majengo ya makazi au shule, maeneo yote yanayozunguka majengo hayo pamoja na vitu vingine. Mazingira huvutia na huwa na manufaa zaidi endapo yatatunzwa vizuri. Mazingira ya shuleni au nyumbani yanapaswa kuwa na viunga vinavyotunzwa vema. Ikiwa viunga havikuwekewa sakafu au vigae ni vyema kutunzwa kwa kupandwa nyasi kama vile ukoka. Hii husaidia kuzuia vumbi na mmomonyoko wa udongo.



Stadi za Kazi darasa la 6.indd 20 23/07/2021 15:11

FOR ONLINE USE ONLY
DO NOT DUPLICATE

Nyasi pia hupendezesha viunga na kuzuia kuwepo kwa matope na madimbwi ya maji wakati wa mvua. Bustani za maua nazo ni muhimu kuwepo katika mazingira ya nyumbani au shuleni. Maua yana faida mbalimbali katika mazingira yetu, mfano hupendezesha mazingira na huwavutia nyuki wa asali pamoja na wadudu wengine kama vipepeo wanaochavusha mimea. Faida nyingine ya maua ni kuongeza ajira na kuwapatia watu kipato. Maua pia hutumika kupamba maeneo mbalimbali. Vilevile, ni muhimu kuwa na bustani za mboga katika mazingira ya nyumbani pamoja na shuleni. Bustani za mboga huwezesha kupata mahitaji ya mboga kwa urahisi. Mboga hutupatia vitamini na madini ambayo hulinda miili yetu. Hali kadhalika, iwapo bustani ni kubwa, ziada ya mboga zinazopatikana huweza kuuzwa na kusaidia kuongeza kipato.

## Utunzaji wa viunga vya nyasi

Viunga vya nyasi katika mazingira yetu vinapaswa kutunzwa vyema. Mambo yafuatayo yanatakiwa kuzingatiwa katika kutunza viunga vya nyasi.

1. Kufyeka nyasi ili kuepuka nyoka, panya na wadudu waharibifu kufanya maskani yao. Nyasi ndefu pia ni mazalia na makazi ya wadudu kama mbu.
2. Kumwagilia maji hasa wakati wa kiangazi ili nyasi zisikauke.
3. Kung'oa magugu katika nyasi ili kuzipa nafasi ya kukua vizuri na kuwa na mwonekano wa kupendeza.
4. Kupanda nyasi mpya iwapo zilizopo zimechakaa.
5. Kuweka njia za kupita ili kuepuka kukanyaga nyasi ovyo.
6. Kutunza nyasi vizuri ili kuzikinga dhidi ya wadudu waharibifu pamoja na magonjwa. Unaweza kutumia viuatilifu au kung'oa na kuangamiza nyasi zenye magonjwa kisha kupanda nyingine.


FOR ONLINE USE ONLY



Stadi za Kazi darasa la 6.indd 21 23/07/2021 15:11

FOR ONLINE USE ONLY
DO NOT DUPLICATE

Tazama Kielelezo namba 1 kuona mfano wa viunga vya nyasi vinavyotunzwa katika mazingira ya shule.




**Kielelezo namba 1:** *Mwonekano wa viunga vya nyasi shuleni*

## Kazi za kufanya namba 1

1. Fanya uchunguzi katika viunga vya nyasi kwenye mazingira ya shule na nyumbani ili kubaini endapo mambo yote muhimu katika utunzaji wake yanazingatiwa.
2. Tunza viunga vya nyasi shuleni na nyumbani kwa kuzingatia mambo yote muhimu uliyojifunza.
3. Andaa taarifa ya namna ulivyotunza viunga vya nyasi shuleni na nyumbani, bainisha changamoto zilizojitokeza na namna ulivyokabiliana nazo. Wasilisha taarifa hiyo darasani.

FOR ONLINE USE ONLY



Stadi za Kazi darasa la 6.indd 22 23/07/2021 15:11

FOR ONLINE USE ONLY
DO NOT DUPLICATE

## Utunzaji wa bustani za maua

Yafuatayo ni baadhi ya mambo muhimu ya kuzingatia katika kutunza bustani za maua.

1. Kupanda maua ya kutosha katika mpango mzuri.
2. Kuepuka kuwa na msongamano wa miti ya maua karibu na nyumba ili yasizuie madirisha kuingiza hewa na mwanga wa kutosha.
3. Kwa eneo lenye mwinuko, inapaswa kutayarisha matuta kukinzana na mwinuko ili kupunguza kasi ya mmomonyoko wa udongo.
4. Kupalilia ili kuondoa magugu, pia kuinulia udongo kwa namna itakayosaidia kutunza maji wakati yanapomwagiliwa.
5. Kupogolea maua ili kuondoa matawi na majani yaliyochakaa au yasiyohitajika.
6. Kung'oa maua yaliyozeeka au yasiyohitajika.
7. Kumwagilia maji endapo unyevunyevu katika udongo hautoshi hasa wakati wa kiangazi. Ni vyema kumwagilia mapema asubuhi na wakati wa jioni ili kuepuka upotevu wa maji kutokana na mvukizo.
8. Kukinga maua dhidi ya wadudu waharibifu pamoja na magonjwa kwa kutumia njia na mbinu stahiki. Mfano, kung'oa maua yaliyoathiriwa na magonjwa na kuyaangamiza kisha kupanda mengine. Hii itazuia au kupunguza kasi ya kuenea kwa ugonjwa husika. Unaweza pia kutumia viuatilifu vinavyostahili.
9. Kutafuta ushauri kutoka kwa wataalamu wa kilimo ili uweze kutunza vizuri bustani za maua.

FOR ONLINE USE ONLY



Stadi za Kazi darasa la 6.indd 23 23/07/2021 15:11

FOR ONLINE USE ONLY
DO NOT DUPLICATE

Tazama Kielelezo namba 2 kuona mfano wa bustani za maua zinazotunzwa vyema katika mazingira ya nyumbani.



**Kielelezo namba 2:** *Mwonekano wa bustani za maua nyumbani*

### Kazi za kufanya namba 2

1. Fanya uchunguzi wa bustani za maua zilizopo shuleni na nyumbani ili kubaini endapo mambo yote muhimu katika utunzaji wake yanazingatiwa.
2. Tunza bustani za maua shuleni na nyumbani kwa kuzingatia mambo yote muhimu uliyojifunza.
3. Andaa taarifa ya namna ulivyotunza bustani za maua, bainisha changamoto zilizojitokeza na namna ulivyokabiliana nazo. Wasilisha taarifa hiyo darasani.

FOR ONLINE USE ONLY



Stadi za Kazi darasa la 6.indd 24 23/07/2021 15:12

FOR ONLINE USE ONLY
DO NOT DUPLICATE

## Utunzaji wa bustani za mboga

Mboga zinaweza kupandwa moja kwa moja katika bustani au kwa kuzalisha miche kwenye kitalu na kisha baadaye kupandikiza miche katika matuta au bustani.

***Mambo yanayoweza kuzingatiwa katika kutunza kitalu cha miche ya mboga:***

1. Kuchagua sehemu yenye udongo tifutifu kwa ajili ya kuandaa kitalu. Epuka eneo linalotuamisha maji.
2. Kudhibiti eneo la kitalu dhidi ya uharibifu wa wanyama wa porini au wanaofugwa kwa kulizungushia wigo.
3. Kutayarisha kitalu na kusia mbegu za mboga.
4. Kudhibiti jua kali katika kitalu kwa kuweka kichanja au kivuli cha miti. Unaweza pia kuweka urefu wa kitalu kuelekea mashariki na magharibi ili miche mingi isidhurike na jua linalochomoza pembeni mwa kitalu.
5. Kufanya uzoeshaji wa miche kabla ya kuihamisha ili iweze kustahimili mshituko wa upandikizaji. Uzoeshaji unafanywa kwa kuipa miche mazingira magumu kiasi ambacho huzuia ukuaji wa haraka wa miche hiyo. Punguza polepole kiasi cha maji unachomwagilia pamoja na vipindi vya umwagiliaji kwa siku. Fanya hivyo kwa siku 7 hadi 10 kabla ya kupandikiza.

***Mambo ya kuzingatia katika utunzaji wa bustani ya mboga:***

1. Kuzungushia wigo eneo la bustani ya mboga ili kuzuia wanyama wa porini au wanaofugwa wasiharibu mimea hiyo.
2. Kusafisha eneo na kutayarisha matuta. Wakati wa mvua nyingi, tayarisha matuta mbinuko au yaliyoinuka juu ya usawa wa ardhi. Matuta ya aina hii husaidia kuzuia mizizi ya mimea isiharibiwe na maji mengi yanayosababisha kukosekana kwa hewa ndani ya udongo. Wakati wa kiangazi au katika sehemu kame, tayarisha matuta mbonyeo au yaliyo chini ya usawa wa ardhi ili kusaidia kutunza maji. Mahali ambapo hapana uhaba wa maji wala tatizo la udongo kutuamisha maji, unaweza kutumia matuta yaliyo usawa wa ardhi. Kwa maeneo yenye uhaba wa ardhi kama mijini, mboga zinaweza kuoteshwa katika mifuko ya salfeti,

FOR ONLINE USE ONLY

FOR ONLINE USE ONLY
DO NOT DUPLICATE

makopo au vyombo vingine vya aina mbalimbali kama inavyooneshwa katika Kielelezo namba 3.

3. Kupandikiza miche katika matuta kwa njia sahihi na wakati unaofaa. Inafaa zaidi upandikize mwanzoni mwa kipindi cha mvua endapo huna maji ya kumwagilia. Hata hivyo, baadhi ya mboga mfano nyanya, pilipili na biringanya hustawi zaidi wakati wa kiangazi. Hii ni kwa sababu nyakati hizo magonjwa hasa ya majani, hupungua kwa kiasi kikubwa. Kipindi kinachofaa zaidi kwa upandikizaji ni kile cha ubaridi kidogo, hasa siku ya mawingu. Kama siku hiyo haiwezi kupatikana, pandikiza wakati wa jioni. Hii ni kwa sababu mvukizo ni kidogo hivyo utawezesha miche kuanza vizuri maisha mapya katika mazingira mapya.

4. Kupandikiza miche ya mboga zenye mizizi nyuzi, mfano vitunguu maji na vitunguu saumu inapofikisha wiki 4 hadi 6. Wakati huo miche itakuwa na majani halisi au kufikia urefu wa sentimeta 13 hadi 25. Pandikiza miche ya mboga zenye mizizi mikuu kabla ya kuwa na majani sita, kabla mizizi mikuu haijakua sana.

5. Kumwagilia maji ya kutosha hasa msimu wa kiangazi. Unashauriwa kumwagilia mapema asubuhi na wakati wa jioni ili kuepuka upotevu wa maji kutokana na mvukizo. Mimea imwagiliwe kwa chini tu na kamwe maji yasiguse majani ya mimea. Umwagiliaji wa namna hii unapunguza mazingira yanayochochea magonjwa ya majani.

6. Kupunguzia miche pale inapolazimika ili kila mmea upate nafasi ya kutosha. Hii inahusu zaidi zile mboga ambazo hupandwa moja kwa moja kwenye bustani bila kuanzia kwenye kitalu.

7. Kudhibiti magugu kwa kupalilia ama kwa kutumia viuatilifu. Wakati wa kupalilia inulia udongo kwenye mimea ili kuboresha ukuaji na uimara wa mimea.

8. Kuweka matandazo inapostahili ili kuhifadhi maji hasa wakati wa kiangazi. Matandazo yanaweza kukupa faida nyingine nyingi, mfano kupunguza uotaji wa magugu hasa yenye majani mapana pamoja na kuongeza rutuba kwenye udongo pale yanapooza.

9. Kuweka mbolea kama vile samadi au mboji ili kustawisha mboga. Unaweza pia kutumia mbolea za kisasa kama vile chumvichumvi endapo huna samadi au mboji.

FOR ONLINE USE ONLY

FOR ONLINE USE ONLY
DO NOT DUPLICATE

10. Kuweka mategemezo kulingana na aina ya mboga, mfano nyanya, maboga, na maharage yanayokwea. Mategemezo huwezesha mboga zinazozaa matunda kusimama wima hivyo kutokugusa udongo. Hii huepusha matunda hayo kupata magonjwa hasa yale yenye asili ya udongo.

11. Kudhibiti wadudu waharibifu na magonjwa pindi inapohitajika.

12. Kuvuna kwa wakati unaofaa kwa ajili ya matumizi yako au kuuza.

Tazama Kielelezo namba 4 kuona mfano wa bustani ya mboga inayotunzwa katika mazingira ya shule.

***Angalizo:*** *Unaweza kutafuta ushauri kutoka kwa wataalamu wa kilimo ili uweze kutunza bustani yako ya mboga ipasavyo. Tafuta ushauri huo kuanzia wakati wa matayarisho ya kupanda hadi kuvuna. Kumbuka kwamba ukitunza vema mimea yako, itakua vizuri na hatimaye utapata mavuno bora na mengi.*



**Kielelezo namba 3:** *Bustani za mboga kwenye vifaa vilivyokwishatumika*



**Kielelezo namba 4:** *Bustani ya mboga*



Stadi za Kazi darasa la 6.indd 27 23/07/2021 15:12

FOR ONLINE USE ONLY

FOR ONLINE USE ONLY
DO NOT DUPLICATE

### Kazi za kufanya namba 3

1. Fanya uchunguzi katika bustani za mboga zilizopo mazingira ya shuleni na nyumbani ili kubaini endapo mambo yote muhimu katika utunzaji wake yanazingatiwa.
2. Undeni vikundi kisha mtengeneze matuta mawili ya bustani. Tuta moja lenye miche yenye mzizi mkuu na tuta lingine lenye miche yenye mizizi nyuzi. Tunzeni matuta hayo kwa kufuata kanuni zote za utunzaji wa bustani za mboga.
3. Andaeni taarifa ya namna mlivyotunza bustani za mboga, bainisheni changamoto zilizojitokeza na namna mlivyokabiliana nazo. Wasilisheni taarifa hiyo darasani.

### Zoezi la kwanza

**Jibu maswali yafuatayo kwa kuandika majibu yake kwenye daftari lako la mazoezi.**

1. Taja aina tatu za matuta.
2. Eleza aina kuu mbili za upandaji wa mbegu za mboga.
3. Taja faida tatu za maua katika mazingira.
4. Eleza njia mbili za kudhibiti jua kali katika kitalu cha miche.
5. Eleza sababu ya uzoeshaji wa miche kabla ya kuihamisha kwa ajili ya kupandikiza.
6. Bainisha mambo matatu ya kuzingatia katika umwagiliaji wa bustani ya mboga au maua.

FOR ONLINE USE ONLY



Stadi za Kazi darasa la 6.indd 28 23/07/2021 15:12

FOR ONLINE USE ONLY
DO NOT DUPLICATE

## Udhibiti wa taka



Fikiri

1. Zipi ni taka zinazooza na zipi ni taka zisizooza katika mazingira ya shule na nyumbani kwenu?
2. Namna gani taka hizo zinadhibitiwa?
3. Ni zipi athari za kutodhibiti taka hizo kwa njia sahihi?

Katika shughuli zetu za kila siku, tunazalisha taka za aina mbalimbali. Kuna taka zenye asili ya kuoza mapema, taka ngumu zenye asili ya kutooza mapema na taka zisizooza. Udhibiti wa taka hizi unatofautiana. Udhibiti wa taka unaanza kwa kuzichambua kulingana na makundi yake kisha kuendelea na hatua nyingine za udhibiti. Tazama Kielelezo namba 5 kuona namna taka zinavyotakiwa kuchambuliwa kabla ya hatua nyingine za udhibiti. Iwapo taka hazitadhibitiwa ipasavyo huweza kuchafua mazingira na kusababisha vimelea vya magonjwa ambavyo vinaweza kuathiri afya zetu. Baadhi ya taka ni hatari kwetu na kwa mazingira yetu hivyo huhitaji kudhibitiwa kwa uangalifu mkubwa. Hata hivyo, baadhi ya taka zikidhibitiwa ipasavyo zitaweza kuwa za manufaa katika mazingira yetu.




**Kielelezo namba 5:** *Taka zilizochambuliwa na kuhifadhiwa kwa usahihi*

Ili kutunza mazingira vyema, tunashauriwa kuzingatia mambo muhimu yafuatayo katika kudhibiti taka: (a) kupunguza au kuepuka kuzalisha taka, (b) kuzipa taka matumizi mbadala, (c) kubadili taka ili kupata bidhaa zitakazotufaa tena yaani kuzirejeleza (d) kuzitupa ama kuzihifadhi kwa kuzingatia kanuni za usalama.

FOR ONLINE USE ONLY



Stadi za Kazi darasa la 6.indd 29 23/07/2021 15:12

FOR ONLINE USE ONLY
DO NOT DUPLICATE

### Udhibiti wa taka kwa kupunguza au kuepuka kuzizalisha

Udhibiti huu unalenga kupunguza matumizi ya vitu vinavyogeuka kuwa taka baada ya kutumika. Hii ni kwa kuwa taka zilizopo nyumbani, shuleni, vijijini na mitaani kwetu huanzia katika shughuli zetu za kila siku. Hivyo, kuepuka au kupunguza kuzalisha taka katika shughuli zetu za kila siku ni jambo muhimu. Zifuatazo ni baadhi ya njia za kupunguza kuzalisha taka.

1. Kutonunua vitu vilivyofungwa katika vifungashio vingi.
2. Kuchagua vitu vyenye asili ya kioo au glasi na mbao kuliko plastiki na chuma.
3. Kutumia mfuko au kikapu kubebea vitu hasa unapokwenda kununua bidhaa dukani au sokoni. Hii itakuwezesha kuepuka vifungashio dhaifu na vya muda mfupi vinavyotolewa na wafanyabiashara ambavyo huchangia kuongeza taka.

Aidha, udhibiti huu ni salama kwa kuwa hutuepusha na athari zinazotokana na kuwepo kwa taka katika mazingira yetu.

### Udhibiti wa taka zenye asili ya kuoza mapema

Taka hizi ni zile zinazotokana na viumbe hai ikiwepo mimea na wanyama. Kwa kuwa taka hizi zina asili ya kuoza mapema, zinatakiwa kufukiwa ili kutunza mazingira pamoja na afya zetu. Taka hizi zisipodhibitiwa vizuri huchafua mazingira na kuharibu mwonekano wake. Zinaweza pia kutoa harufu mbaya au kuvutia wadudu wanaoeneza magonjwa, mfano nzi. Taka hizi zinaweza kufukiwa ardhini. Zingatia hatua zifuatazo unapofukia taka hizi:

1. Hakikisha taka hizi zimechambuliwa ili kuzitenga na zile zisizooza mapema;
2. Chimba shimo la kutosha kulingana na wingi wa taka unazotaka kufukia;
3. Weka taka ndani ya shimo bila kumwaga pembeni; na
4. Funika shimo kwa udongo kwa namna ambayo wanyama kama mbwa hawataweza kufukua.

FOR ONLINE USE ONLY



Stadi za Kazi darasa la 6.indd 30 23/07/2021 15:12

FOR ONLINE USE ONLY
DO NOT DUPLICATE

Taka hizi zinaweza kubadilishwa kuwa mbolea inayoitwa mboji au mboleavunde. Mboji inaweza kutumika katika bustani za maua na mboga. Mboji hurutubisha udongo na kusaidia maua, mboga na mazao mengine kustawi na hivyo kutoa mazao mengi na bora. Iwapo kuna wahitaji na unao uwezo wa kuzalisha kiasi kikubwa cha mboji, unaweza kuiuza ili kupata kipato.

### Udhibiti wa taka zinazofaa kutumika tena

Baadhi ya taka zinaweza kutumika tena kwa shughuli mbalimbali. Taka zinazofaa kutumika zinatakiwa kutengwa na kukusanywa mahali maalumu kwa ajili ya utaratibu wa kuzitumia kwa namna mbalimbali. Ifuatayo ni mifano ya taka zinazoweza kutumika tena kwa ajili ya matumizi mbalimbali.

1. Matairi; hutumika kama vyombo vya kuoteshea mimea na kuzuia mmomonyoko wa ardhi.
2. Makopo; hutumika kama vyombo vya kuoteshea mimea pia kuhifadhia vitu.
3. Mifuko ya salfeti; hutumika kuhifadhia vitu, kuoteshea mimea na kubebea bidhaa kutoka dukani, sokoni au shambani.
4. Majani makavu ya migomba na minazi; hutumika kama vifungashio, matandazo, kutengeneza mapambo na kuezekea nyumba.
5. Karatasi zilizotumika; hutumika kuandikia au kuchapia upande wa pili, pia huwashia moto hasa majiko ya mkaa.

### Urejelezaji

Urejelezaji hutumia vitu ambavyo havifai tena na kuvigeuza kuwa malighafi kwa ajili ya kutengenezea vitu vipya ambavyo vinafaa. Urejelezaji pia huokoa nishati inayotumika viwandani katika utengenezaji wa bidhaa mpya. Kwa mfano, kutengeneza karatasi kwa njia ya urejelezaji hupunguza nishati inayohitajika kutengeneza karatasi mpya kabisa kwa takribani theluthi mbili ($\frac{2}{3}$). Urejelezaji wa baadhi ya taka kama vyuma na mipira ni lazima ufanyike viwandani. Hata hivyo, baadhi ya taka kama karatasi, glasi au vioo na bati zinaweza kushughulikiwa katika karakana ndogo au hata kwenye nyumba za watu.

FOR ONLINE USE ONLY



Stadi za Kazi darasa la 6.indd 31 23/07/2021 15:12

FOR ONLINE USE ONLY
DO NOT DUPLICATE

***Faida za urejelezaji:*** Zifuatazo ni baadhi ya faida za urejelezaji wa taka:

1. Hupunguza kiwango cha taka ngumu ambazo zinachafua mazingira yetu;
2. Huokoa fedha na nafasi au ardhi ambayo ingetumika kuhifadhia taka;
3. Hupunguza matumizi ya rasilimali kwa kutumia rasilimali zaidi ya mara moja;
4. Husaidia kukuza uchumi wa eneo husika pia uchumi wa taifa kwa kupunguza kiasi cha malighafi ambazo zinatakiwa kuagizwa kutoka nje ya nchi; na
5. Hutoa fursa za ajira.

***Baadhi ya taka zinazoweza kurejelezwa:*** Taka ambazo zinaweza kurejelezwa hutegemea viwanda vya urejelezaji vilivyopo katika eneo husika. Ifuatayo ni mifano ya taka zinazoweza kurejelezwa:

1. Mifuko ya salfeti; hutengenezea mifuko ya kuhifadhia vitu na vikapu vya kubebea bidhaa kutoka dukani au sokoni;
2. Vifuu vya nazi; hutengenezea vikombe, uma, vijiko, mifuniko, upawa, kata na mapambo kama bangili na hereni;
3. Majani makavu ya migomba; hutengenezea kamba, vifaa vya sanaa, vifungashio, mikeka na majamvi;
4. Vumbi la mbao, hususani kwenye karakana; hutengenezea mboji. Pia hutengenezea nishati ya kupikia katika majiko maalumu au hugandamizwa kama tofali na kutumika kama chanzo cha nishati ya kupikia;
5. Mabaki ya vyuma chakavu; hutengenezea majiko, taa na vitu vya sanaa;
6. Kioo au glasi; huyeyushwa na kuwa kimiminika ambacho hutengenezwa katika maumbo mbalimbali ya vyombo vipya;
7. Aluminiamu; huyeyushwa na kutengenezwa kuwa bidhaa mpya kama makopo;

FOR ONLINE USE ONLY



Stadi za Kazi darasa la 6.indd 32 23/07/2021 15:12

FOR ONLINE USE ONLY
DO NOT DUPLICATE

8. Makopo ya chuma na bati; hurejelezwa kwa kutenganisha bati na chuma. Chuma na bati baadaye husafishwa na kuuzwa kama malighafi ya kutengenezea makopo au vifaa vingine. Makopo pia hutengenezea taa za kandili, vibatari na stendi za mishumaa;

9. Mpira; hurejelezwa kwa kuyeyushwa au kukatwakatwa na kutengenezwa katika maumbo ya bidhaa nyingine. Katika viwanda vidogovidogo, mpira kama matairi hutumika kutengenezea bidhaa kama kandambili na vipuri vya mashine mbalimbali;

10. Karatasi; ni moja ya taka chache ambazo zinaweza kurejelezwa na kurudia hali yake ya awali. Karatasi kwa ajili ya matumizi ya kibiashara mara nyingi hurejelezwa viwandani. Inaweza pia kurejelezwa kwa kutumia mikono na kutoa bidhaa za karatasi kwa ajili ya matumizi ya nyumbani na biashara mfano mifuko, makasha na vifungashio; na

11. Taka zenye kemikali za sumu; Taka hizi, zikiwemo kompyuta, betri, vifaa vya elektroniki, rangi, viuatilifu na vyombo vinavyohifadhi bidhaa hizo vinahitaji uangalifu mkubwa katika kuvishughulikia ili wale wanaofanya kazi ya kuvirejeleza wasidhurike. Hata hivyo, baadhi ya bidhaa hizo haziwezi kurejelezwa kabisa.

### Changamoto za urejelezaji taka



Fikiri

Je, kuna changamoto gani katika urejelezaji taka?

Baadhi ya taka hususani za plastiki zinaporejelezwa, ubora wake hupungua. Mfano, chupa ya plastiki haitumiki kutengeneza chupa nyingine ya plastiki bali hutengenezea bidhaa nyingine yenye ubora wa chini. Kwa sababu hii, plastiki inaweza kurejelezwa mara chache tu na baada ya hapo haitafaa tena. Vilevile, urejelezaji wa baadhi ya taka za plastiki huzalisha gesi ya sumu yenye madhara kwa wafanyakazi viwandani, kwenye mazingira tunayoishi na jamii kwa ujumla. Mara nyingi taka nyingi za plastiki ambazo zinatakiwa kurejelezwa huishia kwenye mashimo ya taka. Hivyo, ni bora kupunguza matumizi ya plastiki kadiri iwezekanavyo.

FOR ONLINE USE ONLY

FOR ONLINE USE ONLY
DO NOT DUPLICATE

## Udhibiti wa taka zisizofaa kutumika



Jadiliana katika kikundi na wenzako

Ni zipi taratibu za serikali za eneo unaloishi na za nchi kuhusu udhibiti wa taka za aina mbalimbali zikiwemo zenye sumu?

---

Zipo taka zisizofaa kutumiwa tena, kurejelezwa au kutumika kutengenezea mboji. Taka hizi inabidi ziondolewe au kuhifadhiwa kwa usalama. Hupaswi kuzichoma, kuzifukia shimoni kiholela wala kuzikatakata na kuzitumia kama chanzo cha nishati wakati wa kupika. Mfano, uchomaji wa plastiki au mpira huzalisha kemikali zenye sumu ambazo husababisha madhara mengi ya kiafya. Ni vema taka hizi zipelekwe kwenye shimo maalumu la kuhifadhia taka kwa usalama iwapo lipo katika kijiji au mtaa unaoishi. Shimo maalumu ni lile lenye tabaka la kinga sakafuni na kwenye kuta zake. Tabaka la kinga linazuia kuvuja kwa sumu ambazo zinaweza kuingia kwenye vyanzo vya maji. Iwapo shimo maalumu halipo, taka hizi zinaweza kuhifadhiwa kwa kuchimba shimo dogo mbali na vyanzo vya maji, kuweka taka kwenye shimo hilo kisha kulifukia vizuri kwa udongo.

***Angalizo:*** *Taka zenye kemikali za sumu zinapofukiwa ardhini, kemikali hizo zinaweza kuvuja ardhini na kuchafua maji hivyo kuhatarisha afya za watumiaji wa maji hayo.*

### Kazi za kufanya namba 4

1. Katika kikundi fanya kazi zifuatazo:
   (a) Bainisha njia zote zinazotumika kudhibiti taka shuleni na nyumbani kwenu
   (b) Eleza faida za kila njia
   (c) Eleza hasara za kila njia. Je, utachukua hatua gani kuepuka hasara hizo?
2. Chambua taka mbalimbali pamoja na kuzidhibiti katika mazingira ya shuleni na nyumbani.
3. Andaa taarifa ya shughuli ulizofanya kwa kubainisha changamoto zilizojitokeza na namna ulivyokabiliana nazo. Wasilisha taarifa hiyo darasani.



Stadi za Kazi darasa la 6.indd 34 23/07/2021 15:12

FOR ONLINE USE ONLY
DO NOT DUPLICATE

## Zoezi la pili

**A. Chagua jibu sahihi kwa kila swali na uliandike katika daftari lako la mazoezi**

1. Taka zifuatazo zinafaa kwa mbolea isipokuwa:
   (a) vinyesi vya wanyama
   (b) maganda ya matunda
   (c) majani ya miti
   (d) vifuu vya nazi

2. Tunadhibiti taka kwa sababu gani?
   (a) Kuongeza eneo la kijiji na kuboresha mazingira.
   (b) Kuwa na mazingira safi na kuepuka magonjwa.
   (c) Kurejeleza taka na kupata bidhaa bora.
   (d) Kupata mbolea za kisasa kwa matumizi ya nyumbani.

3. Zifuatazo ni taka zinazofaa kutumika tena isipokuwa:
   (a) Matairi na vifuu vya nazi
   (b) Mifuko ya salfeti na vyuma chakavu
   (c) Chupa za vipodozi na makopo ya viuatilifu
   (d) Majani makavu na karatasi zilizotumika.

4. Kuweka matandazo katika bustani kunaleta faida ya:
   (a) Kuzuia upepo mkali usivunje miche.
   (b) Kuhifadhi unyevu wakati wa kiangazi.
   (c) Kuzuia jua kali lisikaushe majani.
   (d) Kuzuia mwanga ili miche isirefuke sana.

FOR ONLINE USE ONLY



Stadi za Kazi darasa la 6.indd 35 23/07/2021 15:12

FOR ONLINE USE ONLY
DO NOT DUPLICATE

5. Hizi zote ni faida za kutunza mboga isipokuwa:
   (a) Kupata mboga kwa urahisi.
   (b) Kuimarisha afya ya mlaji.
   (c) Kuongeza kipato cha mkulima.
   (d) Kumpatia mlaji protini mwilini.

**B. Oanisha sentensi kutoka fungu "A" na maneno yaliyoko fungu "B" ili upate majibu sahihi**

| Na. | Fungu "A" | | Fungu "B" |
|---|---|---|---|
| 1. | Jumla ya mambo yote yanayomzunguka binadamu | A | Mategemezo |
| 2. | Husaidia mboga zinazokwea zisianguke kwenye udongo | B | Mboji |
| 3. | Kuondoa matawi na majani yasiyohitajika | C | Mazingira |
| 4. | Sehemu ya kusia mbegu kabla ya kuzipanda | D | Pogolea |
| 5. | Mchanganyiko wa vitu hai vilivyooza ambao hutumika kama mbolea | E | Kitalu |
| | | F | Samadi |
| | | G | Nishati |

**C. Jibu maswali yafuatayo kwa kuandika majibu yake kwenye daftari lako la mazoezi**

1. Taja vipaumbele vitatu vya kuzingatia katika udhibiti wa taka.
2. Bainisha mambo manne ya kuzingatia wakati wa kufukia taka zenye asili ya kuoza mapema.



Stadi za Kazi darasa la 6.indd 36 23/07/2021 15:12

FOR ONLINE USE ONLY

FOR ONLINE USE ONLY
DO NOT DUPLICATE

# Sura ya Tatu

## Upishi

### Utangulizi

*Ulipokuwa Darasa la Tano, ulijifunza kuhusu umuhimu wa kupika chakula, usalama wakati wa kupika chakula, kanuni za upishi na za usafi binafsi unapoandaa chakula. Vilevile, ulijifunza kuhusu makundi ya vyakula, usafi wa mazingira katika eneo la kuandaa chakula, njia mbalimbali za mapishi na namna ya kuandaa juisi kwa njia ya kukamua matunda. Katika sura hii, utajifunza kuhusu taratibu za uandaaji wa vyakula vinavyopikwa kwa kutumia mafuta mengi. Utajifunza pia utayarishaji wa vyakula vya safari pamoja na uandaaji wa vinywaji kwa njia ya kupondaponda na kuloweka viambaupishi. Hali kadhalika, utajifunza namna ya kuandaa vyakula kwenye mkeka na mezani. Aidha utajifunza upambaji wa chakula na tabia njema wakati wa kula. Hivyo, maudhui ya sura hii yatakuwezesha kuandaa vyakula na vinywaji vya aina mbalimbali kwa usahihi.*

### Ukaangaji wa vyakula kwa mafuta mengi



Fikiri
Je, unafahamu vyakula vinavyofaa kukaangwa kwa kutumia mafuta mengi?

Chakula ni mojawapo ya mahitaji muhimu kwa maisha ya binadamu. Chakula huupatia mwili virutubishi muhimu kwa afya bora. Baadhi ya vyakula huweza kuliwa vikiwa vibichi kama matunda na vingine huhitaji kupikwa kwa njia mbalimbali. Kukaanga vyakula katika mafuta mengi ni njia ya haraka ya kutayarisha chakula. Njia hii hutumia mafuta mengi kiasi cha kufunika chakula. Vyakula vilivyokaangwa kwa njia hii, vinaweza kutumika kwa muda mrefu bila kuharibika kwa kuwa vimepunguzwa kiasi



Stadi za Kazi darasa la 6.indd 37 23/07/2021 15:12

FOR ONLINE USE ONLY
DO NOT DUPLICATE

kikubwa cha maji. Vipo vyakula mbalimbali vinavyoweza kupikwa kwa kutumia mafuta mengi. Vyakula hivyo ni pamoja na maandazi, ndizi za kukaanga, kaukau na kababu. Ufuatao ni utaratibu wa kuandaa baadhi ya vyakula:

### 1. Maandazi

**Viambaupishi**

Unga wa ngano $^{1}/_{2}$ kilo

Sukari vijiko 4 vya chakula

Siagi gramu 125

Tui la nazi au maziwa mililita 300 kama yanapatikana

Hamira chenga kijiko 1 cha chai.

Hiliki gramu 100 au $^{1}/_{4}$ kijiko cha chai

Mayai 2 au 3 kama yapo

Mafuta ya kupikia.

**Tanbihi:** Ujazo wa mafuta uwe theluthi mbili ya chombo kinachotumika kukaanga maandazi.

Hatua

(i) Tayarisha viambaupishi na vyombo.

(ii) Kuna nazi kisha chuja tui zito.

(iii) Menya iliki kisha isage kupata unga au chenga.

(iv) Chekecha unga kwenye bakuli kuondoa takataka.

(v) Weka sukari, hiliki, hamira ya chenga, siagi katika unga uliochekecha.

(vi) Changanya vizuri viambaupishi vyako kwa kutumia ncha za vidole huku ukinyanyua mikono kuruhusu hewa iingie vizuri kwenye mchanganyiko.

(vii) Ongeza yai kwenye mchanganyiko kisha changanya vizuri.

FOR ONLINE USE ONLY

FOR ONLINE USE ONLY
DO NOT DUPLICATE

(viii) Ongeza tui la nazi au maziwa kidogokidogo. Iwapo hakuna tui la nazi au maziwa tumia maji.

(ix) Kanda mchanganyiko huo mpaka ulainike. Funika na kitambaa au chombo safi kisha weka kwenye sehemu yenye joto ili uumuke.

(x) Kata madonge ya kinyunga yenye ukubwa wa wastani kisha sukuma kupata umbo bapa lenye unene kiasi.

(xi) Kata maumbo kwa namna unayopenda mfano umbo la mstatili au duara ukitumia vifaa kama kisu, bilauri, gilasi au kikombe. Weka kwenye sehemu ya joto yaumuke.

(xii) Chemsha mafuta katika karai au sufuria safi na iliyokavu. Hakikisha mafuta yanapata joto la kutosha.

(xiii) Tumbukiza kipande cha andazi kujaribisha kama mafuta yamepata joto la kutosha. Iwapo andazi litapanda juu baada ya muda mfupi, basi joto la mafuta litakuwa limetosha. Endapo kipande cha andazi kitabaki chini kwa muda mrefu, joto la mafuta litakuwa halitoshi kukaanga chakula hicho.

(xiv) Tumbukiza maandazi kulingana na ukubwa wa chombo unachotumia.

(xv) Maandazi yakiiva upande mmoja geuza upande wa pili. Kaanga maandazi yawe na rangi ya kahawia.

(xvi) Epua maandazi kisha yaweke katika chombo kinachoruhusu mafuta kuchuruzika au kwenye karatasi maalumu ya kufyonza mafuta.

(xvii) Hifadhi maandazi kwenye chombo safi yakishapoa.

Maandazi yanaweza kuliwa na chai au kinywaji chochote baridi kama vile juisi. Vilevile, yanaweza kuuzwa ili kuongeza kipato.

FOR ONLINE USE ONLY

## 2. Ndizi za kukaanga

### Viambaupishi

Ndizi kadri ya mahitaji

Mafuta ya kupikia chakula kulingana na idadi ya ndizi

FOR ONLINE USE ONLY
DO NOT DUPLICATE

Mayai kulingana na idadi ya ndizi iwapo yatahitajika

Chumvi kiasi

**Tanbihi:** Ndizi zinaweza kuwa mbichi au zilizoanza kuiva. Kuweka yai au rojo ya ngano ni matakwa ya mtu. Ndizi zinaweza kukaangwa bila kuchovya kwenye yai au rojo ya ngano.

Hatua

(i) Tayarisha viambaupishi na vyombo utakavyotumia kama kisu, bakuli, na kijiko cha kuipulia.

(ii) Menya ndizi kisha kata vipande virefuvirefu .

(iii) Piga yai, weka chumvi kidogo.

(iv) Chovya vipande vya ndizi kwenye yai.

(v) Pasha mafuta yapate joto la kutosha.

(vi) Weka vipande vya ndizi katika mafuta yaliyopata joto la kutosha

(vii) Kaanga ndizi hadi ziwe na rangi ya kahawia.

(viii) Toa ndizi katika mafuta na weka katika chombo chenye matundu ili mafuta yachuruzike.

(ix) Weka ndizi kwenye chombo safi tayari kuliwa.

Unaweza kula ndizi zilizokaangwa pamoja na chai au kinywaji chochote baridi.

### 3. Kaukau

#### Viambaupishi

Ndizi, viazi mviringo au mbatata, viazi vitamu au mihogo kadri ya mahitaji

Mafuta ya kupikia chakula kulingana na kiasi cha ndizi au viazi vinavyohitaji kukaangwa

Chumvi kiasi kulingana na kiasi cha kaukau zitakazokaangwa.

FOR ONLINE USE ONLY



Stadi za Kazi darasa la 6.indd 40 23/07/2021 15:12

FOR ONLINE USE ONLY
DO NOT DUPLICATE

Hatua

(i) Menya ndizi au viazi,osha na kisha kata katika vipande vyembamba.

(ii) Pasha mafuta yapate joto la kutosha.

(iii) Tumbukiza vipande ulivyokata katika mafuta yaliyopata joto la kutosha kisha kaanga hadi ziwe na rangi ya kahawia.

(iv) Toa kaukau katika mafuta na weka katika chombo chenye matundu ili mafuta yachuruzike.

(v) Hifadhi kaukau katika chombo safi au fungasha kwenye vifungashio sahihi.

Unaweza kula kaukau pamoja na kinywaji chochote. Vilevile, unaweza kufungasha kwa ajili ya biashara au safari.

**4. Kababu**

**Viambaupishi**

Nyama $^1/_4$ kilo. Unaweza kutumia nyama ya ng'ombe, mbuzi, kondoo, kuku au minofu ya samaki.

Mafuta ya kupikia chakula

Pilipili 2 kama unahitaji

Kitunguu 1

Mayai 2

Chenga kavu za mkate

Chumvi $^1/_4$ kijiko cha chai

Hatua

(i) Saga nyama kwa kutumia mashine. Iwapo huna mashine twanga nyama ndani ya kinu au icharange kwa kutumia ubao na kisu kupata vipande vidogovidogo.

FOR ONLINE USE ONLY

FOR ONLINE USE ONLY
DO NOT DUPLICATE

(ii) Saga au katakata vitunguu vipande vidogovidogo. Weka vipande vya pilipili kama unahitaji.

(iii) Weka chumvi kisha changanya pamoja vyote.

(iv) Tumia mchanganyiko huo kutengeneza vibonge vidogovidogo vya duara.

(v) Viringisha vibonge kwenye chenga za mkate kisha chovya kwenye yai lililokorogwa. Hii husaidia kushikanisha nyama vizuri.

(vi) Kaanga kwenye mafuta mengi yaliyopata joto la kutosha.

Unaweza kula kababu pamoja na kinywaji chochote kama chai au juisi. Vilevile, unaweza kutayarisha kwa ajili ya kuuza ili kujipatia kipato.

***Angalizo:*** *Katika uandaaji wa vyakula, zingatia usafi binafsi, vyombo, vifaa na eneo la kuandalia chakula.*

## Kazi za kufanya namba 1

1. Katika vikundi, chagueni aina mbili za vyakula vya kukaanga kwa mafuta mengi katika orodha ya vyakula mlivyojifunza au vinavyopatikana katika mazingira yenu.
2. Fanyeni maandalizi ya viambaupishi pamoja na vyombo kisha mpike vyakula hivyo kwa njia ya kukaanga kwa mafuta mengi mkizingatia taratibu za upishi mlizojifunza.

## Zoezi la kwanza

1. Eleza jinsi ya kujaribisha joto la mafuta kwa ajili ya kukaanga chakula.
2. Andika sababu za kutumia mafuta yaliyopata joto la kutosha wakati wa kukaanga vyakula.
3. Bainisha njia utakazotumia kusaga nyama iwapo huna mashine ya kusagia.
4. Taja aina nyingine za vyakula vinavyokaangwa kwa mafuta mengi tofauti na vyakula ulivyojifunza.

FOR ONLINE USE ONLY



Stadi za Kazi darasa la 6.indd 42 23/07/2021 15:12

FOR ONLINE USE ONLY
DO NOT DUPLICATE

## Utengenezaji wa juisi

Matunda hutupatia madini na vitamini muhimu mwilini ikiwemo vitamini C ambayo husaidia mwili usipatwe na magonjwa. Matunda kama vile machungwa, malimau, machenza, ndimu, mabalungi, madalanzi pamoja na ubuyu au ukwaju yana kiasi kikubwa cha vitamini C. Unaweza kutumia aina mojawapo ya matunda haya au mchanganyiko wa matunda kutengeneza kinywaji. Vinywaji hivyo vya matunda huweza kutengenezwa kwa njia ya kukamua, kupondaponda au kuloweka viambaupishi. Ulipokuwa Darasa la Tano ulijifunza kutengeneza juisi kwa njia ya kukamua matunda. Sasa utajifunza kutengeneza juisi kwa njia ya kupondaponda na kuloweka viambaupishi.

### *Taratibu za kutengeneza juisi*

Zifuatazo ni taratibu unazopaswa kuzingatia unapotengeneza juisi:

1. Tumia viambaupishi bora, safi na salama. Iwapo unahitaji kutengeneza juisi ya mchanganyiko wa matunda ni vema tunda la aina moja liwe na ladha ya uchachu.
2. Ladha ya juisi hupatikana kwa kuongeza sukari kiasi kidogo. Kiasi cha sukari hutegemea mahitaji ya mtu binafsi. Andaa shira kwa kukoroga sukari kwenye maji yaliyochemshwa kisha acha yapoe.
3. Kamua au pondaponda matunda pale unapohitaji kutengeneza juisi kuepuka kupoteza vitamini.
4. Ongeza shira iliyopoa kwenye matunda yaliyopondwa. Unaweza pia kutumia asali.
5. Iwapo kinywaji au juisi inahitajika kunywewa ikiwa baridi, weka sehemu yenye ubaridi au ongeza vipande vya barafu.
6. Epuka kutumia vyombo vya metali kwani huweza kuharibu ladha ya juisi hususani iliyotengenezwa kwa kutumia matunda yenye uchachu kama machungwa. Vilevile, juisi za aina hii huweza kuharibu mwonekano wa vyombo hivyo.
7. Tumia gilasi ndefu kuweka juisi kisha pamba kwa kutumia kipande cha tunda lililotumika kutengeneza juisi husika kumvutia mtumiaji.

FOR ONLINE USE ONLY



Stadi za Kazi darasa la 6.indd 43 23/07/2021 15:12

FOR ONLINE USE ONLY
DO NOT DUPLICATE

8. Zingatia usafi binafsi, wa vyombo na mazingira ya kutengenezea juisi ili kuepuka madhara yanayoweza kusababishwa na mazingira machafu.

***Utengenezaji wa juisi kwa njia ya kupondaponda:*** Hii ni njia rahisi na ya haraka ya kutengeneza kinywaji ambacho huweza kutumiwa na mtu yeyote. Matunda yanayofaa kutengeneza juisi kwa kutumia njia hii ni kama vile nanasi, parachichi, papai, embe, karakara na tikitimaji.

**a) Juisi ya nanasi**

**Viambaupishi**

Nanasi 1

Sukari kidogo kulingana na mahitaji

Maji safi na salama

Hatua

(i) Andaa shira kwa kukoroga sukari kwenye maji yaliyochemshwa kisha acha ipoe.


(ii) Menya nanasi, katakata vipande vidogovidogo kisha pondaponda kwa kutumia mwiko au mashine maalumu kupata mchanganyiko mzito.

(iii) Chuja nanasi lililopondwa kwa kutumia chujio safi la juisi.

(iv) Ongeza shira kwenye juisi ya nanasi iliyochujwa. Koroga vizuri mchanganyiko wako kuhakikisha viambaupishi vimechanganyika vizuri.

(v) Hifadhi juisi sehemu yenye ubaridi tayari kwa kunywa.

(vi) Tumia gilasi au bilauri safi kuandaa juisi tayari kwa kunywa kama inavyoonekana katika Kielelezo namba 1.



**Kielelezo namba 1:** *Juisi ya nanasi*

FOR ONLINE USE ONLY

FOR ONLINE USE ONLY
DO NOT DUPLICATE

**b) Juisi ya papai**

**Viambaupishi**

Papai lililoiva vizuri

Sukari kidogo

Maji safi na salama

Hatua


(i) Andaa shira kwa kukoroga sukari kwenye maji yaliyochemshwa kisha acha ipoe.

(ii) Menya papai, kata vipande vidogovidogo na kuvipondaponda kwa kutumia mwiko au mashine maalumu.

(iii) Chuja kisha weka kwenye chombo safi na ongeza shira kwenye papai ulilochuja.

(iv) Koroga vizuri mchanganyiko wako kuhakikisha viambaupishi vimechanganyika vizuri.

(v) Tumia gilasi au bilauri safi kuandaa juisi tayari kwa kunywa kama inavyoonekana katika Kielelezo namba 2. Unaweza kuweka juisi sehemu yenye ubaridi ili ipoe.



**Kielelezo namba 2:** *Juisi ya papai*

**Tanbihi**: Unaweza kutumia viambaupishi vya aina mbalimbali kutengeneza juisi kwa kufuata hatua hizi za kupondaponda matunda.

FOR ONLINE USE ONLY

FOR ONLINE USE ONLY
DO NOT DUPLICATE

***Utengenezaji wa juisi kwa njia ya kuloweka viambaupishi:*** Hii ni njia rahisi ya kutengeneza juisi. Matunda mengine kama vile ubuyu, ukwaju na rozela huhitaji kulowekwa kwa muda wa saa kadhaa ili kupata juisi. Unapaswa kuloweka matunda uliyochagua katika maji safi na salama. Utengenezaji wa juisi kwa njia ya kuloweka ni kama ifuatavyo:

**Juisi ya ukwaju**

Viambaupishi

Ukwaju ½ kilo

Sukari vijiko vitatu au asali vijiko viwili

Maji safi na salama lita moja

Hatua

(i) Safisha ukwaju kisha menya vizuri.

(ii) Loweka ukwaju uliosafishwa kwenye maji safi na salama. Hakikisha unafunika chombo kuzuia upotevu wa virutubishi.

(iii) Acha kwa muda wa saa moja.

(iv) Koroga kupata mchanganyiko mzuri.

(v) Chuja kisha ongeza asali au sukari uliyoiandaa.

(vi) Hifadhi juisi sehemu yenye ubaridi ili ipoe vizuri.

(vii) Andaa juisi tayari kwa kunywa kama inavyoonekana katika Kielelezo namba 3.


**Tanbihi:** Unaweza kutumia ubuyu au rozela kutengeneza juisi kwa njia hii. Baadhi ya viungo huweza kuongezwa katika juisi kwa ajili ya kuongeza ladha na harufu. Unaweza kuongeza kiasi kidogo cha hiliki au tangawizi.

FOR ONLINE USE ONLY



Stadi za Kazi darasa la 6.indd 46 23/07/2021 15:12

FOR ONLINE USE ONLY
DO NOT DUPLICATE



**Kielelezo namba 3:** *Juisi ya ukwaju*

**Kazi ya kufanya namba 2**

Chagua matunda au viambaupishi vinavyopatikana katika mazingira yanayokuzunguka kisha tengeneza juisi kwa njia ya kupondaponda au kuloweka. Zingatia kanuni za usafi na usalama wakati wa kutengeneza juisi uliyoichagua.

**Zoezi la pili**

1. Eleza sababu za kufuata kanuni za usafi binafsi, usafi wa vyombo na mazingira wakati unapotengeneza juisi?
2. Orodhesha aina nyingine za juisi zinazoweza kutengenezwa katika mazingira yenu tofauti na ulizojifunza darasani.
3. Ainisha njia tatu zinazoweza kutumika kutengeneza juisi.

## Uandaaji wa vyakula baada ya kupika

Bila shaka umeshajenga umahiri wa kutayarisha vyakula kwa kutumia njia mbalimbali. Umejifunza pia utengenezaji wa juisi za aina mbalimbali kwa njia ya kukamua, kupondaponda au kuloweka viambaupishi. Sasa utajifunza uandaaji wa chakula baada ya kupika. Uandaaji wa vyakula ni maandalizi ambayo hufanywa baada ya upishi kukamilika. Hatua hii ni ya kukiweka

FOR ONLINE USE ONLY



Stadi za Kazi darasa la 6.indd 47 23/07/2021 15:12

FOR ONLINE USE ONLY
DO NOT DUPLICATE

chakula katika mpangilio mzuri tayari kwa kuliwa. Zipo njia mbalimbali unazoweza kutumia kuandaa chakula. Unaweza kuandaa chakula mezani au kwenye mkeka kulingana na mazingira au desturi za jamii husika. Wakati wa kuandaa chakula hakikisha unazingatia mambo yafuatayo:

(a) Usafi na usalama wa chakula.

(b) Usafi na usalama wa eneo linalotumika kuandaa chakula baada ya kupikwa.

(c) Tumia vyombo safi na sahihi kulingana na aina ya chakula kilichotayarishwa.

(d) Weka vyombo katika mpangilio mzuri ili kuruhusu watumiaji kupakua chakula bila usumbufu.

(e) Tumia ungo au sinia kubeba vyombo na vyakula unapoandaa chakula.

(f) Pamba chakula ili kuwavutia walaji.

(g) Hakikisha unatenga maji na sabuni kwa ajili ya kunawa mikono kabla na baada ya kula chakula.

## Kuandaa chakula kwenye mkeka

Utaratibu huu wa kuandaa chakula bila ya kutumia meza umekuwa ukitumiwa na makabila mengi ya kitanzania. Utamaduni huu wa uandaaji chakula unahusisha kutumia mkeka, ngozi au juu ya kitu chochote kulingana na mazingira yanayohusika. Ni vema kila mtu akatumia chombo chake peke yake wakati wa kula chakula kama inavyoonekana katika Kielelezo namba 4 kuepuka kuambukizana magonjwa kama kifua kikuuu.

Mambo ya kuzingatia katika uandaaji wa chakula katika mkeka:

(i) Andaa jamvi, ngozi au mkeka katika mazingira safi.

(ii) Andaa chakula, maji safi na salama ya kunawa mikono pamoja na ya kunywa juu ya mkeka. Tumia vyombo safi na salama kuwekea maji.

FOR ONLINE USE ONLY



Stadi za Kazi darasa la 6.indd 48 23/07/2021 15:12

FOR ONLINE USE ONLY
DO NOT DUPLICATE

(iii) Kumbuka kufunika chakula kilichoandaliwa ili kuzuia nzi, vumbi na uchafu mwingine kuingia katika chakula. Unaweza kutumia kitambaa safi cheupe cha pamba au aina ya neti kufunika chakula kilichoandaliwa.



**Kielelezo namba 4:** *Uandaaji chakula katika mkeka*

### Kuandaa chakula mezani

Huu ni utaratibu mzuri kiafya kwa kuwa unaepusha chakula kuchafuliwa na vumbi au mchanga. Zingatia mambo yafuatayo wakati wa kuandaa chakula mezani:

(a) Andaa chakula katika mazingira safi ya meza. Ni vyema kutandika kitambaa safi cha kuvutia katika meza ya kuandalia chakula.

(b) Hakikisha unatenga vyombo safi vya chakula vinavyohitajika kwa kila mtu kama vile sahani, bakuli, kijiko, uma, kisu na gilasi au bilauri katika eneo au sehemu atakayokaa mlaji kama inavyoonekana katika Kielelezo namba 5.

(c) Weka vyombo vya chakula katika mpangilio mzuri kama inavyoonekana katika kielelezo namba 5.

FOR ONLINE USE ONLY

FOR ONLINE USE ONLY
DO NOT DUPLICATE


(d) Weka uma upande wa kushoto mwa sahani ya mlaji. Kisu na kijiko upande wa kulia mwa sahani ya mlaji.

(e) Hakikisha unaweka vyombo vya kutosha vya kupakulia chakula kulingana na aina ya chakula kilichoandaliwa.

(f) Hakikisha unatenga chakula cha kutosha kulingana na idadi ya walaji.

(g) Ni vema kila mlaji kujipakulia chakula mwenyewe ili achukue chakula anachopenda na cha kumtosha. Inashauriwa mlaji achote chakula ambacho atakimaliza kuliko kubakiza chakula na kukimwaga. Hii sio tabia njema bali ni uharibifu wa chakula.

***Angalizo:*** *Mlaji anakumbushwa kunawa mikono kwa maji safi na salama pamoja na sabuni kabla na baada ya kula chakula, ili kuepuka kula uchafu na pia kuwa msafi.*



**Kielelezo namba 5:** *Uandaaji wa chakula mezani*

FOR ONLINE USE ONLY



Stadi za Kazi darasa la 6.indd 50 23/07/2021 15:12

FOR ONLINE USE ONLY
DO NOT DUPLICATE

## Upambaji wa Chakula



Fikiri:
Je, ulishawahi kuona chakula kilichopambwa?
Ni kwa nini chakula kinapambwa?

Zipo sababu kadhaa za kupamba chakula. Sababu kuu ni kukiwezesha chakula kimvutie mlaji kwa rangi na mpangilio katika sahani. Hata hivyo, upambaji wa chakula huongeza thamani ya ubora wa chakula na ladha. Hivyo, mazingira yanayowekwa chakula yapambwe pia kwa lengo la kumvutia mlaji. Unahitaji kuwa mbunifu katika upambaji wa chakula ili kumvutia mlaji. Zingatia umaridadi, mahitaji ya virutubishi na ladha ya chakula. Epuka kuchanganya vyakula vyenye ladha ya chumvi na vile vyenye ladha ya sukari kwa kuwa mchanganyiko huo unakuwa na ladha ambayo haiwavutii walaji. Zingatia rangi ya chakula kinachopambwa pamoja na rangi za viambaupishi unavyotaka kutumia kupamba chakula. Mathalani, unaweza kutumia njegere au karoti kupamba wali uliowekwa kwenye sahani. Itakuwa haivutii iwapo utapamba wali kwa kutumia vipande vya tango lililomenywa. Wakati wa kupamba chakula, hakikisha kuwa unaweka mapambo kwenye chakula na sio kwenye sahani kama inavyoonekana katika Kielelezo namba 6.



**Kielelezo namba 6:** *Chakula kilichopambwa*
***Chanzo:*** *https://www.kenyanvibe.com/5-inexpensive*

FOR ONLINE USE ONLY

FOR ONLINE USE ONLY
DO NOT DUPLICATE

**Zoezi la 3**

1. Eleza sababu tatu za kupamba chakula.
2. Eleza mambo matano muhimu ya kuzingatia wakati wa kuandaa chakula baada ya kupika.
3. Eleza madhara unayoweza kupata iwapo utakula chakula ambacho kimeandaliwa mezani na kuachwa kwa muda mrefu bila kufunikwa.
4. Ainisha wadudu wa aina tatu waharibifu wanaoweza kuchafua chakula kilichoachwa wazi.

## Tabia njema wakati wa kula



Fikiri
Je, unatakiwa kufanya nini kabla ya kuanza kula chakula?

Kabla ya kula chakula unapaswa kunawa mikono kwa maji safi na sabuni. Nawa mikono vizuri ukizingatia kusafisha maeneo ya kucha pamoja na katikati ya vidole kuhakikisha umeondoa uchafu wote. Usiponawa mikono vizuri kabla ya kula chakula unaweza kula uchafu au vijidudu vinavyoweza kusababisha magonjwa mbalimbali kama magonjwa ya tumbo, kuhara, minyoo na kipindupindu.

Wakati wa kula chakula unapaswa kuzingatia mambo yafuatayo:

(a) Kukaa kwa unyoofu karibu na sehemu iliyoandaliwa chakula kuepuka kudondosha chakula wakati wa kula.

(b) Pakua chakula unachoweza kukimaliza. Vilevile angalia idadi ya watu wanaotakiwa kula chakula hicho.

(c) Weka kinywani chakula cha kutosha, epuka kujaza kinywa kwani unaweza kupaliwa, kukabwa, kutokwa na chakula mdomoni wakati wa kutafuna, pia sio ustaarabu.

(d) Tafuna chakula polepole bila kupanua kinywa. Hakikisha unapokula chakula unatulia na huzungumzi bila sababu.

FOR ONLINE USE ONLY



Stadi za Kazi darasa la 6.indd 52 23/07/2021 15:12

FOR ONLINE USE ONLY
DO NOT DUPLICATE

(e) Ni vyema kula chakula cha kukutosha, usishibe kupita kiasi.

(f) Epuka kujikuna wakati unakula hususani kukuna kichwa kwa kuwa nywele zinaweza kudondokea katika chakula.

(g) Endapo itakulazimu kukohoa au kupiga chafya wakati unatafuna chakula, funika mdomo kwa mkono au kitambaa.

(h) Epuka kunywa maji wakati una chakula mdomoni kwani unaweza kupaliwa.

(i) Epuka tabia ya uchoyo au ulafi unapokula chakula.

Aidha, ni vema kushukuru baada ya kula chakula kisha nawa mikono vizuri kwa maji safi na sabuni. Baada ya kula chakula, epuka kutoa masalio ya chakula kwenye meno mbele za watu kwani sio ustaarabu. Aidha, epuka kukaa na kijiti cha kutolea masalio ya chakula mdomoni kwa muda mrefu kwani ni uchafu kiafya na hatari kwani unaweza kujiumiza au kukimeza.

**Zoezi la 4**

1. Eleza madhara ya kuweka chakula kingi mdomoni unapokula.
2. Taja athari unazoweza kupata kwa kuacha kijiti cha kutolea masalio ya chakula mdomoni kwa muda mrefu?
3. Bainisha madhara unayoweza kupata iwapo hutanawa mikono kabla na baada ya kula chakula.
4. Kutokana na umahiri ulioujenga, eleza jinsi utakavyomuelimisha mwenzako juu ya tabia njema wakati wa kula chakula.

## Usafi wa vyombo baada ya kula

Ni vema kuondoa vyombo mezani mara tu baada ya kula chakula. Kuacha vyombo vilivyotumika wakati wa kula chakula kutawavutia wadudu kama nzi, mende na sisimizi ambao wanaweza kubeba vijidudu na kusambaza magonjwa. Vilevile, mabaki ya vyakula katika vyombo husababisha harufu mbaya. Japokuwa kusafisha vyombo mara baada ya kula ni jambo muhimu, watu wengi hulipuuzia kwa kuwa wanakuwa wameshiba na huhitaji kupumzika. Hivyo, ni vema vyombo vikasafishwa mara tu baada ya



Stadi za Kazi darasa la 6.indd 53 23/07/2021 15:12

FOR ONLINE USE ONLY

FOR ONLINE USE ONLY
DO NOT DUPLICATE

kuondolewa mezani kuepuka harufu mbaya na wadudu. Fanya maandalizi yafuatayo kwa ajili ya kusafisha vyombo:

(a) Ondoa mabaki ya vyakula katika vyombo na kuweka katika chombo maalumu cha kuhifadhi taka chenye mfuniko;

(b) Weka vyombo kwenye maji safi. Hii itasaidia kulainisha uchafu uliopo kwenye vyombo vilivyotumika;

(c) Tenganisha vyombo kulingana na aina ya vyombo pamoja na kiasi cha uchafu uliopo katika vyombo;

(d) Unaweza kusafisha vyombo katika sinki au beseni la kuoshea vyombo;

(e) Epuka kupachika vikombe au gilasi ndani ya nyingine kwani zinaweza kuvunjika wakati wa kuzitoa; na

(f) Hakikisha unaandaa vifaa sahihi vya kusafishia vyombo kama osheo, mchanga au majivu, sabuni na waya maalumu kwa ajili ya kusugulia vyombo vyenye asili ya chuma na bati.

### Hatua za usafishaji vyombo

Hatua zifuatazo zinaweza kufuatwa wakati wa kusafisha vyombo:

(a) Andaa maji ya uvuguvugu na sabuni. Anza kusafisha vyombo ambavyo havijachafuka sana kama gilasi za maji au juisi. Suuza kwa maji safi kisha hifadhi sehemu safi vikauke au kuchuruzisha maji. Unaweza kukausha vyombo kwa kutumia kitambaa safi chenye uwezo wa kufyonza maji kama kitambaa cha pamba au kwa kuanika kwenye kichanja;

(b) Osha vijiko katika maji ya uvuguvugu na sabuni kisha suuza kwa maji ya moto kisha kausha vizuri;

(c) Osha na suuza sahani kisha vyombo vilivyokuwa vimehifadhi vyakula kama sinia au mabakuli na kausha vizuri;

(d) Osha sufuria au vyungu vilivyopikia chakula kwa kutumia maji ya uvuguvugu na sabuni. Sugua sufuria kwa kutumia mchanga, jivu au brashi maalumu ngumu ya kusugulia sufuria. Suuza kwa maji safi na kisha zikaushe;

FOR ONLINE USE ONLY

FOR ONLINE USE ONLY
DO NOT DUPLICATE

(e) Vyombo vyote vilivyokauka vitunzwe kabatini au kwenye beseni kwa matumizi ya baadaye; na

(f) Safisha sehemu uliyotumia kusafishia vyombo. Safisha osheo, vitambaa ulivyotumia kukaushia vyombo kisha vianike vikauke vizuri.

**Tanbihi:** Katika maeneo mengi ya vijijini vyombo huanikwa katika kichanja ili vikauke badala ya kukausha kwa kitambaa.

## Vyakula vya safari



Fikiri

1. Kuna umuhimu gani wa kubeba chakula unapokuwa safarini?
2. Je, ni njia zipi ambazo ni sahihi zaidi kuandaa vyakula vya safari?
3. Je, ni aina gani ya vyakula vinafaa kufungasha kwa safari?
4. Je, ni namna gani utafungasha vyakula vya safari ili visi haribike upesi?

Unapokuwa safarini ni muhimu kupata mahitaji ya chakula kama inavyostahili. Unaweza kufungasha chakula au kununua vyakula katika sehemu mbalimbali kama hotelini na mgahawani. Wakati mwingine njiani huwa hakuna hoteli wala mahali panapouzwa chakula au hata kama hoteli ipo, inawezekana hali yake ya usafi hairidhishi. Kwa upande mwingine, chombo mnachosafiria kinaweza kupatwa na matatizo na kulazimika kuchelewa sana kufika au kulala njiani. Hivyo, ni muhimu unaposafiri kubeba chakula cha kutosha kulingana na idadi ya watu mnaosafiri pamoja.

Bila shaka umejifunza kutayarisha vyakula na juisi kwa kutumia njia mbalimbali. Sasa utaweza kutayarisha vyakula vya safari kwa kutumia ujuzi uliojenga wa kuandaa vyakula kwa njia mbalimbali. Vyakula vya kufungasha inabidi vitayarishwe kwa namna ambayo vitaweza kudumu kwa muda wote wa safari bila kuharibika. Njia bora zaidi za kutayarisha vyakula vya safari ni kama vile kukaanga, kubanika, kuoka na kuchoma. Njia hizi ni sahihi kwa sababu vyakula vinakuwa vimepunguzwa kiasi kikubwa cha maji na hivyo vinaweza kutumika kwa muda mrefu bila kuharibika.



Stadi za Kazi darasa la 6.indd 55 23/07/2021 15:12

FOR ONLINE USE ONLY
DO NOT DUPLICATE

Chakula kinachofungashwa kwa ajili ya safari lazima kiwe mlo kamili kadri inavyowezekana. Hakikisha unafungasha chakula kilichojitosheleza kutokana na makundi mbalimbali ya vyakula.

Kumbuka ulipokuwa Darasa la Tano ulijifunza kuhusu makundi ya chakula ambayo ni vyakula vya kujenga mwili, vyakula vya kulinda mwili na vyakula vya kutia nguvu na joto mwilini. Hata hivyo, vyakula vinavyofaa kwa safari ni kama samaki wa kubanika au kukaanga, nyama ya kukaanga au ya kubanika kama mishikaki, mayai ya kuchemsha na karanga za kukaanga. Vilevile, maandazi, chapati, mkate, muhogo wa kuchoma au kukaanga, vibanzi vya viazi mbatata, vitumbua, ndizi za kukaanga au kuchoma na vitafunwa vingine vilivyo vikavu hufaa kufungashwa kwa ajili ya safari. Inafaa pia kufungasha matunda kama machungwa, mananasi au matunda mengine yasiyoharibika upesi.

Ni vizuri kuchukua maji ya moto kwa ajili ya kutengeneza chai, maziwa ya kopo au unga, sukari, majani ya chai au kahawa. Vilevile, ni muhimu kuchukua maji yaliyo salama ya kunywa. Unaweza pia kufungasha vinywaji vingine kama vile juisi. Hata hivyo, juisi inayotengenezwa nyumbani ni vema ikatumika mapema kabla haijaharibika. Unaweza kuhifadhi juisi kwenye chombo chenye uwezo wa kuhifadhi ubaridi ili isiharibike mapema.

### Ufungashaji wa vyakula vya safari

Ni vema vyakula vya safari vikaandaliwa na kufungashwa kwa namna ambayo wadudu hawataweza kuviharibu. Unapaswa kuwa makini katika upishi na ufungashaji wa vyakula hivyo ili kuzuia kuharibika. Hakikisha unafungasha vyakula kwa usafi na usalama. Tumia vyombo vikavu na safi vinavyoweza kuhifadhi vyakula kwa masaa kadhaa bila kuharibika. Vipo baadhi ya vyakula vinavyohitaji kuwekwa kila kimoja katika chombo chake kuepuka harufu na ladha kuingiliana hivyo kutompendeza mlaji. Matunda ambayo hayajakatwa hayana lazima ya kuwekwa katika vyombo maalumu.

Unaweza kufungasha vyakula kwa ajili ya safari kwa kutumia njia mbalimbali. Zipo njia za asili za kufungasha vyakula vya safari kama kufungasha kwa kutumia majani ya migomba. Njia hii hutumiwa na makabila mengi hususani kufungasha chakula wanapokwenda shamba lililoko mbali na nyumbani. Japokuwa njia hii imekuwa ikitumiwa na watu wengi, sio bora kama njia za kisasa. Maendeleo ya sayansi na teknolojia yamewezesha ubunifu wa vyombo vya kisasa ambavyo hufunga vizuri na huhifadhi joto la chakula.

FOR ONLINE USE ONLY

FOR ONLINE USE ONLY
DO NOT DUPLICATE

Vifaa hivi vya kisasa ni kama chupa ya chai, chupa za maji na vinywaji, vikasha vya plastiki, mifuko ya karatasi, karatasi zisizokuwa na michoro au maandishi, makopo pamoja na bakuli maalumu kwa safari. Baada ya kuweka vyakula katika vyombo vinavyofaa, vifungashe kwa mpango mzuri katika kikapu au mfuko wa kutosha. Weka matunda mazima humo pamoja na vyombo vingine kama vikombe, bilauri, visu, vijiko na sahani. Hakikisha unafunika vyakula kwa kitambaa au karatasi safi kuepusha visipate uchafu.








**Kielelezo namba 6:** *Ufungashaji wa vyakula kwa safari*
***Chanzo:*** *https://www.printerest.com* tarehe 27/07/2019

## Kazi za kufanya namba 3

1. Katika vikundi, jadilini juu ya mapishi mbalimbali mliyojifunza, kisha chagueni na kuandaa mlo kamili wenye vyakula vya aina tatu kwa ajili ya safari.
2. Baada ya kupika, fungasheni vyakula mlivyoandaa kwa kutumia vyombo na vifaa sahihi.

FOR ONLINE USE ONLY


Stadi za Kazi darasa la 6.indd 57 23/07/2021 15:12

FOR ONLINE USE ONLY
DO NOT DUPLICATE

## Zoezi la 5

**A. Jibu maswali yafuatayo katika daftari lako la mazoezi**

1. Eleza sifa tatu za vyakula vya safari
2. Eleza madhara manne yanayoweza kutokea iwapo vyakula vya safari havitafungashwa kwa njia sahihi.
3. Taja vyakula vya aina tano vinavyofaa kufungashwa safarini ukipendekeza vifaa na vyombo sahihi vya kufungashia vyakula hivyo.
4. Eleza sababu tatu zinazowalazimu watu kufungasha vyakula vya safari.

**B. Chagua jibu sahihi na uandike katika daftari lako la mazoezi**

1. Ni aina gani ya chakula kati ya vyakula vifuatavyo kinafaa kufungasha kwa ajili ya safari?
   (a) Ugali na mchuzi wa samaki
   (b) Wali na maharage ya nazi
   (c) Viazi na samaki wa kukaangwa
   (d) Kande zilizoungwa kwa nazi
2. Yafuatayo ni mahitaji ya kuandaa “kababu” isipokuwa
   (a) Nyama
   (b) Mafuta
   (c) Mayai
   (d) Hamira
3. Ni kiasi gani cha ujazo wa mafuta katika chombo kinashauriwa kutumia wakati wa kukaanga maandazi?
   (a) Theluthi moja
   (b) Theluthi mbili
   (c) Robo
   (d) Lita moja

FOR ONLINE USE ONLY



Stadi za Kazi darasa la 6.indd 58 23/07/2021 15:12

FOR ONLINE USE ONLY
DO NOT DUPLICATE

4. Changamoto ipi inaweza kujitokeza wakati wa kukaanga chakula kwenye mafuta mengi?
   (a) Mafuta kulipuka na kumwagika
   (b) Kuivisha vizuri chakula na kupata rangi nzuri
   (c) Chakula kinakuwa hakinyonyi mafuta
   (d) Hakikisha vyakula vinakuwa vikavu

5. Faida ya matunda mwilini ni kutupatia
   (a) Protini
   (b) Wanga
   (c) Joto
   (d) Vitamini

6. Ni wakati gani mlaji anakumbushwa kunawa mikono kwa maji safi na salama pamoja na sabuni
   (a) Kabla ya kula chakula
   (b) Baada ya kula chakula
   (c) Kabla na baada ya kula chakula
   (d) Wakati wote wa kula chakula

FOR ONLINE USE ONLY

## Msamiati

| | |
|---|---|
| **Bilauri** | Chombo mithili ya kikombe chembamba kirefu kilichotengenezwa kwa kioo au bati kisicho na mkono kinachotumiwa kunywea vimiminika. |
| **Shira** | Maji yaliyochemshwa na kuongezwa sukari kisha yakapoa kwa ajili ya kuongeza kwenye mchanganyiko wa matunda wakati wa kutengeneza juisi. |



Stadi za Kazi darasa la 6.indd 59 23/07/2021 15:12

FOR ONLINE USE ONLY
DO NOT DUPLICATE

# Sura ya Nne

## Ala za muziki

### Utangulizi

*Ulipokuwa Darasa la Tano ulijifunza kuwa, kuimba ni kutamka maneno kwa sauti ya kughani iliyo kwenye mpangilio wa muziki kulingana na makubaliano ya jamii inayohusika. Vilevile, uchezaji wa ngoma hutofautiana kati ya jamii moja na nyingine. Katika sura hii utajifunza juu ya ala za muziki, makundi yake na asili zinakopatikana ala hizo. Ala za muziki husaidia sana katika uimbaji na uchezaji wa ngoma uwapo shuleni au mahali pengine popote na katika maisha yako yote. Ala za muziki huwaongoza waimbaji na wachezaji ngoma wakati wanapoimba na kucheza ngoma.*

FOR ONLINE USE ONLY

### Ala mbalimbali za muziki


Ala za muziki ni zana mbalimbali zinazotumika katika shughuli za muziki. Ala hizi hutumika wakati wa kuimba nyimbo na kucheza ngoma mbalimbali. Pia hutumika kunogesha na kukoleza uimbaji wa kwaya, uchezaji wa ngoma na uimbaji wa nyimbo mbalimbali. Ala za muziki huwasaidia waimbaji kutohama ufunguo wa wimbo na kufuata mapigo ya wimbo kwa usahihi. Ala pia huwasaidia wachezaji kucheza ngoma kwa kufuata mkong'osio na mitindo ya ngoma inayohusika.

### Makundi ya ala za muziki

Ala za muziki zipo katika makundi mbalimbali na asili tofauti. Kuna ala za muziki zenye asili ya Tanzania na pia zipo zenye asili ya bara la Ulaya, Amerika na Asia. Ala zenye asili ya nje ya Tanzania tunaziita ala za muziki za kigeni. Kwa ujumla ala za muziki zipo katika makundi matano.

FOR ONLINE USE ONLY
DO NOT DUPLICATE

***1. Ala za kupuliza:*** Katika kundi hili la ala za muziki, kuna aina kuu mbili. Aina ya kwanza ni ala za kupuliza zenye kutoa sauti zenye kuimbika. Mfano wa ala hizo ni filimbi yenye matundu sita, tarumbeta, saksafoni na zumari. Mara nyingi ala hizi hutumika katika bendi ya shule. Zumari ni ala ambayo hupatikana mwambao wa pwani ya Tanzania. Tarumbeta na saksafoni zina asili ya Ulaya. Aina ya pili ya ala za kupuliza ni zile zenye kutoa sauti zisizo imbika kwa mfano baragumu ambazo hupatikana katika mikoa mingi ya Tanzania na lipenenga ambayo hupatikana katika mikoa ya Ruvuma na Mbeya. Kielelezo namba 1 kinaonesha ala mbalimbali za kupuliza za kitanzania na za kigeni.




| Kundi la ala | Ala za kitanzania | Ala za kigeni |
|---|---|---|
| Ala za kupuliza | <br>Baragumu<br><br>Baragumu | <br>Tarumbeta<br><br>Saksafoni |

**Kielelezo namba 1:** *Ala za muziki za kupuliza*

***2. Ala za kugonga:*** Ala za kugonga zipo nyingi na hupatikana kwa urahisi katika mazingira yetu. Kuna ala za kugonga zenye kutoa sauti za kuimbika mfano marimba ya mbao ambayo hupatikana katika mikoa ya Morogoro na Pwani. Pia zipo ala za kugonga zinazotoa mkong'osio tu. Ala hizo ni towazi, dufu, traiengo, kengele na vijiti. Kielelezo namba 2 kinaonesha ala mbalimbali za muziki za kugonga za kitanzania na za kigeni.


Stadi za Kazi darasa la 6.indd 61 23/07/2021 15:12

FOR ONLINE USE ONLY
DO NOT DUPLICATE

| Kundi la ala | Ala za kitanzania | Kundi la kigeni |
|---|---|---|
| Ala za kugonga |  Marimba ya mbao |  Traiengo |
| |  Vijiti |  Dufu |
| |  Vibao |  Towazi |

**Kielelezo namba 2:** *Ala za muziki za kugonga*

***3. Ala za nyuzi:*** Ala za nyuzi zipo za aina nyingi. Ala hizi pia zimegawanyika katika makundi mawili. Kundi la kwanza ni ala za nyuzi zenye kutoa sauti za kuimbika. Kwa mfano zeze ambayo hupatikana zaidi mikoa ya Dodoma, Singida na Morogoro. Ala nyingine ni litungu ambayo hupatikana mkoani Mara na enanga ambayo hupatikana mkoani Kagera. Kundi la pili ni la ala za nyuzi zenye kutoa sauti za mkong'osio kwa mfano ndono inayopatikana mkoani Dodoma na Singida. Kielelezo namba 3 kinaonesha ala mbalimbali za muziki za nyuzi za kitanzania na za kigeni.

FOR ONLINE USE ONLY



Stadi za Kazi darasa la 6.indd 62 23/07/2021 15:12

FOR ONLINE USE ONLY
DO NOT DUPLICATE

| Kundi la ala | Ala za kitanzania | Ala za kigeni |
|---|---|---|
| Ala za nyuzi |  Litungu  Zeze  Enanga |  Vayolini  Gitaa la umeme |

**Kielelezo namba 3:** *Ala za muziki za nyuzi*



***4. Ala za kuwambwa:*** Ala za kuwambwa ni jumla ya ngoma za aina mbalimbali zinazowambwa kwa kutumia ngozi za wanyama. Ngoma nyingine huwambwa kwa kufunikwa pande zote mbili, na nyingine huwambwa kwa kufunikwa upande mmoja tu. Kielelezo namba 4 kinaonesha ala za kuwambwa, zipo za kitanzania na za kigeni.

FOR ONLINE USE ONLY



Stadi za Kazi darasa la 6.indd 63 23/07/2021 15:12

FOR ONLINE USE ONLY
DO NOT DUPLICATE

| Kundi la ala | Ala za kitanzania | Ala za kigeni |
|---|---|---|
| Ala za kuwambwa |   Ngoma mbalimbali za kitanzania |   Ngoma mbalimbali za kigeni |

**Kielelezo namba 4:** *Ala za muziki za kuwambwa*



***5. Ala za kutikisa:*** Ala za kutikisa ni ala ambazo hutoa mdundo wa mkong'osio. Mfano wa ala hizo ni kayamba, manyanga, tatarizo, kokwa, kinjeketule na njuga. Kayamba, njuga, tatarizo na manyanga hupatikana katika mikoa mingi ya Tanzania. Kinjekutule na kokwa ni ala zinazopatikana mkoani Ruvuma, Mtwara na Iringa. Ala za kutikisa zipo za kitanzania na za kigeni kama inayoonekana katika kielelezo namba 5.

FOR ONLINE USE ONLY



Stadi za Kazi darasa la 6.indd 64 23/07/2021 15:12

FOR ONLINE USE ONLY
DO NOT DUPLICATE

| Kundi la ala | Ala za kitanzania | Ala za kigeni |
|---|---|---|
| Ala za kutikisa | <br>Njuga<br><br>Manyanga<br><br>Kayamba | <br>Sheka<br><br>Sheka |

**Kielelezo namba 5:** *Ala za muziki za kutikisa*

Ikumbukwe kuwa, baadhi ya ala za muziki hutumika katika matukio maalumu. Kwa mfano baragumu, filimbi na ngoma hutumika wakati wa kupiga mbiu kuwaita watu kujongea katika mikusanyiko maalumu.

## Kazi za kufanya namba 1

1. Andaa ala za asili za muziki zinazopatikana katika mazingira yako kisha imba nyimbo na kucheza ala hizo.
2. Chagua wimbo mmoja kati ya nyimbo za kitaifa au za kizalendo, kisha imba kwa kutumia na kufuata sauti au mkong'osio wa ala hizo.
3. Tengeneza ala yoyote kulingana na aina ya makunzi kisha eleza namna ya kuitumia wakati wa kuimba au kucheza ala hiyo.

FOR ONLINE USE ONLY

FOR ONLINE USE ONLY
DO NOT DUPLICATE

## Zoezi

**Sehemu A: Chagua jibu sahihi na uandike herufi yake katika sehemu iliyoachwa wazi mbele ya swali.**

1. Ala za muziki huwasaidia waimbaji---------------.

a) kufurahi wanapoimba

b) kuimba bila kuhama ufunguo

c) kuimba na kucheza ngoma

d) kupiga na kucheza ngoma

2. Kundi la ala za kupuliza linajumuisha ala zifuatazo ---------------.

a) filimbi, lipenenga na baragumu

b) zeze, filimbi na malimba

c) filimbi, baragumu na gitaa

d) filimbi, malimba ya mbao na lipenenga

**Sehemu B: Fanya zoezi lifuatalo kwa kujaza nafasi zilizo wazi.**

1. Taja mifano mitatu ya ala za kugonga zenye kutoa sauti za mkong'osio tu -----, -----, na --------.
2. ----------ni mfano wa ala za nyuzi zinazotoa sauti za kuimbika.
3. Toa mifano ya ala za kuwambwa kwa kutumia ngozi za wanyama mbalimbali.
4. Saksafoni ni ala ya kupuliza yenye asili ya ------------.

FOR ONLINE USE ONLY

FOR ONLINE USE ONLY
DO NOT DUPLICATE

**Sehemu C: Jibu maswali yafuatayo**

1. (a) Ala za muziki ni nini?

   (b) Bainisha makundi yanayowakilisha ala za muziki

2. Kwa nini tunatumia ala za muziki wakati wa kuimba nyimbo?

3. Baragumu hutengenezwa kwa kutumia nini?

4. Kwa nini ala za muziki ni muhimu wakati wa kucheza ngoma?

## Msamiati

| | |
|---|---|
| **Ala za muziki** | Vifaa vinavyotumika katika sanaa ya muziki |
| **Baragumu** | Pembe kubwa lililotobolewa tundu karibu na ncha yake inayopulizwa katika ngoma ili kutumbuiza au kutoa taarifa fulani ya wito katika kusanyiko |
| **Kayamba** | Kifaa kinachotengenezwa kwa matete na ndani yake hutiwa punje kavu za nafaka au changarawe ndogondogo |
| **Njuga** | Kengele ndogo zinazofungwa miguuni, mikononi au shingoni wakati watu wachezapo ngoma |
| **Saksafoni** | Chombo cha muziki cha kupuliza ambacho hubadili sauti kwa kubonyeza vifungo vyake |

FOR ONLINE USE ONLY



Stadi za Kazi darasa la 6.indd 67 23/07/2021 15:12

FOR ONLINE USE ONLY
DO NOT DUPLICATE

# Sura ya Tano

## Kumudu misingi ya uigizaji

### Utangulizi

*Ulipokuwa Darasa la Tano ulijifunza juu ya maigizo, uigizaji, aina za uigizaji na misingi ya uigizaji. Katika sura hii utajifunza kuhusu maana ya maigizo, uigizaji, mapambo, kughani ngonjera, majigambo na uigizaji wa kuganda. Kwa kujifunza sura hii, utapata ujuzi utakaokusaidia kukabiliana na changamoto mbalimbali katika maisha na kujipatia kipato mara umalizapo masomo yako.*

### Dhana ya maigizo na uigizaji

Maigizo ni sanaa katika fasihi simulizi ambayo watendaji wake ndio wahusika wakuu. Maigizo hayasimuliwi katika hali tuli ya mwili kama zilivyo aina nyingine za fasihi. Wahusika wa maigizo huzungumza na kufikisha ujumbe kwa hadhira kulingana na muktadha wa kisanaa uliopo. Maigizo hayo ni kama michezo ya watoto, malumbano ya watani, hadithi za soga, vichekesho, uigizaji kwa kucheza ngoma, majigambo, maigizo bubu na kuganda na maigizo ya kutumia maneno na vitendo. Maigizo haya hutofautiana kulingana na uhusika wa mwigizaji mwenyewe, mazingira, madhumuni na aina ya uigizaji.

Uigizaji ni uwasilishaji wa uhalisia wa maisha na shughuli za kila siku za binadamu. Uwasilishaji huu ni wa njia ya utendaji mbele ya hadhira hai. Uigizaji hubeba ujumbe mahususi na unahitaji ubunifu wa mtendaji .

### Mapambo ya kuigizia

Mapambo ni urembo unaoongeza uzuri wa kitu au mtu. Kuna mapambo ya kuvaa mikononi, masikioni, shingoni, miguuni, puani, kiunoni, kichwani,

FOR ONLINE USE ONLY



Stadi za Kazi darasa la 6.indd 68 23/07/2021 15:12

FOR ONLINE USE ONLY
DO NOT DUPLICATE

mabegani na yale ya kufunika mdomo, kichwa na macho. Mapambo yanayovaliwa ni kama vile bangili, hereni, kago, kikuku, kipini, kishaufu, mkufu, mshipi, nyerere, nywele za bandia, usinga, taji, tai, vibwaya na ngozi za wanyama.

Pia kuna mapambo ya kujipaka kama vile unga wa udongo wa rangi mbalimbali na mkaa uliosagwa. Mwigizaji hujipaka miguuni, mikononi, mwilini, usoni, midomoni na kwenye kucha za miguuni na mikononi. Baadhi ya makabila hujipamba kwa kujichora mwilini, kwenye nyusi na usoni. Hujichora mapambo hayo kwa kutumia rangi mbalimbali, udongo au mkaa uliosagwa. Wachezaji wengine hujipaka hina, kauta, poda, rangi za kucha, wanja na rangi za midomo.

Mapambo humsaidia mwigizaji kuonekana na kuleta uhalisia wa jambo analotaka kuwasilisha. Vilevile, humsaidia mwigizaji kubuni miondoko, mkao wa mwili, sauti ya uigizaji, jukwaa na mazingira anayoigizia kuwa na uhalisia. Kielelezo namba 1 kinaonesha watu waliovaa mapambo mbalimbali ya kuchezea ngoma.



**Kielelezo namba 1:** *Wachezaji wa ngoma wamevaa mapambo mbalimbali.*

FOR ONLINE USE ONLY



Stadi za Kazi darasa la 6.indd 69 23/07/2021 15:12

FOR ONLINE USE ONLY
DO NOT DUPLICATE

**Kazi za kufanya namba 1**

1. Katika vikundi vyenu igizeni kwa muda mfupi matendo mbalimbali yanayofanywa katika jamii zenu. Mfano kuimba, kupanda miti na kumpatia mgonjwa huduma ya kwanza.
2. Tengeneza mapambo mbalimbali ya kuvaa, kujipaka na kujichora wakati wa kuigiza.
3. Ukishirikiana na wenzako fanya ziara ya kutembelea kikundi cha uigizaji kilichopo karibu na shule yenu.

***Kughani ngonjera kwa kufuata utaratibu unaotakiwa***

Jadili na wenzako katika kikundi



1. Je, unafahamu nini kuhusu ngonjera?
2. Umewahi kughani ngonjera?
3. Ni hatua zipi za kufuata kabla ya kughani ngonjera?
4. Je, anayeghani ngonjera anapaswa kuwa na sifa zipi?

Ngonjera ni utunzi wa aina ya mashairi ya kimapokeo. Ngonjera ni majibizano baina ya watu wawili au pande mbili au zaidi. Watu hujibizana kwa lugha ya ushairi. Msemaji mmoja hutoa hoja kwa kuuliza swali katika ubeti uliotangulia na msemaji wa pili hutoa hoja kwa kumjibu mtoa hoja wa kwanza katika ubeti unaofuata.

Mara nyingi malumbano hayo hubeba ujumbe maalumu kwa wasikilizaji. Mwisho wa malumbano hayo hupatikana mwafaka. Pia ngonjera inaweza kuwa na ujumbe mmoja ambao hauhusishi malumbano. Ujumbe huo unaweza kuongelea ubaya au uzuri wa jambo au kitu kuanzia mwanzo hadi mwisho.

## Sifa za anayeghani ngonjera

Anayeghani ngonjera anapaswa kuwa na sifa zifuatazo:

(a) Awe ana uwezo wa kutamka maneno vizuri kwa sauti ya kusikika;

FOR ONLINE USE ONLY

FOR ONLINE USE ONLY
DO NOT DUPLICATE

(b) Awe mchangamfu;

(c) Ajue kuvaa vizuri uhusika kulingana na ujumbe uliopo;

(d) Ajue kutumia vema viungo vya mwili wake wakati wa kughani, yaani mikono, miguu na kiwiliwili chote; na

(e) Awe ana mawasiliano mazuri na wenzake na hadhira.

***Hatua za kughani ngonjera:*** Zifuatazo ni hatua za kughani ngonjera:

(a) Andaa ngonjera utakayoghani;

(b) Gawa beti za ngonjera kulingana na idadi yenu;

(c) Soma kwa makini kisha msimulie mwenzako;

(d) Soma tena ngonjera ili upate matendo ya kutenda kulingana na ujumbe uliomo; na

(e) Anza kughani ngonjera kwa usahihi na kwa kuzingatia sifa za kughani.

### Kazi ya kufanya namba 2

Ghani ngonjera zifuatazo kwa kufuata hatua zake

**a) Maisha ya mjini na vijijini**

(i) Hodi hodi twaingia, uwanjani tumefika,
Salamu zetu twatoa, kwa wadada na wakaka,
Ni mengi tutayatoa, muyapokee hakika,
Maisha yaliyo bora, wapi twaweza yapata?

(ii) Salamu twawatumia, mijini na vijijini,
Wala msije umia, mezani sogeleeni,
Mawazo kujivunia, pamoja tuwe mezani,
Maisha yaliyo bora, wapi twaweza yapata?

FOR ONLINE USE ONLY

FOR ONLINE USE ONLY
DO NOT DUPLICATE

(iii) Hebu kwanza sikiliza, jibu sasa unapata,
Ni mengi mnayowaza, majibu mtayapata,
Ni vizuri kujifunza, ukweli mkaupata,
Maisha yaliyo bora, vijijini mtapata.

(iv) Mengi tunayoyaona, mijini kote fedheha,
Aibu hata hawana, kila kukicha kuhaha,
Mipango inagongana, wakimbia kama mbweha,
Maisha yaliyo bora, vijijini mtapata.

(v) Hebu kwanza nyamazeni, mpate kunijulisha,
Leteni hoja mezani, tatizo kubainisha,
Mmekereka na nini, msitake nififisha,
Maisha yaliyo bora, tapataje vijijini?

(vi) Wale wote vijijini, ni wale hawakusoma,
Sisi wale wa mjini, ni wale tuliosoma,
Ndugu zetu vijijini, kimaisha wamekwama,
Maisha yaliyo bora, tapataje vijijini?

(vii) Hata kidogo si kweli, hayo unayobaini,
Vyakula vyetu asili, wala si vya viwandani,
Tunazijenga akili, afya zetu ni makini,
Maisha yaliyo bora, vijijini mtapata.

(viii) Acheni yenu maneno, mijini kumeshajaa,
Tazama msongamano, majumbani mmejaa,
Mtafaidi vinono, vijijini kirejea,
Maisha yaliyo bora, vijijini mtapata.

FOR ONLINE USE ONLY



Stadi za Kazi darasa la 6.indd 72 23/07/2021 15:12

FOR ONLINE USE ONLY
DO NOT DUPLICATE

(ix) Siyo kweli msemayo, na tena siyo makini,
Kwa sasa fateni nyayo, mjionee mijini,
Maisha tena si hayo, yalivyokuwa zamani,
Mjini kunapendeza, karibu mjionee.

(x) Bajaji na bodaboda, usafiri rahisisha,
Kina kaka kina dada, wanafaidi maisha,
Acheni makidakida, mjini kwafurahisha,
Mjini kunapendeza, karibu mjionee.

(xi) Maisha ya maigizo, huu si wakati wake,
Acheni yenu mizozo, wanaume wanawake,
Vijijini ni tulizo, ukweli siyo makeke,
Maisha yaliyo bora, vijijini mtapata.

(xii) Viyoyozi nazo feni, magonjwa jizalishia,
Mtapata ahueni, vijijini kirejea,
Kumbukeni majumbani, makwenu mje rejea,
Maisha yaliyo bora, vijijini mtapata.

(xiii) Kweli sasa naelewa, ukweli nimetambua,
Nilikuwa nimelewa, maisha kuzuzukia,
Shime wenzangu elewa, vijijini kurejea,
Maisha yaliyo bora, vijijini tutapata.

FOR ONLINE USE ONLY

**b) Rushwa ni sawa na Nyoka**

(i) Hodi hodi naingia, uwanjani nimefika,
Nakuja eleza nia, yaniondoke mashaka,



Stadi za Kazi darasa la 6.indd 73 23/07/2021 15:12

FOR ONLINE USE ONLY
DO NOT DUPLICATE

Na lengo kulifikia, linaloleta mwafaka,
Nyoka kiumbe mbaya, na tena hakumbatiwi.

(ii) Watutia mashakani, nyoka kumuongelea,
Nyoka huyu nyoka gani, unayemuongelea?
Ni yule wa msituni au nyoka wa kufugwa?
Nyoka kiumbe mbaya, kwa nini hakumbatiwi?

(iii) Nyoka kimkumbatia, lazima atakung'ata,
Sumuye takupatia, mauti yatakupata
Rushwa kafanania, kwa tabia na utata,
Rushwa ni sawa na nyoka, kimgusa takung'ata.

(iv) Mnyama huyu hatari, hupenda haribu watu,
Mlaghai na mahiri, kuteka akili zetu,
Ukikaa jihadhari, kucheza usithubutu,
Rushwa ni sawa na nyoka, usije mkumbatia.

(v) Kaenea ofisini, kazini hata shuleni,
Anafanya uhaini, haki kutia kapuni,
Yabidi kuwa makini, usimtie kwapani,
Rushwa kiikumbatia, daima takuharibu.

(vi) Watu wengi makazini, hongo nyingi hupokea,
Askari barabarani, mlungula hujipatia,
Haki zetu matatani, ni wapi takimbilia?
Rushwa kiikumbatia, daima takuharibu.

(vii) Rushwa ukiizoea, wajibu hutotimiza,
Ni bora kuizomea, wajibu kuutukuza,

FOR ONLINE USE ONLY

FOR ONLINE USE ONLY
DO NOT DUPLICATE

Wanyonge mwatuonea, sheria kuzipuuza,
Rushwa adui wa haki, hukwamisha haki zetu.

(viii) Sasa kweli naelewa, rushwa ni sawa na nyoka,
Elimu ingetolewa, ya sheria kwa hakika,
Haki zetu kuelewa, sote tungeelimika,
Rushwa ni sawa na nyoka, usije ikumbatia.

(ix) Sasa tuchapeni kazi, maendeleo takuja,
Pia tung'oe mizizi, kazi iwe na tija,
Maendeleo ni kazi, na siyo vitu vya kuja,
Rushwa adui wa haki, hudumaza maendeleo.

## Kazi ya kufanya namba 3

1. Kila mmoja atunge ngonjera yenye beti 4 inayohusu ubaya wa kuiba mali ya umma.
2. Kila mmoja aghani ngonjera aliyotunga.

## Zoezi la kwanza

**Sehemu A: Andika NDIYO kwa sentensi iliyo sahihi na HAPANA kwa sentensi isiyo sahihi**

1. Mtu mmoja anaweza kughani ngonjera --------------.
2. Ngonjera hutungwa kwa kufuata mtindo wa mashairi ya kimapokeo -------------.
3. Malumbano ya ngonjera hayana wasikilizaji -------------.
4. Mwanzo wa ngonjera huanza kwa kutoa hoja, na mwisho wake pande zinazolumbana hupata mwafaka -------------.

FOR ONLINE USE ONLY

FOR ONLINE USE ONLY
DO NOT DUPLICATE

**Sehemu B: Jibu maswali yafuatayo kwa kutoa maelezo.**

1. Je, ngonjera ni nini?
2. Ni zipi hatua za kughani ngonjera?
3. Je, unapoghani ngonjera unaweza kuonesha vitendo. Kwa nini?
4. Je, anayeghani ngonjera anapaswa kuwa na sifa zipi?

**Majigambo**

Kujigamba kwa kutumia wasifu wa vitu



Jadiliana na wenzako katika kikundi:

1. Je, kujigamba ni nini?
2. Majigambo ni nini?
3. Anayetamba majigambo anapaswa kuwa na sifa zipi?
4. Je, umewahi kusikia au kuona watu wakijigamba?

Msanii hutamba majigambo ya kijadi yaliyomo katika sanaa za maonesho. Msanii hutamba kwa kutumia maneno na vitendo. Vitendo hivi huonesha mambo aliyowahi kutenda au anayotarajia kuyatenda katika masuala mbalimbali ya kijamii. Mfano majigambo ya kivita, uwindaji, uchezaji ngoma, uganga, kusifu mali na viongozi wao. Mtambaji huweza kujisifu kwa kutumia maneno ya kusemwa kwa sauti au kwa kuimba.

Majigambo huchezwa na mtu mmoja, wawili au pande mbili au zaidi ambazo kila mmoja hujigamba dhidi ya mwenzake. Mtu anapojigamba hutumia mkusanyiko wa maneno yenye sifa zake binafsi, familia yake, shule, kabila au Taifa lake. Anayejigamba hutunga sifa zake kutokana na tukio katika maisha yake. Mfano wa matukio hayo ni kama vile kushinda vita, kurudisha mali iliyoibiwa, kulima shamba kubwa kuliko wengine. Mfano mwingine ni kushinda mashindano ya kukimbia, mashindano ya mpira wa miguu, mashindano ya kuimba kwaya au kufaulu mitihani.

FOR ONLINE USE ONLY

FOR ONLINE USE ONLY
DO NOT DUPLICATE

### Sifa za mtambaji wa majigambo

Mtambaji wa majigambo anapaswa kuwa na sifa zifuatazo:

1. Aweze kutumia lugha fasaha;
2. Aweze kutamka maneno kwa sauti ya kusikika na kwa usahihi;
3. Awe mchangamfu na shupavu; na
4. Aweze kutumia vema viungo vya mwili wake yaani kichwa, macho, mikono, miguu na hata kiwiliwili chote.

**Faida za majigambo:** Majigambo yana faida zifuatazo:

1. Kuburudisha jamii;
2. Kukuza uwezo wa kujieleza na kujiamini;
3. Kukuza stadi ya kujieleza katika lugha;
4. Kukuza ushujaa kwa wanajamii;
5. Kuendeleza mila na desturi za jamii inayohusika;
6. Kukuza uzalendo;
7. Kukuza stadi ya kujenga hoja kimantiki; na
8. Kuimarisha ushirikiano.

Soma kwa makini majigambo yafuatayo kisha chagua uhusika kati ya Mzee Maji na Mzee Moto.

1. Mimi ndiye Maji.

   Mimi ndiye niliyeshika uhai wa viumbe vyote duniani.

   Mijini na vijijini tegemeo lao ni mimi.

   Nisipokuwepo, maisha ya viumbe duniani yanasimama.

   Nani kama MAJI?

FOR ONLINE USE ONLY

FOR ONLINE USE ONLY
DO NOT DUPLICATE

2. Mimi ndiye moto!

   Mimi ndiye chanzo na chimbuko la maendeleo duniani.

   Utengenezaji wa zana bora za kisayansi ulianzia kwangu.

   Nani kama MOTO?

3. Nani amekudanganya?

   Binadamu tangu kuzaliwa kwake mpaka kufa kwake,

   Ananitegemea mimi.

   Ninamnywesha, ninamuogesha, ninasitawisha mimea ya mazao yake na

   Ninafua nguo zake. Bila mimi hakuna maisha.

   Nani kama MAJI?

4. Acha maneno wewe!

   Mimi huwaangazia wakati wa giza, mimi ni nuru,

   Huiangaza nuru katika giza, mimi ni ishara ya binadamu kuwasiliana,

   Binadamu hawezi kula bila ya mimi.

   Nani kama MOTO?

5. Mbona unajisifia sana?

   Wanyama na viumbe wote duniani, wananitegemea mimi.

   Mimea yote inanitegemea mimi.

   Bila ya mimi maji, hakuna maisha duniani.

   Nani kama MAJI?

6. Nani anajisifia?

   Sikiliza. Kwanza wewe huleta majanga ya mafuriko duniani.

   Mimi ndiye moto rafiki wa kweli wa binadamu na viumbe wengine.

   Nikitokeza sehemu, adui na wanyama wakorofi hufyata mikia na

FOR ONLINE USE ONLY



Stadi za Kazi darasa la 6.indd 78 23/07/2021 15:12

FOR ONLINE USE ONLY
DO NOT DUPLICATE

Kukimbia ovyo. Mimi ndiye Moto.

Nani kama MOTO?

7. Mimi ndiye Maji

   Ndani yangu wanaishi viumbe,

   Kwako ni kiumbe gani anaishi ndani yako?

   Samaki wa kila aina na mimea yenye kuvutia watalii vyote huishi ndani yangu.

   Mimi ni chanzo cha hewa safi kwa afya ya binadamu.

   Nani kama MAJI?

8. Acha mchongo wa maneno mimi ndiye moto,

   hakuna binadamu anaweza kula chakula bila mimi kutengeneza na

   ninaivisha ugali, nyama, ndizi na mboga za majani.

   Nani kama MOTO?

9. Funga mdomo wako wewe!

   Mimi ndiye Maji, juu yangu binadamu wanasafiri,

   Wanajipatia fedha kwa kuvua samaki,

   Wanajipatia protini na madini mengi, mimi ndiye maji, maji!

   Nani kama MAJI?

10. Mimi ndiye Moto! Moto!

    Kwangu adui hakai.

    Hata wewe maji ninao uwezo wa kukuchemsha ukawa wa moto.

    Kaa mbali na mimi.

11. Mimi ni tegemeo la dunia, viwandani, migodini kwenye

    Nyumba za ibada na majumbani

    Nikikosekana kila kiumbe hujua,



FOR ONLINE USE ONLY

Stadi za Kazi darasa la 6.indd 79 23/07/2021 15:12

FOR ONLINE USE ONLY
DO NOT DUPLICATE

Mimi ndiye Moto! Moto! Moto!

Nani kama MOTO?

12. Nyamaza kimya kuanzia sasa,

Mimi ninao uwezo wa kukuzima na ukapotea kabisa

Na pale unapoleta majanga mimi huitwa

Na nikifika ninakudhibiti kabisa, au unajitoa fahamu?

Mimi ndiye maji bwana! Maji, maji!

Nani kama MAJI?

**Kazi ya kufanya namba 4**

1. Kaa katika kikundi cha wanafunzi wasiozidi sita.
2. Kila kikundi kichague wanafunzi wa kuwakilisha katika majigambo dhidi ya kikundi kingine.
3. Kila kikundi kichague kitu cha kujigamba.
4. Kila kikundi kitambe majigambo mbele ya wenzao kwa kushindana na kikundi kingine.

## Maigizo ya kuganda

Maigizo ya kuganda ni aina ya uigizaji ambayo muigizaji hajitikisi mwili, hajongei wala hatumii sauti. Katika uigizaji huu, mwigizaji hukaa na kutulia kama sanamu. Mfano wa uigizaji huu ni kama inavyofanyika katika halaiki ambapo wahusika hushika karatasi ambazo huunda maneno ambayo husomeka kwa watazamaji. Kulingana na nguo zilizovaliwa washiriki wa halaiki huweza kukaa mkao unaotengeneza Bendera ya Taifa au kuandika namba inayokusudiwa.

FOR ONLINE USE ONLY



Stadi za Kazi darasa la 6.indd 80 23/07/2021 15:12

FOR ONLINE USE ONLY
DO NOT DUPLICATE

Maigizo haya yanaweza yakafanyika pia kwa washiriki kusimama katika mkao ambao watazamaji wanaweza kutafsiri juu ya kile kinachofanyika. Kwa mfano, waigizaji wawili wanaweza kusimama kimya wakiwa wamekunja ngumi na kutazamana kuonyesha ishara ya kupigana. Maigizo ya kuganda siyo lazima yawe na mapambo maalumu.

**Faida za maigizo ya kuganda**

Baadhi ya faida za maigizo ya kuganda ni:

a) Kukuza ushirikiano;

b) Kujenga hali ya kujiamini;

c) Kukuza stadi ya ubunifu;

d) Kuimarisha afya ya mwili; na

e) Kukuza usikivu.

**Kazi ya kufanya namba 5**

1. Katika vikundi vyenu igiza kwa usahihi matendo yafuatayo:

   (a) Mtu anayesoma kwa umakini;

   (b) Mama anayepika chakula; na

   (c) Mtoto anayeomba msamaha kwa wazazi.

2. Tembelea kikundi cha maigizo kilicho jirani na shule na kisha chunguza uigizaji wa kuganda unavyofanyika au angalieni mkanda wa video wa maigizo kuona uigizaji wa kuganda unavyotendeka

FOR ONLINE USE ONLY

FOR ONLINE USE ONLY
DO NOT DUPLICATE

## Zoezi la pili

**Sehemu A: Oanisha maneno ya fungu "A" na yale ya fungu "B" ili kupata majibu sahihi.**

| Na. | Fungu "A" | | Fungu "B" |
|---|---|---|---|
| 1 | Ngonjera | A | Hali ya mazungumzo ambayo watu zaidi ya mmoja huzungumza kwa kupokezana. |
| 2 | Majibizano | B | Kifungu kimojawapo katika vifungu vingi vya maneno kilichopangwa kwa mishororo, mistari miwili au zaidi katika shairi au ngonjera. |
| 3 | Ubeti | C | Utunzi wa aina ya mashairi ya kimapokeo au majibizano ya watu wawili au pande mbili au zaidi. |
| 4 | Uigizaji | D | Vipande viwili katika mshororo. |
| 5 | Maigizo | E | Sanaa katika fasihi simulizi ambayo watendaji wake ndiyo wahusika wakuu. |
| | | F | Uwasilishaji wa uhalisia wa maisha na shughuli za kila siku za binadamu kwa njia ya utendaji mbele ya hadhira hai. |

**Sehemu B: Andika "Ndiyo" kwenye sentensi sahihi na "Hapana" kwa sentensi ambayo si sahihi**

1. Mapambo ya kuvaa ni bangili, kago, hereni, kipini na mkufu.
2. Ngonjera ni utunzi wa aina ya mashairi ya kisasa.
3. Majigambo hayakuzi stadi ya lugha ya kujieleza.
4. Moja ya faida za igizo mgando ni pamoja na kujenga ushirikiano, kujiamini na usikivu.



Stadi za Kazi darasa la 6.indd 82 23/07/2021 15:12

FOR ONLINE USE ONLY
DO NOT DUPLICATE

**Sehemu C: Jibu maswali yafuatayo kwa kutoa maelezo**

1. (a) Nini maana ya majigambo?

   (b) Kujigamba ni nini?

2. Taja faida tano za majigambo katika jamii

3. Orodhesha sifa za mtambaji wa majigambo

4. Taja matukio matatu anayoweza kutumia mtambaji wa majigambo kujigamba.

## Msamiati

| | |
|---|---|
| **Keekee** | Bangili kwa ajili ya urembo inayovaliwa mguuni kwa mwanamke |
| **Kikuku** | Bangili maalum ya madini ya fedha au dhahabu inayovaliwa na wanawake mguuni kwa lengo la kujiremba |
| **Kishaufu** | Ni pambo linalovaliwa na wanawake kwenye uti wa pua |
| **Kitani** | Nyuzi zinazotokana na gome la mti wenye asili ya India ambao hutumika kutengeneza vitu kama vile magunia, mazulia na kamba |
| **Kushaufu** | Hali ya kuringa au majisifu |
| **Maleba** | Mavazi maalumu yanayovaliwa na wasanii wanapokuwa wanafanya maonesho |
| **Nakshi** | Urembo utokanao na matokeo ya kuchora, kutarizi au kuchonga |
| **Nyerere** | Madini ya waya nyembamba ambayo baadhi ya makabila hutumia kama pambo la mkononi na mguuni |

FOR ONLINE USE ONLY

FOR ONLINE USE ONLY
DO NOT DUPLICATE

# Sura ya Sita

## Picha, vichezeo na uchapaji

### Utangulizi

*Ulipokuwa Darasa la Tano ulijifunza usanii wa picha kwa kutumia mbinu mbalimbali. Baadhi ya mbinu hizo ni uchoraji kwa kutumia penseli na usanii wa picha kwa kutumia rangi. Ulijifunza pia ufinyanzi na ususi wa vitu mbalimbali. Katika sura hii utajifunza usanii wa picha za kubandika kwa kutumia makunzi mbalimbali, upatikanaji wa motifu pamoja na matumizi yake katika kuchapa ruwaza. Zaidi ya hapo utajifunza jinsi ya kutengeneza fremu ya kubeba picha na ruwaza. Mwisho utajifunza kutumia kanuni anuwai zinazoongoza usanii wa picha kwa ujumla.*

### Picha za kubandika

Zipo picha zinazoonekana kwa macho tu bila kushikika. Mifano ya picha hizo ni michoro, picha za rangi, picha za kuchapwa na zile zinazotokana na kamera. Aina nyingine ni picha zinazoonekana na kushikika. Picha za aina hii hutengenezwa kwa njia mbalimbali. Moja ya njia hizo ni utengenezaji wa picha za kubandika. Hii inatokana na namna picha hizo zinavyopatikana. Vitu vinavyobandikwa ili kuibua picha hizo ni kama vile karatasi, majani, mbegu za nafaka, vitambaa, mchanga, manyoya na vitu vingine vinavyopatikana katika mazingira. Ili picha iweze kubandikwa ni lazima ishikizwe kwenye fremu. Fremu zinaweza kuwa kipande cha ubao, karatasi ngumu, bati, ngozi, plastiki na hata ukuta. Picha hubandikwa kwenye fremu kwa kuzingatia kanuni za sanaa ya picha. Baadhi ya kanuni hizo ni ulinganifu wa maumbo ya picha katika fremu, mwafaka wa rangi za picha na matumizi sahihi ya nafasi ya fremu.

FOR ONLINE USE ONLY




Stadi za Kazi darasa la 6.indd 84 23/07/2021 15:12

FOR ONLINE USE ONLY
DO NOT DUPLICATE

### Kutengeneza picha za kubandika

Kielelezo namba 1 kinaonesha picha ya kubandika.



**Kielelezo namba 1:** *Picha ya kubandika*

Katika kutengeneza picha za kubandika unaweza kuanza na uandaaji wa makunzi na fremu.

***Uandaaji wa makunzi:*** Unaweza ukapata makunzi kutokana na vyanzo mbalimbali kama vile:

1. Vitambaa – kutoka kwa mafundi cherahani;
2. Ngozi au turubali – kutoka kwa watengenezaji viatu, makochi na mikoba;
3. Mchanga – kutoka sehemu mbalimbali kama zinapojengwa nyumba;
4. Plastiki – kutoka kwenye mazingira au vifaa visivyotumika tena;
5. Punje za nafaka - kwa kununua sokoni au kwenye maduka ya vyakula, kuokota shambani au bustanini;
6. Shanga – kununua; na
7. Majani mapana ya migomba au ya miwa.

FOR ONLINE USE ONLY

FOR ONLINE USE ONLY
DO NOT DUPLICATE

Ni lazima makunzi yasafishwe ili yawe safi kabla ya kubandikwa. Makunzi safi hubandikwa kwa urahisi na huwa madhubuti. Makunzi yakiwa na uchafu gundi hushindwa kunatisha kwa umadhubuti na picha yake haitapendeza. Kila aina ya makunzi yanasafishwa kwa namna yake, kwa mfano:

1. Vitambaa – hukung'utwa vumbi, hufuliwa kisha hupigwa pasi;
2. Ngozi – hupukutwa na pia kusafishwa kwa brashi;
3. Mchanga - huoshwa kwenye maji ili kuondoa udongo na vumbi. Pia huchambuliwa au kuchekechwa ili kuondoa vipande visivyo mchanga;
4. Plastiki – hufutwa kwa kitambaa au kusafishwa kwa maji na sabuni;
5. Mbegu au punje – hupepetwa. Hizi hazitiwi maji kwani maji hubadilisha mwonekano wake; na
6. Majani mapana – hupukutwa na kufutwa kwa kitambaa kikavu.

***Utayarishaji wa fremu ya kubandika picha:*** Fremu ya picha ni ule uso ambao picha hubandikwa. Karatasi ngumu kama zile zitumikazo kutengeneza makasha, ubao mpana wa dari, bapa la plastiki, ubao, kipande cha bati na ngozi vinaweza kutumika kutengeneza fremu za picha. Fremu ya picha hupimwa urefu na upana na kukatwa kulingana na ukubwa wa picha itakayotengenezwa. Baada ya fremu kukatwa husafishwa tayari kwa ajili ya zoezi la utungaji wa picha.

***Utungaji wa picha ya kubandika:*** Baada ya kuandaa makunzi na fremu, inafuata hatua ya utungaji wa picha. Kutunga picha ni kuibua wazo la picha na kuliwasilisha katika taswira ya kuonekana. Wazo hilo hupangiliwa kwa kufuata kanuni za usanii wa picha. Kanuni za usanii wa picha zinaongoza utunzi wa picha ili usiwe wa kiholela bali uwe wa kisayansi. Kanuni hizo huufanya utungo huo ulete mwonekano uliokusudiwa na msanii. Kanuni hizo ni kama vile: Mizania, msigano au ukinzani, mkazo, wizani, ruwaza, umoja na uaina.

FOR ONLINE USE ONLY

FOR ONLINE USE ONLY
DO NOT DUPLICATE

***Sifa za picha ya kubandika:*** Yapo mambo ambayo msanii anapaswa kuzingatia anaposanii picha za kubandika. Baadhi ya mambo hayo ni haya yafuatayo:

1. Maumbo ya picha yawe sahili;
2. Maumbo yasiwe na vijisehemu vidogovidogo;
3. Makunzi yawe yanayoweza kubandikwa vizuri kwa gundi;
4. Makunzi yawe makavu kabisa na yanayodumu kwa muda mrefu;
5. Makunzi yasiwe yanayopauka rangi au kusinyaa;
6. Mbegu na punje huliwa na wadudu. Endapo zitatumika ziwekewe kinga ili wadudu wasizifikie; na
7. Rangi za picha ya kubandika ni zile za asili zilizomo kwenye makunzi yenyewe. Kamwe usipake rangi yoyote.

## Kupangilia maumbo katika fremu ya picha

Kupangilia maumbo ya picha ni kuyaweka maumbo kwenye fremu ya picha bila kuyabandika ili uone picha itakavyojitokeza. Hapo unaweza kuyapanga na kupangua hadi uridhike na mwonekano utakaopendeza zaidi. Picha huwa na sehemu kuu tatu. Sehemu ya mbele, sehemu ya kati na sehemu ya nyuma. Sehemu ya mbele hubeba maumbo yanayokuwa kwenye uso wa picha. Sehemu ya kati hubeba maumbo yanayokuwa nyuma ya yale ya mbele. Sehemu ya nyuma hubeba maumbo ya nyuma ya picha. Maumbo ya mbele huwa makubwa na yenye kuonekana kinaganaga. Maumbo ya kati huonekana madogo kidogo yakilinganishwa na yale ya mbele. Pia, baadhi hukingwa na yale ya mbele na hivyo kuonekana baadhi ya sehemu tu. Maumbo ya nyuma huonekana madogo zaidi ya yale ya kati. Maumbo hayo hufifia rangi na hayaonekani kinaganaga kama yale ya mbele na kati. Maumbo yanayounda picha yanapaswa kujaza fremu ya picha. Hivyo, unapopangilia maumbo ya picha kwenye fremu zingatia kanuni hizo. Kielelezo namba 2 kinaonesha sehemu kuu tatu za picha.

FOR ONLINE USE ONLY



Stadi za Kazi darasa la 6.indd 87 23/07/2021 15:12

FOR ONLINE USE ONLY
DO NOT DUPLICATE



**Kielelezo namba 2:** *Sehemu kuu tatu za picha*

**Kubandika maumbo ya picha kwenye fremu**

Hatua inayofuata baada ya kupanga maumbo ni kutia gundi nyuma ya maumbo na kuyabandika kwenye fremu. Mambo muhimu ya kuzingatia hapa ni usafi na uimara. Picha inapaswa kuwa safi ili iwavutie watazamaji, watumiaji na hata wanunuzi wake. Usafi utatokana hasa na maandalizi sahihi ya makunzi, usafi wa eneo la kazi na upakaji sahihi wa gundi. Gundi ipakwe upande wa nyuma wa umbo linalobandikwa. Uimara wa picha utatokana na usahihi wa fremu. Kwa mfano, ukitumia punje za nafaka katika picha utapaswa kutumia fremu imara kwani punje ni nzito. Gundi imara na ya kutosha huongeza uimara wa picha. Kwa mfano, usitumie gundi ya ofisini kubandikia makunzi mazito kama vile punje mbalimbali za nafaka, badala yake utapaswa kutumia gundi nzito kama ya mbao.

**Kukamilisha picha:** Kukamilisha picha ni kurekebisha maeneo mbalimbali ya picha kwa kuisawazisha na kuihifadhi. Wakati wa kukamilisha picha, itakupasa kufanya mambo yafuatayo:

1. Kagua maeneo ambayo hayakukamilika vizuri ili kuyakamilisha kwa mfano, kama gundi haikushika vizuri sehemu fulani ya maumbo;
2. Ongeza madoido yatakayozidi kupendezesha picha;



Stadi za Kazi darasa la 6.indd 88 23/07/2021 15:12

FOR ONLINE USE ONLY
DO NOT DUPLICATE

3. Pulizia picha utandu wa kuzuia wadudu waharibifu hasa wa karatasi na mbegu;
4. Iache picha kwa muda ili ikauke; na
5. Weka picha kwenye fremu.

**Hatua za kusanifu picha ya kubandika kwa kutumia karatasi:** Unaweza kusanifu picha ya kubandika kwa kutumia karatasi. Karatasi zina sifa nzuri sana katika kusanifu picha hupatikana katika aina na rangi mbalimbali. Baadhi ya sifa hizo ni kuwa hukatika na hubandikwa vizuri, hudumu kwa muda mrefu na hupatikana kwa urahisi. Katika kusanifu picha za kubandika kwa kutumia karatasi fuata hatua zifuatazo:

1. Kusanya karatasi za aina na rangi mbalimbali;
2. Andaa karatasi kwa kuzinyoosha, kuzikata na kuziainisha;
3. Buni picha;
4. Andaa aina ya fremu itakayofaa kubebea picha yako;
5. Pangilia maumbo ya picha hadi ipendeze kabla ya kuyabandika;
6. Bandika maumbo ya picha;
7. Hakiki picha ili uone kama imebandikwa vizuri;
8. Iache picha kivulini kwa muda fulani ili ikauke; na
9. Hifadhi picha yako kwa kupulizia utando au kuweka kwenye fremu yenye kioo.

**Kazi ya Kufanya namba 1**

1. Tengeneza picha ya kubandika kwa kutumia karatasi. Tumia fremu ya kasha na picha iwe na urefu wa sm 40 na upana wa sm 30.
2. Kaa katika kikundi cha wanafunzi wasiozidi watano kisha mbuni na kusanifu picha ya kubandika. Tumieni punje za nafaka aina tofauti zenye kutofautiana rangi. Saizi ya picha iwe urefu sm.60 na upana sm.30. Zingatia hatua sahihi za kusanifu picha ya kubandika.

FOR ONLINE USE ONLY



Stadi za Kazi darasa la 6.indd 89 23/07/2021 15:12

FOR ONLINE USE ONLY
DO NOT DUPLICATE

**Zoezi la kwanza**


Andika insha fupi juu ya "Uboreshaji wa mazingira kwa kutumia sanaa ya picha za kubandika".

## Kubuni chapa za sanaa za ufundi


Uchapaji ni ufundi wa kisanaa wa kunakili picha, maumbo, alama au michoro katika wingi na mfanano. Sanaa ya uchapaji hutumika sana katika maisha yetu. Kutokana na uchapaji tunapata vitu kama vile kalenda, vitabu, magazeti, kadi, mabango na picha. Uchapaji katika sanaa unajitokeza kama mapambo kwenye vitu kama nguo, mazulia, mapazia, vitambaa vya mezani na vitu vingine vingi. Uchapaji wa mapambo katika sanaa unaanza na kubuni kisha kuandaa motifu.

## Motifu ni nini?

Kielelezo namba 3 na 4 vinaonesha motifu na ruwaza mbalimbali. Kielelezo namba 4 kinaonesha motifu mbalimbali na jinsi zinavyoweza kupangiliwa kwa mitindo tofauti na kuweza kupendezesha ruwaza.



**Kielelezo namba 3:** *Motifu*




**Kielelezo namba 4:** *Ruwaza*

FOR ONLINE USE ONLY

FOR ONLINE USE ONLY
DO NOT DUPLICATE


Kielelezo namba 3 kinaonesha alama 3 tofauti. Kila alama moja hapo huitwa motifu. Katika kilelelzo Na. 4 mpangilio wa motifu hizo huitwa ruwaza. Ukiangalia utaona alama zilezile zimewekwa kwa kurudiarudia tena kwa mpangilio tofauti. Chunguza mpangilio katika safu ya kwanza, ya pili na ya tatu ya alama hizo. Ruwaza ni namna mpangilio wa vitu ulivyo katika nafasi fulani. Zipo ruwaza za aina nyingi katika mazingira yetu. Ruwaza zaweza kuonekana kwenye nguo, mazulia, sakafu za vigae, miili ya wanyama, wadudu, mapazia, masega ya asali, utando wa buibui na vitu vingine. Katika sanaa ruwaza hutumiwa zaidi katika upambaji. Kielelezo namba 5 kinaonesha picha za ruwaza zikiwa sehemu mbalimbali.



*Ruwaza kwenye kitambaa*



*Ruwaza kwenye pazia*




*Ruwaza kwenye sakafu ya vigae*

FOR ONLINE USE ONLY




Stadi za Kazi darasa la 6.indd 91 23/07/2021 15:12

FOR ONLINE USE ONLY
DO NOT DUPLICATE



*Ruwaza kwenye manyoya ya tausi*



*Ruwaza kwenye ngozi ya twiga*

**Kielelezo namba 5:** *Picha za ruwaza zikiwa sehemu mbalimbali*

Ruwaza huundwa na motifu. Motifu ni alama ya msingi katika uchapaji. Zipo motifu za asili na zile za kubuniwa. Motifu za asili ni kama vile ramani za maumbo ya majani, viganja, nyayo za watu na wanyama, kokwa za matunda na maganda magumu kama vile vifuu vya nazi. Motifu za kubuni ni kama zile zinazochongwa, mathalani maumbo ya kijiometri, namba, herufi na alama mbalimbali. Aina nyingine ya motifu ni zile zilizotengenezwa kutokana na midomo ya chupa au vikombe, mikato ya matawi ya mimea yenye uwazi katikati, nati na vingine vingi. Jambo la msingi ni ubunifu wa msanii katika kutumia mazingira ili kuibua motifu zinazokidhi mahitaji yake ya uchapaji.

Kumbuka kuwa motifu utakazotumia kuchapa zitapaswa kuendana na dhana au dhamira ya ruwaza itakayochapwa. Kwa mfano, kitambaa cha mezani kitakuwa na maana zaidi endapo kitakuwa na motifu za matunda. Katika kuchonga motifu, msanii anaweza akatumia vifaa kama vile visu, nyembe au vifaa vingine vyenye ncha kali. Makunzi yanayofaa kuchonga motifu ni maada laini kama vile viazi mviringo, muhogo, mpira wa ndala, na miti laini.

Hatua za kuchonga motifu ni kama zifuatazo:

1. Tafuta makunzi laini kama vile kiazi mviringo;

2. Safisha kiazi;

FOR ONLINE USE ONLY

FOR ONLINE USE ONLY
DO NOT DUPLICATE

3. Kata kiazi nusu ili upate uso bapa;

4. Chora umbo la motifu kwenye uso bapa wa kiazi; na

5. Chonga umbo la motifu ili litokeze juu ya usawa wa uso wa kiazi.

Uchongaji wa motifu unahitaji kuzingatia sifa zifuatazo:

1. Usafi wa uchongaji;

2. Usahihi wa umbo;

3. Ukali wa vichongeo;

4. Umbo lisiwe na vijisehemu vidogovidogo;

5. Umbo kujitokeza vema juu ya uso wa kiazi; na

6. Usalama, kuwa na tahadhari kwani zana zinazotumika zina ncha kali.

**Kuchapa ruwaza ya motifu za kijiometri**

Ruwaza ni mpangilio wa motifu kwa namna ambayo itaunda pambo. Mfano wa mavazi kama khanga na vitenge hupambwa kwa motifu zilizopo katika ruwaza. Ukichunguza mavazi hayo, utaona yana alama na maumbo yaliyopangiliwa kwa kanuni za usanii wa picha zinazoongoza utunzi wa picha ili usiwe wa kiholela bali uwe wa kisayansi. Kanuni hizo huufanya utungo huo ulete mwonekano uliokusudiwa na msanii ambazo ni:

1. Mizania;

2. Msigano au ukinzani;

3. Umoja na uaina;

4. Mkazo; na

5. Wizani.

Hivyo ruwaza huchapwa kwa kuzingatia kanuni hizi.


FOR ONLINE USE ONLY



Stadi za Kazi darasa la 6.indd 93 23/07/2021 15:12

FOR ONLINE USE ONLY
DO NOT DUPLICATE

1 **Mizania:** Motifu zinazounda ruwaza huwekwa katika mpangilio unaoleta ulinganifu ambao unaweza kuonekana kwa macho. Motifu husambazwa kwenye ruwaza katika uzito sawa kati ya motifu za upande wa kushoto na kulia. Vivyo hivyo, kwa maumbo ya upande wa juu na wa chini wa ruwaza. Kielelezo namba 6 kinaonesha mizania ya motifu katika ruwaza.



**Kielelezo namba 6:** *Mizania ya motifu katika ruwaza*

2 **Ukinzani:** Hii ni ile hali ya kutofautiana kwa sura za motifu. Kwa mfano, motifu za duara dhidi ya motifu za mstatili. Motifu za rangi ya njano dhidi ya motifu za rangi nyeusi. Motifu zingine zikielekea juu na zingine zikielekea chini. Kielelezo namba 7 kinaonesha ukinzani au msigano wa motifu za ruwaza.




**Kielelezo namba 7:** *Ukinzani au msigano wa motifu za ruwaza*



Stadi za Kazi darasa la 6.indd 94 23/07/2021 15:12


FOR ONLINE USE ONLY
DO NOT DUPLICATE

3 **Umoja na uaina:** Hapa ni pale ambapo motifu zinakuwa ni zilezile ila kwa mpangilio, rangi na mielekeo tofauti. Kwa mfano, motifu ya tunda la nyanya kama kielelezo namba 8 kinavyoonesha. Motifu ya kwanza kikonyo cha nyanya kimeelekea kulia, motifu ya pili kikonyo kimeelekea kushoto. Motifu ya tatu kikonyo kimeelekea chini. Hiyo ni mielekeo, kuhusu rangi, motifu hizohizo zinaweza kutofautiana mwonekano. Mathalani, motifu za mstari wa kwanza zina rangi ya kijani na za mstari wa pili zina rangi ya njano na mstari wa tatu nyanya ina rangi nyekundu.



**Kielelezo namba 8:** *Umoja na uaina*

4 **Mkazo:** Motifu mojawapo katika pambo au picha inakuwa kivutio cha macho kwa watazamaji. Motifu ya namna hii huonesha mkazo wa motifu zingine kwa kutofautisha rangi moja. Kielelezo namba 9 kinaonesha motifu inayoonesha mkazo katika ruwaza.




**Kielelezo namba 9:** *Motifu inayoonesha mkazo katika ruwaza*

FOR ONLINE USE ONLY

FOR ONLINE USE ONLY
DO NOT DUPLICATE

5 **Wizani:** Ni mpangilio wa kurudiarudia kwa maumbo katika ruwaza ambao unaashiria mwendo wa mwelekeo fulani. Maumbo yanayoashiria kubiringika kuelekea kulia na kushoto. Kielelezo namba 10 kinaonesha wizani katika ruwaza.



**Kielelezo namba 10:** *Wizani katika ruwaza*

**Hatua za kuchapa ruwaza**

Ruwaza huchapwa kwa kupitia hatua zifuatazo:


1. Buni aina ya bidhaa – kama vile kitambaa cha mezani;
2. Buni motifu zitakazofaa kwa ajili ya kitambaa cha mezani;
3. Andaa makunzi ya kuchongea motifu na vifaa vya kupiga chapa;
4. Chonga motifu;
5. Pima saizi ya ruwaza kwenye karatasi;
6. Gawa na kuchora vyumba vya kupangilia motifu za ruwaza kwenye karatasi hiyo;
7. Chapa motifu katika vyumba vya ruwaza; na
8. Anika kazi kivulini hadi ikauke.

FOR ONLINE USE ONLY

FOR ONLINE USE ONLY
DO NOT DUPLICATE

## Maumbo ya kijiometri

Maumbo ya kijiometri ni chanzo cha motifu ambazo huweza kutumiwa kuunda ruwaza. Baadhi ya maumbo hayo ni duara, mraba, mstatili, msambamba sawa, pembe tatu sawa na pembe tatu mraba. Kielelezo namba 11 kinaonesha mifano ya motifu za maumbo ya kijiometri.




**Kielelezo namba 11:** *Motifu za maumbo ya kijiometri*

### Kazi za kufanya namba 2


1. Chagua maumbo matatu tofauti ya kijiometri.
2. Chonga motifu ya kila aina moja ya umbo la kijiometri ulilochagua.
3. Chapa ruwaza ya motifu hizo za kijiometri katika karatasi.

***Angalizo:*** *Hakikisha unachapa kwa kuzingatia kanuni na hatua za kuchapa ruwaza. Tumia rangi za aina tatu tu.*

**Kuweka fremu kwenye ruwaza:** Zipo aina mbili za fremu. Fremu ya aina ya kwanza ni ule uso ambao picha hukaa. Fremu ya aina ya pili ni ukanda unaowekwa pembezoni mwa picha ili kuipa mwonekano nadhifu. Baada ya kuchapa ruwaza hukamilishwa kwa kuweka ukanda pembezoni mwa fremu. Kielelezo namba 12 kinaonesha ruwaza yenye fremu ya utepe.

FOR ONLINE USE ONLY

FOR ONLINE USE ONLY
DO NOT DUPLICATE



**Kielelezo namba 12:** *Ruwaza yenye fremu ya utepe*

**Hatua za kutengeneza fremu kwenye ruwaza:** Unapotengeneza fremu kwenye ruwaza yakupasa kufuata hatua zifuatazo:

1. Andaa karatasi imara ya utepe. Chagua rangi itakayoendana na rangi za ruwaza yako;
2. Pima eneo la fremu ya ruwaza na utepe;
3. Kata utepe kutokana na karatasi imara;
4. Paka gundi upande mmoja wa utepe; na
5. Bandika utepe pembezoni mwa fremu ya ruwaza.

## Pambo la Kuchapa

Mapambo hupatikana kwa kupitia njia nyingi kama vile kuchora, kuchapa, kuunda, kupangilia na kuremba. Katika kipengele hiki tutajifunza namna ya kutengeneza pambo kwa njia ya kuchapa.

**Hatua za kuchapa pambo:** Zifuatazo ni hatua za kuchapa pambo:

1. Chagua jani pana lenye umbo zuri na lenye unamu unaochapika vizuri;
2. Pima fremu itakayobeba pambo;
3. Kata fremu katika saizi utakayopenda;

FOR ONLINE USE ONLY

FOR ONLINE USE ONLY
DO NOT DUPLICATE

4. Bandika karatasi nyeupe ya manila kufunika ubao wa fremu. Unaweza pia kufunika kwa kupaka rangi tabaka mbili;
5. Chagua rangi za aina tatu tofauti au zaidi utakazotumia. Changanya rangi hizo na mafuta ya taa ili kuzilainisha;
6. Andaa majani matatu yanayolingana saizi na kufanana;
7. Paka rangi sehemu ya juu ya jani kwa kutumia brashi. Kila jani liwe na rangi tofauti na lingine. Brashi moja itumike kwa aina moja ya rangi;
8. Hakikisha rangi inaenea eneo zima la uso wa jani;
9. Laza jani kwenye karatasi uliyobandika kwenye fremu. Uso wa jani wenye rangi ulalie karatasi;
10. Kandamiza jani kwa ubapa wa mkono au hata vidole hadi jani lote liguse karatasi. Baada ya hapo, bandua jani kutoka kwenye karatasi;
11. Endelea kuchapa kwa jani hapa na pale kwa rangi moja hadi lienee theluthi moja ya fremu;
12. Endelea na jani la pili lenye rangi ya pili. Chapa kama ulivyofanya katika hatua za jani la kwanza. Utakuwa umejaza theluthi ya pili ya fremu;
13. Kamilisha kwa jani la tatu lenye rangi ya tatu;
14. Malizia pambo kwa kujazia sehemu unazoona bado zina uwazi mkubwa; na
15. Weka pambo kivulini ili likauke taratibu.


***Angalizo:*** *Unapochapa maumbo ya majani hakikisha kuwa yanaingiliana. Kielelezo namba 13 kinaonesha hatua za kuchapa motifu za majani na mfanano wake.*

FOR ONLINE USE ONLY



Stadi za Kazi darasa la 6.indd 99 23/07/2021 15:12

FOR ONLINE USE ONLY
DO NOT DUPLICATE



**Kielelezo namba 13:** *Hatua za kuchapa kwa motifu za majani*

**Kuweka pambo fremu ya utepe**


Mahitaji au vifaa:

Rula, karatasi za manila za rangi mbalimbali, mkasi, penseli na gundi.

Hatua

1. Pima eneo la fremu ya pambo;
2. Chagua karatasi yenye rangi inayooana na zile za pambo;
3. Pima kisha kata tepe za karatasi hiyo zenye upana wa sentimeta 2 au 3 zitakazozunguka pambo;
4. Paka gundi vizuri tepe hizo na zibandike pembezoni mwa fremu; na
5. Weka pambo sehemu yenye hewa ili utepe wa fremu ukauke vizuri.

Kielelezo namba 14 kinaonesha pambo lililochapwa lenye fremu ya utepe.



**Kielelezo namba 14:** *Pambo la kuchapa lenye fremu ya utepe*

FOR ONLINE USE ONLY

FOR ONLINE USE ONLY
DO NOT DUPLICATE

**Kazi ya kufanya namba 3**

Chapa pambo kwa kutumia motifu za majani mapana. Tumia rangi za msingi yaani njano, bluu na nyekundu paka rangi moja kwa jani au motifu moja.

## Sifa za pambo

Pambo liwe safi. Motifu za pambo ziingiliane, pambo liwe na saizi ya upana wa sentimeta 24 na urefu wa sentimeta 35 kwa mazoezi ya darasani

### Kutengeneza maleba au mavazi bandia

Watu hutumia mavazi bandia na mapambo kwa ajili ya shughuli mbalimbali. Shughuli hizo zinaweza kuwa maigizo, kuwinga ndege au maadhimisho ya kitu fulani mithili ya sikukuu. Waigizaji huvaa mavazi yanayolandana na dhamira ya igizo lao. Katika sehemu hii utajifunza kutengeneza vazi la kuigizia kwa kutumia mfuko wa sandarusi na karatasi.

### Mahitaji au vifaa

Mfuko wa sandarusi, uzi mnene, sindano kubwa, mkasi, brashi za bapa, rangi za msingi za mafuta, mafuta ya taa, vikopo vidogo vinne vya nusu lita na vibanio vya nguo.

**Hatua za kutengeneza maleba:** Unapotengeneza maleba unatakiwa kufuata hatua zifuatazo:

1. Tafuta kifuko cha sandarusi na kisha ukisafishe;
2. Jipime urefu wako, upana wa kifua chako na pima saizi hiyo kwenye kifuko cha sandarusi kisha tia alama;
3. Weka alama ya umbo la nusu duara katikati ya sehemu ya kitako cha mfuko huo itakayoonesha tundu la shingo. Kama ilivyooneshwa kwenye Kielelezo namba 15, kata kufuatia alama ulizoweka ili kupata saizi uliyokusudia;
4. Kata umbo la nusu duara kwenye pembe mbili za mfuko wa sandarusi ili kupitisha mikono. Maleba hiyo itakuwa na mikono ya mkato;

FOR ONLINE USE ONLY

FOR ONLINE USE ONLY
DO NOT DUPLICATE

5. Pinda sehemu ya shingo na mikono ya sandarusi kwa mshono wa blanketi; na

6. Tumia brashi na rangi za mafuta katika kuchora mapambo kwenye vazi hilo. Baada ya hapo shona sehemu zingine zote. Pambo hilo liwe na mwelekeo wa dhana itakayoigizwa. Kwa mfano, igizo la UKIMWI linaweza kuchorwa alama ya fuvu na mifupa kwa rangi nyeusi, nyekundu au nyeupe.

**Upakaji rangi kwenye vazi la sandarusi:** Hatua za upakaji wa rangi kwenye vazi la sandarusi ni kama zifuatazo:

1. Chora mipaka ya pambo lako kwa kalamu ya wino;
2. Chora sura ya pambo kwa wino;
3. Paka rangi katika picha ya pambo pasipo rangi kuingiliana. Subiri mpaka rangi ya kwanza ikauke ndipo upake rangi ya pili;
4. Jaribu kutumia rangi zinazosigana mfano rangi nyeupe dhidi ya rangi nyekundu;
5. Unaweza kupamba vazi lako kwa kuchora au kuchapa moja kwa moja; na
6. Andika maandishi yanayosomeka vizuri hata ukiwa mbali.

Kielelezo namba 15 kinaonesha picha ya kubandika iliyomo kwenye vazi la sandarusi.



**Kielelezo namba 15:** *Vazi la sandarusi.*

FOR ONLINE USE ONLY

FOR ONLINE USE ONLY
DO NOT DUPLICATE

**Kazi ya kufanya namba 4**

Kaeni katika vikundi vya wanafunzi watano watano. Tengenezeni maleba kwa kutumia sandarusi. Vazi hilo litumike katika sherehe za maadhimisho ya siku ya kula matunda duniani

Sifa za vazi la sandarusi: Vazi la sandarusi linatakiwa kuwa na sifa zifuatazo:

1. Liwe limepindwa shingoni na mikononi;
2. Liwe na mapambo ya matunda mbalimbali;
3. Liwe safi; na
4. Liwe na alama au mapambo yanayoonekana vizuri.

**Zoezi la pili**

1. Eleza tofauti kati ya motifu na ruwaza.
2. Orodhesha vyanzo vitano vya motifu za asili.
3. Eleza faida za kuwa na ujuzi wa kuchapa ruwaza.

## Kutengeneza Vichezeo

Vichezeo ni vitu, vifaa au zana zinazotumika kuwezesha kucheza mchezo fulani. Vichezeo hivyo ni kama; mpira, drafti, bao, kisahani, tufe na upodo. Vipo vichezeo vya aina nyingi sana. Vingine ni vigumu kuvitengeneza na vingine ni rahisi. Katika sehemu hii utajifunza kutengeneza baadhi ya vichezeo rahisi.

### Nyoka na ngazi

Huu ni mchezo wa jamii ya drafti. Mchezo huu unatumia namba, picha za ngazi, nyoka na dadu. Wakati wa kucheza, kazi ya ngazi ni kumpandisha juu mchezaji. Kazi ya nyoka ni kumshusha chini mchezaji. Kinachopandishwa au

FOR ONLINE USE ONLY

FOR ONLINE USE ONLY
DO NOT DUPLICATE

kushushwa ni dadu. Mchezo huu huburudisha, hufikirisha na kushindanisha. Ujuzi wa kutengeneza kibao cha mchezo wa nyoka na ngazi humpatia mtengenezaji kipato na kukuza kipaji cha ubunifu.

Mahitaji au vifaa: Ubao wa dari wa saizi ya sentimita 30 x sentimita 30, rangi nyeupe ya maji, rula, rangi za mafuta za bluu, nyekundu na kijani, brashi ngumu za bapa na mafuta ya taa.

Hatua za kutengeneza kichezeo: Zifuatazo ni hatua za kutengeneza kichezeo cha nyoka na ngazi:

1. Kata ubao wa dari saizi ya sm. 35 x 45;
2. Paka rangi nyeupe upande wenye unamu kwaruzi. Acha ukingo wa sm 2 kuzunguka ubao wote;
3. Paka tena tabaka la rangi nyeupe baada ya ile ya kwanza kukauka;
4. Subiri hadi ubao ukauke vizuri;
5. Paka rangi nyingine moja tofauti inayovutia katika ubao wote;
6. Subiri rangi hiyo ikauke;
7. Pima miraba ya sm. 1 x 5 upana na sm 1 x 6 urefu;
8. Chora vyumba hivyo na upate jumla ya vyumba 100;
9. Tumia rangi nyeusi kuandika namba 1 hadi 100 na subiri rangi hiyo ikauke;
10. Chora ngazi sita kwa kutumia rangi tofauti;
11. Subiri rangi za ngazi zikauke;
12. Chora picha sita za nyoka, wawili warefu, wawili wafupi na wawili wa kawaida, nao watawanywe kwenye ubao mzima kwa kutumia rangi tofauti;
13. Subiri rangi za nyoka zikauke; na
14. Chagua rangi moja kati ya zile rangi za kwenye safu. Paka rangi hiyo kwenye ule ukingo na kisha subiri rangi hiyo ikauke.


FOR ONLINE USE ONLY



Stadi za Kazi darasa la 6.indd 104 23/07/2021 15:12

FOR ONLINE USE ONLY
DO NOT DUPLICATE

Kielelezo namba 16 kinaonesha kibao cha mchezo wa nyoka na ngazi.



**Kielelezo namba 16:** *Kibao cha mchezo wa nyoka na ngazi*

## Dadu

Kete inayotumika kuchezea mchezo huu huitwa dadu. Dadu ya mchezo huu ina pande 6 zinazolingana. Pande hizo zina vidoti kimoja hadi sita. Dadu inaweza kutengenezwa kwa mpira wa ndala. Pima vizuri kipande cha mpira wa ndala saizi ya sentimita1x1 kila upande kisha kikate. Hakikisha pande zote zinalingana. Dadu hutumbukizwa kwenye kikopo kisha kikopo hutikiswa na dadu kumwagwa mezani. Mchezaji hutumia namba iliyoelekea juu kucheza. Namba katika dadu huwakilishwa na idadi ya vidoti. Kielelezo namba 17 kinaonesha dadu mbili na kopo la kuchezea mchezo wa nyoka na ngazi.





**Kielelezo namba 17:** *Dadu na kopo la kuchezea mchezo wa nyoka na ngazi*

### Kazi za kufanya namba 5

1. Tengeneza kibao cha mchezo wa nyoka na ngazi kwa kutumia karatasi ngumu ya kasha. Tumia rangi za maji au za mafuta. Kichezeo hicho kiwe na saizi ya sm. 20 x sm. 30.

2. Kaeni katika vikundi vya wanafunzi watano kisha tengenezeni dadu ya saizi ya sm. 1 x sm. 1 kwenye vipande vya mpira. Tumieni rangi za mafuta.

FOR ONLINE USE ONLY

FOR ONLINE USE ONLY
DO NOT DUPLICATE

**Sifa za kichezeo cha nyoka na ngazi:** Kichezeo hicho kiwe safi, na kipakwe rangi zinazoonekana vema. Namba na picha ziwe nadhifu na zinazoonekana wazi.

## Drafti

Mchezo wa drafti ni jamii ya mchezo wa bao. Mchezo huu hutumia kete 24 na huchezwa na watu wawili. Ni mchezo unaofikirisha sana na unaopendwa na watu wengi kwani, hutoa burudani kwa wachezaji na watazamaji pia. Hujenga tabia ya ushindani, huhamasisha uwezo wa kufanya uamuzi, na kujenga stadi za hisabati. Unaweza kutengeneza drafti kwa ajili ya kuchezea au kuuza. Katika sehemu hii utajifunza kutengeneza drafti.

## Mahitaji au vifaa

Ubao wa dari saizi ya urefu sentimeta 35 na upana sentimeta 35, rangi nyeupe ya maji, penseli, rula, rangi za mafuta za aina mbili zinazosigana, kete 12 za rangi moja na kete nyingine 12 za rangi tofauti, brashi ngumu za bapa, mafuta ya taa na vikopo vidogo vinne.

**Hatua za kutengeneza drafti:** Zifuatazo ni hatua za kutengeneza drafti:


1. Kata fremu ya ubao wa dari saizi ya sentimeta 35 x 35;
2. Paka rangi nyeupe ya maji ya usuli kwenye upande wa ubao wa dari wenye unamu kwaruzi ili kupata usuli. Subiri rangi ikauke;
3. Paka tena tabaka lingine la rangi nyeupe ya maji kama ile ya kwanza kisha subiri ikauke;
4. Tenga ukanda wenye upana wa sentimeta 3 kuzunguka ubao huo;
5. Pima urefu wa sentimeta 32 na upana wa sentimeta 32. Gawanya vyumba vya upana wa sentimeta 4 na urefu wa sentimeta 4;
6. Chora vyumba 64 vya drafti katikati ya ubao vyenye saizi ya sentimeta 4 x sentimeta 4;
7. Paka rangi aina ya kwanza ndani ya vyumba 32. Paka chumba kimoja na kuruka kinachofuata hadi vitimie 32. Fanya kama ilivyooneshwa katika Kielelezo namba 18;
8. Paka tena rangi ya pili tofauti katika vyumba 32 vilivyobaki;

FOR ONLINE USE ONLY

FOR ONLINE USE ONLY
DO NOT DUPLICATE

9. Andaa kete 24 za rangi mbili tofauti. Kete 12 ziwe za rangi moja na nyingine 12 ziwe za rangi tofauti. Kete zinaweza kuwa vizibo vya chupa za soda, maji, juisi au mafuta, ili mradi vitofautiane rangi; na

10. Tumia mafuta ya taa kusafisha brashi na vikopo ulivyotumia. Kielelezo namba 18 kinaonesha mfano wa drafti.



**Kielelezo namba 18:** *Drafti lililochorwa*

FOR ONLINE USE ONLY

### Kazi ya kufanya namba 6

1. Tengeneza drafti kama ilivyoelekezwa katika hatua za somo hili. Unaweza kutumia karatasi ngumu, ubao wa dari, bati au bapa ya plastiki.
2. Andaa kete za kuchezea drafti hilo.
3. Drafti litakalotengenezwa liwe na:

   (a) Vyumba 64 vya saizi ya sentimeta 3 urefu na sentimeta 3 upana;

   (b) Vyumba 32 vya rangi moja na 32 vya rangi nyingine;

   (c) Ukanda pembeni wa upana wa sentimeta 3;

   (d) Mwonekano safi; na

   (e) Kete 12 za rangi moja na zingine 12 za rangi nyingine.

FOR ONLINE USE ONLY
DO NOT DUPLICATE

## Zoezi la 3

**Chagua herufi ya jibu sahihi na uiandike kwenye daftari lako la mazoezi.**

1. Uandaaji wa makunzi unatokana na vyanzo vingi isipokuwa...........
   a) vitambaa
   b) ngozi au turubai
   c) mchanga
   d) ngoma

2. Kutunga picha ni kuibua wazo la picha na kuliwasilisha katika ...........
   a) taswira ya kuonekana
   b) fremu ya picha
   c) ukubwa wa picha
   d) umbo la picha

3. Mojawapo kati ya mambo ambayo msanii anapaswa kuzingatia anaposanii picha za kubandika ni.......
   a) maumbo yawe na vijisehemu vidogovidogo
   b) maumbo ya picha yawe sahihi
   c) makunzi yawe ya kioo
   d) makunzi yawe yenye kupauka rangi na kusinyaa

4. .................. ni kurekebisha maeneo mbalimbali ya picha kwa kusawazisha na kuihifadhi.
   a) Kusanifu picha
   b) Kukamilisha picha
   c) Kubandika picha
   d) Kupamba picha

FOR ONLINE USE ONLY

FOR ONLINE USE ONLY
DO NOT DUPLICATE

5. Uchongaji wa motifu unahitaji kuzingatia sifa zifuatazo isipokuwa ..............
   a) usafi wa uchongaji
   b) usahihi wa umbo
   c) ukali wa vichongeo
   d) umbo liwe na vijisehemu vidogovidogo

**B. Jibu maswali yafuatayo.**

1. Kwa nini tunatumia sehemu ya juu ya jani kuchapia?
2. Umeona nini kutokana na mwingiliano wa maumbo katika kuchapa majani?
3. Pambo lina matuminzi gani?

## Msamiati

| | |
|---|---|
| **Dadu** | Kete zinazotumika kuchezea drafti au dhumna |
| **Maleba** | Mavazi maalumu yanayovaliwa na wasanii wanapokuwa wanafanya maonesho |
| **Motifu** | Ni alama ya msingi inayotumika katika uchapaji |
| **Nakshi** | Urembo utokanao na matokeo ya kuchora, kutarizi au kuchonga |
| **Ruwaza** | Mpangilio wa motifu zinazojirudiarudia |

FOR ONLINE USE ONLY

FOR ONLINE USE ONLY
DO NOT DUPLICATE

# Sura ya Saba

## Ufinyanzi, ususi na vifani

### Utangulizi

*Ulipokuwa Darasa la Tano ulijifunza kuhusu ufinyanzi na ususi. Katika sura hii utajifunza kutengeneza vitu kwa kutumia makunzi ya aina mbalimbali yanayopatikana katika mazingira unayoishi. Makunzi hayo ni kama vile karatasi, plastiki, nyaya, sandarusi, mpira, ukindu na vitu vingine. Utatengeneza vitu mbalimbali vya kufinyanga kwa kutumia kinyunya cha karatasi; kuunda umbo pambo; kutengeneza vifani na kushona ukili uliosukwa. Ujuzi wa kutengeneza vifani utakuwezesha kujitegemea kwa kujitengenezea vifaa na pia kuuza na kupata fedha.*

### Kufinyanga vitu kwa kinyunya cha karatasi

Ufinyanzi ni sanaa ya kuunda maumbo mbalimbali kwa kutumia makunzi yanayoweza kufinyangwa. Makunzi yanayofinyangwa ni kama vile udongo wa mfinyanzi, plastiki, nta na kinyunya cha karatasi. Katika sura hii utajifunza kufinyanga kwa kinyunya cha karatasi. Kinyunya cha karatasi ni uji au tope linalotokana na karatasi zilizolowekwa na kutwangwa hadi zikalainika mithili ya tope. Tope hilo huchanganywa na gundi au uji wa muhogo ili liweze kushikamana vizuri. Mchanganyiko huu unaweza kutumika kufinyangia vitu mbalimbali.

### Kuandaa kinyunya cha karatasi

Mahitaji ya kuandaa kinyunya cha karatasi ni: Maji, kinu, mchi, karatasi safi zilizotumika, vijiti vyenye urefu na unene mkubwa wa kalamu na chupa za plastiki. Vingine ni gundi ya mbao, unga wa muhogo, sufuria, jiko, msumari, rangi, brashi, kikorogeo na ndoo ndogo.

FOR ONLINE USE ONLY



Stadi za Kazi darasa la 6.indd 110 23/07/2021 15:12

FOR ONLINE USE ONLY
DO NOT DUPLICATE

**Hatua**

Zifuatazo ni hatua za kutengeneza kinyunya cha karatasi:

1. Kusanya karatasi safi laini;
2. Loweka karatasi hizo kwenye maji kwa siku moja hadi mbili;
3. Ondoa karatasi kwenye maji kisha twanga kwenye kinu;
4. Twanga hadi karatasi zilainike kabisa;
5. Ongeza maji kidogo ili upate uji wa karatasi. Pakua uji wa karatasi na kuuweka kwenye ndoo; na
6. Changanya uji wa karatasi na gundi hasa ya mbao au uji wa unga wa muhogo. Sasa kinyunya cha karatasi ni tayari kwa kuunda umbo.

Baada ya kuandaa kinyunya hatua inayofuata ni ya kubuni na kuunda umbo.

***Uundaji wa kifani cha papai kwa kutumia kinyunya cha karatasi***

Ili kuunda kifani cha papai kwa kinyunya cha karatasi fuata hatua zifuatazo:

1. Fikiria umbo la papai;
2. Unda kiunzi kwa kutumia chupa ya plastiki ya ujazo wa lita moja hivi;
3. Toboa matundu kwa msumari kuzunguka chupa;
4. Pachika vijiti kwenye chupa hadi vijitokeze upande wa pili;
5. Kandika kiunzi kwa tope la karatasi hadi liwe na umbo la papai;
6. Lainisha uso wa umbo kwa kitu chenye ncha bapa kama mfupa bapa au kijiko;
7. Anika umbo kivulini na subiri likauke;
8. Bandika vipande vya tabaka la karatasi lifanane na umbo la papai;
9. Paka rangi kulingana na papai linalohitajika mfano wa papai bichi au lililoiva; na
10. Weka alama muhimu kama zipo.

FOR ONLINE USE ONLY

FOR ONLINE USE ONLY
DO NOT DUPLICATE

Umbo hilo la papai linaweza kutumika kama pambo kwenye meza ya chakula, pia kuwa kielelezo au zana ya kufundishia na kujifunzia. Aidha, linaweza pia kuwa bidhaa itakayouzwa na kuleta kipato.

### Kazi za kufanya namba 1

1. Tengeneza kifani cha papai kwa kutumia kinyunya cha karatasi. Sifa za kifani hicho ziwe kama ifuatavyo:

   (a) kiwe na saizi ya papai;

   (b) kifanane na papai;

   (c) kiwe kimekauka vizuri;

   (d) kiwe safi; na

   (e) kiwe na nakshi.

2 Tengeneza kifani cha kitu kingine utakachochagua mwenyewe. Kifani hicho kifanane na kitu halisi na kiwe na sifa zifuatazo:

   (a) saizi inaweza kuwa ndogo au kubwa zaidi ya kitu halisi;

   (b) kifani kiwe kimekaushwa vizuri;

   (c) kiwe na nakshi; na

   (d) kiwe safi.

FOR ONLINE USE ONLY

### Zoezi la kwanza

1. Eleza maana ya kifani
2. Taja kazi ya kiunzi katika ufinyanzi wa maumbo
3. Fafanua neno nakshi na toa sababu za kutia nakshi.

FOR ONLINE USE ONLY
DO NOT DUPLICATE

## Pambo la kuunda

Tofauti na mapambo ya kuchapa, yapo mapambo ya kuunda. Mapambo ya kuunda yanarahisishwa kwa kuanza na maumbo la msingi. Katika sehemu hii utajifunza kuunda pambo la duara la kuning'iniza ambalo linaweza kuning'inizwa sebuleni, ofisini, darasani na sehemu zingine na kuwa kivutio.

Mahitaji au vifaa: Andaa puto, uzi mwembamba wa manila, mkasi, karatasi laini zinazong'ara za rangi anuwai, gundi, riboni za kumeremeta na shedo.

## Hatua za kuunda pambo

Zifuatazo ni hatua za kuunda pambo:

1. Puliza puto hewa hadi lijae kabisa kisha lizibe;
2. Funga uzi mrefu wa manila kwenye shingo ya puto;
3. Katakata vipande vya karatasi laini za rangi zinazong'ara;
4. Chukua karatasi laini nyeupe za kawaida uzibandike kwa gundi kufunika puto;
5. Bandika vipande vya karatasi laini za rangi za kung'aa kufunika tabaka la karatasi nyeupe;
6. Bandika riboni za kumeremeta hapa na pale kuzunguka umbo;
7. Paka gundi hapa na pale kuzunguka umbo kwa ajili ya kubandika shedo;
8. Nyunyizia shedo kwenye uso wa pambo ulikopaka gundi; na
9. Ning'iniza pambo kwa kutumia uzi mwembamba wa manila uliotunga pale awali.

FOR ONLINE USE ONLY

FOR ONLINE USE ONLY
DO NOT DUPLICATE

Kielelezo namba 1 kinaonesha puto lililopuliziwa na kuning'inizwa



**Kielelezo namba 1:** *Pambo la kuning'iniza*

**Kazi ya kufanya namba 2**

Fanya kazi ifuatayo katika kikundi cha wanafunzi wasiozidi watano.

1. Unda pambo lolote kwa kufuata hatua ulizojifunza, anza na umbo la msingi linalopatikana kwenye mazingira yako. Kwa mfano tumia chupa ya plastiki ya maji ya ujazo wa lita moja.

## Kuunda mwanasesere

Mwanasesere ni umbo linalowakilisha umbo la binadamu. Umbo hilo linaweza kutengenezwa kwa kutumia makunzi mbalimbali. Katika sehemu hii utajifunza jinsi ya kuunda mwanasesere.

Mahitaji au vifaa

Vitambaa, nyaya, vijiti saizi ya penseli, rangi, brashi, galoni la plastiki, gundi, karatasi, kamba na kisu

**Hatua za kuunda mwanasesere**

Uundaji wa mwanasesere hufuata hatua zifuatazo:

1. Buni umbo la mwanasesere unalotarajia kuunda;
2. Chukua chupa au galoni yenye saizi sawa na mwanasesere unayetarajia kumuunda;

FOR ONLINE USE ONLY

FOR ONLINE USE ONLY
DO NOT DUPLICATE

3. Toboa matundu sehemu ya chini ya galoni au chupa. Chukua vijiti vyenye urefu sawa kisha vichomeke chini ya galoni au chupa. Hiyo ni miguu ya mwanasesere;
4. Kunja nyaya mithili ya mikono au kata vijiti linganifu kisha chomeka sehemu ya juu ya galoni au chupa. Hiyo ni mikono ya mwanasesere;
5. Endapo utatumia nyaya unaweza kuzikunja kadri upendavyo mithili ya miguu au mikono ya mwanasesere;
6. Tumia vitambaa au karatasi na gundi kufunika sehemu zote za kifani; na
7. Paka rangi inayohusika, sasa kifani cha mwanasesere ni tayari.

### Kazi za kufanya namba 3

Fanya kazi zifuatazo katika vikundi:

1. Tengeneza mwanasesere kwa kutumia chupa ya plastiki ya maji ya saizi ya lita moja.
2. Tumia vijiti na nyaya kuunda mikono na miguu ya mwanasesere.
3. Funika nyaya na vijiti hivyo kwa mizungusho ya karatasi au vitambaa.

### Zoezi la pili

Jibu maswali haya kwa kuandika

1. Nini maana ya umbo la msingi?
2. Kwa nini tunaunda maumbo kwa kuanza na umbo la msingi?
3. Je, tunaweza kutumia umbo gani lingine la msingi badala ya chupa ya plastiki.?
4. Kwa namna gani sanaa inaweza kuchangia kuboresha mazingira?

FOR ONLINE USE ONLY



Stadi za Kazi darasa la 6.indd 115 23/07/2021 15:12

FOR ONLINE USE ONLY
DO NOT DUPLICATE

## Vifani vya samaki na mbwa

Kifani ni umbo linalotengenezwa na kufanana na umbo halisi japo saizi zinaweza kutofautiana. Vifani vina matumizi mengi kama vile mapambo na vielelezo vya kufundishia, pia vinaweza kuwa vifaa vya michezo na sanamu za kuamia ndege na wanyama waharibifu wa mazao mashambani. Katika kipengele hiki utajifunza kutengeneza vifani vya samaki na mbwa kwa kutumia karatasi na plastiki.

### Mahitaji ya kutengeneza kifani cha samaki


Yafuatayo ni mahitaji ya kutengeneza kifani cha samaki:

Karatasi kama vile za kalenda, magazeti au manila, mkasi, gundi, uzi mwembamba wa manila, maumbo ya mche duara ya karatasi ngumu au ya chupa za plastiki.

### Hatua za kutengeneza kifani cha samaki

Zifuatazo ni hatua za kutengeneza kifani cha samaki:

1. Chunguza maumbo mbalimbali ya samaki katika picha zilizomo katika matini tofauti au mazingira unayoishi;
2. Chagua samaki mwenye umbo rahisi kutengenezwa;
3. Kunja karatasi ya kalenda upate pande mbili;
4. Chora umbo la samaki kwenye upande mmoja wa karatasi ya kalenda uliyokunja. Hakikisha sehemu iliyo na maandishi inakuwa upande wa ndani kama inavyoonekana katika Kielelezo namba 2.



**Kielelezo namba 2:** *Mchoro wa samaki kwenye karatasi iliyokunjwa*

FOR ONLINE USE ONLY

FOR ONLINE USE ONLY
DO NOT DUPLICATE

5. Kata umbo la samaki ulilochora, vitoke vipande viwili vinavyolingana na kufanana;

6. Paka gundi pembezoni mwa pande hizo. Kumbuka kuacha sehemu itakayotumika kujazia karatasi na itakayokuwa mdomo;

7. Unganisha vipande hivyo vya karatasi na subiri gundi ikauke na kushika vizuri;


8. Andaa jicho la samaki kisha ulibandike katika eneo lake sahihi kichwani;

9. Jaza vipande vya karatasi au vitambaa ndani ya mfuko wa umbo la samaki, shindilia hadi mfuko utune;

10. Ziba ile sehemu uliyoingizia vipande vya karatasi au vitambaa; na

11. Tunga uzi katikati kwenye mapezi ya juu kisha ning'iniza kifani hicho.

Kielelezo namba 3. kinaonesha kifani cha samaki kilichoning'inizwa.



**Kielelezo namba 3:** *Kifani cha samaki kinachoning'inia*

**Kazi za kufanya namba 4**

Tengeneza kifani cha samaki kwa kutumia karatasi, kwa kuzingatia maelekezo na vipimo vifuatavyo:

1. Urefu wa sentimeta 30

2. Upana wa sentimeta 20

3. Kiwe na uzi wa kuning'inizia

4. Kiwe kimejazwa vipande vya karatasi zitakazokidhi kutuna vizuri

FOR ONLINE USE ONLY

FOR ONLINE USE ONLY
DO NOT DUPLICATE

**Zoezi la 3**


Andika insha fupi kuhusu faida za kuwa na ujuzi wa kutengeneza maumbo kwa kutumia karatasi.

### Mahitaji ya kutengeneza kifani cha mbwa

Mahitaji ya kutengeneza kifani cha mbwa ni: Karatasi kama vile za kalenda, magazeti na manila, mkasi, gundi, uzi mwembamba wa manila, maumbo ya mche duara ya karatasi ngumu au ya chupa za plastiki, rangi na kalamu za rangi.


### Hatua za kutengeneza kifani cha mbwa

1. Kunja karatasi ngumu katikati upate vipande viwili. Urefu wa kipande cha karatasi kilichokunjwa uwe sentimeta 10 kutoka chini. Fuatilia hatua zote zilizomo katika Kielelezo namba 4 hadi namba 9



**Kielelezo namba 4:** *Karatasi ngumu iliyokunjwa katikati*


2. Chora eneo la kichwa hadi mabega ya mbwa katika karatasi uliyokunja kisha kata kufuata mchoro huo



**Kielelezo namba 5:** *Sehemu ya mbele ya kifani cha mbwa*


FOR ONLINE USE ONLY

FOR ONLINE USE ONLY
DO NOT DUPLICATE



**Kielelezo namba 6:** *Karatasi ngumu iliyokunjwa katikati*


3. Kunja tena karatasi nyingine na chora sehemu ya nyuma ya mbwa. Sasa kata kufuata mchoro wa sehemu ya nyuma ya mbwa.



**Kielelezo namba 7:** *Sehemu ya nyuma ya kifani cha mbwa*

4. Kunja karatasi gumu upate umbo la mcheduara. Umbo hilo liwe na urefu wa sentimeta 12 na kipenyo cha sentimeta 2½. Unganisha sehemu ya mbele na ya nyuma ya mbwa kwa mcheduara huo.

Umbo la mcheduara la kifani cha eneo la tumbo la mbwa



**Kielelezo namba 8:** *Sehemu za kifani cha mbwa kabla ya kuunganishwa*

FOR ONLINE USE ONLY


FOR ONLINE USE ONLY
DO NOT DUPLICATE

5. Paka gundi kwa ndani sehemu ya mbele ya mbwa, ibandike kwenye ncha ya kwanza ya mcheduara.

6. Paka gundi kwa ndani sehemu ya nyuma ya mbwa, ibandike kwenye ncha ya pili ya mcheduara.

7. Chora alama muhimu kama vile macho, pua, masikio na mdomo kwa kalamu ya rangi.

8. Tia nakshi kama vile mabaka au paka rangi moja.



**Kielelezo namba 9:** *Umbo kamili la mbwa*

**Kazi za kufanya namba 5**

1. Katika kikundi tengeneza kifani cha mbwa kwa kufuata hatua kama zilivyoainishwa hapo juu. Tumia makunzi yanayopatikana katika mazingira yako.

2. Buni kiumbe kingine cha chaguo lako kisha utengeneze kifani chake kwa kuzingatia hatua ulizojifunza.

Kazi hizo zizingatie sifa zifuatazo

i) Zifanane au ziakisi kile ulichodhamiria.

ii) Zilingane kushoto na kulia, mbele na nyuma.

iii) Ziwe na nakshi nzuri.

iv) Ziwe safi.

FOR ONLINE USE ONLY



Stadi za Kazi darasa la 6.indd 120 23/07/2021 15:12

FOR ONLINE USE ONLY
DO NOT DUPLICATE

## Kushona kifani cha kili na kukinakshi

Katika ususi kuna hatua mbili. Hatua ya kwanza ni ile ya kusuka ukanda wa ukindu unaoitwa ukili. Hatua ya pili ni kushona ukili ili kupata umbo la kifani unachotaka. Maumbo yanayoweza kujitokeza kutokana na kushona ukili ni kama vile kawa, kikapu, kofia, kipepeo na mkeka. Katika sehemu hii utajifunza kushona kifani cha mkeka na kukinakshi.


### Mahitaji ya kushona kifani cha kili na kukinakshi

Kifani cha kili na kukinakshi hushonwa kwa kutumia: Ukili mfuto na ukili wenye rangi, kibao cha kushonea mkeka, kisu, pini, shazia na uzi imara mwembamba.


### Hatua

Zifuatazo ni hatua za kushona kifani cha kili na kukinakshi

1. Andaa kibao chenye urefu wa sm. 30 na upana wa sm. 15. Kibao hiki kitatumika kuzungushiwa ukili ili kuunda mkeka;
2. Tunga uzi katika sindano;
3. Chukua ukili mfuto, zenye urefu wa futi 6 kila mmoja. Shona kuunganisha kili hizo kwa urefu wake wote;
4. Laza jozi hizo katika ubao na kisha zungusha mzungusho wa kwanza. Shikiza kili kwa kushona na uzi na shazia pale ambapo kili zitakutana kwa mara ya kwanza. Shona kuunganisha ncha hizo mbili kuzunguka kibao
5. Zungusha tena na tena kanda za kili kuzunguka kibao huku ukizishona barabara kama inavyoonekana katika kielelezo katika namba 10.



Ukili



Ukili uliozungushwa kwenye ubao

**Kielelezo namba 10:** *Maandalizi ya kushona kifani cha kili*

FOR ONLINE USE ONLY

FOR ONLINE USE ONLY
DO NOT DUPLICATE

6. Mizungusho ya kili ikutanishwe vizuri ili ushonaji wake ushikamane sawasawa. Shona kwa kupitisha shazia katika macho ya ukili wa kwanza. Choma tena katika ukili wa pili, vuta na kaza vizuri. Hakikisha kili zote zinakutana kwa ulinganifu. Hakikisha unavuta uzi wa kushonea kwa usahihi ili kukaza mshono vizuri;
7. Shona kwa kupitisha shazia katika macho mawilimawili au matatumatatu ya ukili na kukaza vizuri. Hatua hii ikifanywa vizuri ndipo utapatikana mkeka imara;
8. Endelea kushona hivyohivyo kwa kuzunguka ubao hadi mwisho wa ukanda wa ukili. Hapa utakuwa na umbo la mkeka mithili ya mche duara mpana;
9. Kata kwa kisu upande mmoja wa mcheduara huo. Hapo utapata mkeka wenye kingo mbili zenye ncha zilizofumuka. Sehemu hizi ni zile ambazo zilikatwa kwa kisu;
10. Pima urefu wa kingo mbili zilizokatwa kwa kisu. Tumia kipimo hicho kupima na kukata ukili utakaofanya pindo katika kingo hizo; na
11. Kunja kanda hizo za ukili katikati kwa marefu na shonea kanda za ukili zilizokunjwa katika kingo za mkeka. Pindo hili huzuia ncha za mkeka zisifumuke. Kifani cha mkeka ni tayari.

Kifani cha mkeka ni tayari kama inavyoonekana katika Kielelezo namba 11



**Kielelezo namba 11:** *Mkeka uliopindwa*



Stadi za Kazi darasa la 6.indd 122 23/07/2021 15:12

FOR ONLINE USE ONLY

FOR ONLINE USE ONLY
DO NOT DUPLICATE

**Kazi ya kufanya namba 8**

Shona kifani cha mkeka chenye nakshi na chenye urefu wa sm. 30 na upana wa sm. 18.

**Zoezi la 4**

**A. Chagua neno sahihi kutoka kwenye sanduku na ujaze sehemu iliyo wazi.**

| Ususi, mbili, ukili, uji, mapambo, makunzi |
|---|

1. Ufinyanzi ni sanaa ya kuunda maumbo mbalimbali kwa kutumia ........... yanayoweza kufinyangwa.
2. .................... ya kuunda yanarahisishwa kwa kuanza na maumbo msingi.
3. Kuna hatua ................. wakati wa ususi wa mkeka.
4. Ukanda wa ukindu unaitwa ..........................
5. Kinyunya cha karatasi ni ................. unaotokana na karatasi zilizolowekwa na kutwangwa hadi zikalainika.

**B. Fanya kazi ifuatayo:**

6.Andika insha fupi inayohusu "Jinsi ya kushona kifani cha mkeka."

## Msamiati

**Shazia** Sindano kubwa inayotumiwa kushonea vitu vigumu kama gunia, mkeka au tanga

FOR ONLINE USE ONLY

FOR ONLINE USE ONLY
DO NOT DUPLICATE

# Sura ya Nane

## Stadi za ujasiriamali

### Utangulizi

*Ulipokuwa Darasa la Tano ulijifunza umuhimu wa kutumia stadi za ujasiriamali kuendesha mradi au miradi kwa namna itakayokupatia kipato chenye faida. Katika sura hii utajifunza kujitafutia maarifa na ujuzi wa namna mpya ya kutenda mambo ya kijasiriamali, kushiriki katika midahalo na kufanya udadisi. Pia utajifunza kubaini aina za wateja kulingana na bidhaa unazozalisha, kutambua njia bora za ufungashaji wa bidhaa mbalimbali pamoja na vifaa halali vinavyotumika kupimia bidhaa. Vilevile, utajifunza kubaini udanganyifu wa namna mbalimbali unaoweza kufanywa na watu ambao unashirikiana nao katika ujasiriamali. Kujifunza stadi za ujasiriamali kutakuwezesha kubaini na kutumia fursa zenye mianya chanya ya biashara. Hii itakusaidia kupata kipato chenye faida.*

### Kujenga utayari wa kujifunza

Kila mtu anaweza kuwa mjasiriamali kupitia njia mbalimbali endapo atakuwa na nia ya dhati. Kufanya ujasiriamali ni moja kati ya njia za kujipatia kipato kwa mtu mmoja mmoja, kikundi na jamii kwa ujumla. Ili mjasiriamali apate faida katika shughuli zake, anatakiwa awe na maarifa stahiki juu ya uendeshaji wa shughuli hizo. Hivyo ni muhimu mjasiriamali ajijengee utayari wa kujifunza. Miongoni mwa mambo ya msingi mjasiriamali anayotakiwa kujifunza ni namna ya kujijengea uwezo wa kutambua fursa zenye mianya chanya ya kuanzisha na kuendeleza miradi katika jamii. Vilevile, anatakiwa awe na uthubutu wa kutumia fursa hizo kuendesha miradi na kukabiliana na changamoto zinazojitokeza. Kwa kuwa jamii huwa na mabadiliko kila wakati, ni wazi kwamba mjasiriamali anayetaka mafanikio hana budi kujijengea utayari wa kujifunza wakati wote. Zipo njia anuai ambazo mjasiriamali anaweza kuzitumia kujitafutia ujuzi na maarifa

FOR ONLINE USE ONLY



Stadi za Kazi darasa la 6.indd 124 23/07/2021 15:12

FOR ONLINE USE ONLY
DO NOT DUPLICATE

yatakayomwezesha kuendesha shughuli zake kwa tija. Miongoni mwa njia hizo ni ushiriki wa mjasiriamali kwenye midahalo pamoja na kufanya udadisi kuhusu uendeshaji wa shughuli za kijasiriamali.

### Kujitafutia maarifa na ujuzi kupitia ushiriki katika midahalo



Jadiliana katika kikundi na wenzako

1. Mdahalo ni nini?
2. Je,ulishawahi kushiriki katika mdahalo au midahalo yoyote? Ulijifunza nini katika mdahalo au midahalo uliyoshiriki?

Mdahalo ni mbinu ya mawasiliano iliyo rasmi ambapo mada moja hutazamwa kwa namna tofauti na washiriki. Kila upande hujenga hoja zinazopendelea upande wake na hatimaye mwafaka hufikiwa. Katika midahalo ya kijasiriamali, mada za kijasiriamali hutazamwa kwa namna tofauti na washiriki. Hivyo ni muhimu mjasiriamali kushiriki katika midahalo ya kijasiriamali ili aweze kujifunza mambo mbalimbali.

***Umuhimu wa midahalo ya kijasiriamali:*** Ushiriki wa mjasiriamali katika midahalo humwezesha:

1. Kujenga uwezo wa kufikiri kiyakinifu;
2. Kujenga uwezo wa kuchambua hoja;
3. Kujenga mwelekeo wa kushirikiana;
4. Kujenga uwezo kwa kuzungumza hadharani;
5. Kuibua uwezo wa kufanya utafiti;
6. Kujenga uwezo mzuri wa kuuliza na kujibu maswali; na
7. Kujenga tabia ya kupenda kujiendeleza kwa kujifunza maishani.

Ni dhahiri kwamba kila mjasiriamali anahitaji kujijengea maarifa haya ili aweze kuendesha shughuli zake kwa tija.

FOR ONLINE USE ONLY

FOR ONLINE USE ONLY
DO NOT DUPLICATE

**Kazi ya kufanya namba 1**

1. Andaa makundi mawili ya mdahalo. Kundi moja lijenge hoja kwamba ujasiriamali ni jambo la kujifunza na si suala la kuzaliwa nalo. Kundi la pili lipinge hoja hiyo.
2. Andaa na kushiriki midahalo mingine kwa kuongozwa na mwalimu.

**Zoezi la kwanza**

Andika muhtasari wa mambo uliyojifunza katika kila mdahalo.

FOR ONLINE USE ONLY

### Kujitafutia maarifa na ujuzi kupitia udadisi

Udadisi ni miongoni mwa namna za kujipatia maarifa na ujuzi kuhusu ujasiriamali. Mambo ya msingi ambayo mjasiriamali anatakiwa kudadisi ni namna ya kutambua na kutumia fursa zenye mianya chanya ya biashara. Kwa kuwa jamii ina mabadiliko kila wakati, ni wazi kwamba fursa na mahitaji hubadilika pia. Hivyo, mjasiriamali anayetaka mafanikio hana budi kuwa mdadisi wakati wote. Umuhimu wa mjasiriamali kuwa mdadisi ni kujenga uwezo wa kuwa mbunifu. Udadisi unaweza kufanywa kwa namna mbalimbali ikiwemo kuhoji ana kwa ana na kusoma machapisho mbalimbali.

### Soma kisamafunzo kifuatacho kwa makini

Pendo na Baraka ni watoto mapacha wanaosoma Darasa la Sita katika shule ya Msingi Mashujaa. Wakati wa likizo Pendo na Baraka walikwenda kumsalimia shangazi yao anayeishi kijiji cha Makuyuni. Pendo na Baraka walipenda kila wakati kuambatana na shangazi yao katika shughuli zake. Shangazi yao ni mjasiriamali anayemiliki biashara ya duka. Siku moja wakati Pendo na Baraka wamekaa na shangazi yao katika eneo lake la biashara, walipata fursa ya kudadisi masuala ya ujasiriamali. Mazungumzo yao yalikuwa kama ifuatavyo:



Stadi za Kazi darasa la 6.indd 126 23/07/2021 15:12

FOR ONLINE USE ONLY
DO NOT DUPLICATE

**Pendo:** Shangazi, na mimi naweza kuwa mjasiriamali kama wewe?

**Baraka:** Pendo, kama vile ulikuwa akilini mwangu! Nami pia nilitaka kumuuliza shangazi swali hilohilo.

**Shangazi**: Ndiyo, kila mtu anaweza kuwa mjasiriamali.

**Baraka:** Mimi ninataka niwe mjasiriamali mwenye kuuza bidhaa kama hizi za dukani kwako kwa sababu zinahitajika na wateja wengi.

**Pendo:** Mimi pia nataka niwe mjasiriamali mwenye kumiliki duka kubwa na niuze bidhaa nyingi kama unazouza kwani unapata fedha nyingi.

**Shangazi**: Mna mawazo mazuri. Sikilizeni wanangu, ili muweze kufikia ndoto zenu mnahitajika kujifunza mambo ya msingi kuhusu ujasiriamali.

**Baraka:** Kwani tunahitajika kujifunza nini tena? Maana muda tuliokaa na wewe, tayari tumejifunza kuuza bidhaa za dukani. Tena juzi ulitusifia kuwa tumefanya kazi vizuri.

**Shangazi:** Ni kweli mlifanya kazi vizuri ila kuwa mjasiriamali na kuendesha biashara si jambo la kuiga tu, ni vema kujifunza mambo ya msingi katika biashara.

**Pendo:** Kwa hiyo shangazi tunatakiwa kujifunza nini?

**Shangazi:** Yapo mambo mengi. Je, mkimaliza shule mwakani mnategemea kufungua biashara zenu wapi?

**Pendo:** Nitafungua kijijini kwetu, tena mtaani kwetu.

**Baraka:** Na mimi pia nitakapomaliza shule nitafanyia kijijini kwetu. Ila nitafanyia katika mtaa wa Mtakuja mbali kidogo na nyumbani kwani huko hakuna duka lolote. Ni matumaini yangu nitapata wateja wengi.

FOR ONLINE USE ONLY

FOR ONLINE USE ONLY
DO NOT DUPLICATE



**Kielelezo namba 1:** *Duka la shangazi*

**Shangazi:** Vema! Ili mfanye biashara vizuri mnatakiwa kutambua mahitaji ya watu wa pale mnapohitaji kufanyia shughuli. Pia biashara mtakazozifanya ziwe na ubora unaohitajika na wateja wenu.

**Pendo:** Mbona ulisema yapo mengi ya kujifunza? Hakuna jambo jingine?

**Shangazi:** Si hilo tu, mnatakiwa pia kujua uwezo na kipato cha wateja watakaonunua bidhaa zenu au huduma mtakazotoa.

**Pendo:** Shangazi umesema kutoa huduma! Je, ni huduma gani hiyo shangazi?

**Shangazi:** Huduma zinazoweza kutolewa kibiashara ziko nyingi kutegemea mahitaji na uwezo wa wateja wa mahali panapohusika. Huduma kama vile udobi, ususi, upambaji, burudani na nyinginezo nyingi zaweza kutolewa kibiashara.

**Pendo:** Kumbe shangazi! Shuleni tumejifunza ususi, udobi, ushonaji, upambaji na mapishi ya vyakula mbalimbali katika somo la Stadi za Kazi. Sikujua kama hivyo vyote naweza kuvifanya kibiashara na vikanipatia kipato chenye faida.

FOR ONLINE USE ONLY

FOR ONLINE USE ONLY
DO NOT DUPLICATE

**Baraka:** Mimi nimejifunza na ninapenda sana uimbaji na uigizaji tuliojifunza kwenye somo la Stadi za Kazi. Halafu mwalimu aliniambia ninafanya vizuri. Kumbe nayo ni fursa ya biashara! Nitawashawishi wanafunzi wenzangu wanaopenda kuimba na kuigiza tuanzishe kikundi ambacho tutakuwa tunatoa burudani pale kijijini. Ninaamini hadi tutakapomaliza shule, tutakuwa na uwezo wa kwenda kufanya maonesho ya sanaa maeneo mengine pia.

**Shangazi:** Jambo jema Baraka. Tena umenikumbusha jambo muhimu ambalo sijawaambia. Ni vema kujichunguza mwenyewe ili kutambua uwezo na udhaifu wako katika kufanya biashara utakayoichagua. Kwa sasa endeleeni na shule ili mkuze vipaji vyenu. Mkimaliza shule mtafanya ujasiriamali kwa ufanisi.

**Pendo:** Shangazi umesema kujichunguza uwezo na udhaifu. Una maana gani?

**Shangazi:** Ninamaanisha kuwa, ujichunguze uwezo wako katika kuendesha shughuli za ujasiriamali, mfano, kuwa na utaalamu wa ujasiriamali pamoja na vitendea kazi vya kutosha. Pia, nina maana ya kuwa, ujichunguze udhaifu wako katika kuendesha biashara mfano: ukosefu wa utaalamu na mtaji wa kutosha pamoja na kuwa na dhana zisizo sahihi kuhusu ujasiriamali.

**Baraka:** Je, dhana zisizo sahihi kuhusu ujasiriamali ni zipi shangazi?

**Shangazi:** Zipo nyingi, mfano, dhana ya kwamba ujasiriamali ni kujihusisha na biashara ndogondogo tu, ujasiriamali unafaa kufanywa na watu wasio na elimu, ujasiriamali unazaliwa nao, ujasiriamali ni kamari au bahati nasibu, na ujasiriamali unahitaji mtaji mkubwa tu wa biashara.

**Pendo:** Asante sana shangazi! Nimejifunza mengi kutoka kwako juu ya ujasiriamali.

**Baraka:** Asante sana shangazi! Nimejifunza kwa vitendo namna ya kuendesha shughuli za ujasiriamali.

FOR ONLINE USE ONLY



Stadi za Kazi darasa la 6.indd 129 23/07/2021 15:12

FOR ONLINE USE ONLY
DO NOT DUPLICATE

**Shangazi:** Nimefurahi kuwa na ninyi. Ninaamini likizo ijayo mtanitembelea tena. Kumbukeni, yapo mambo mengi ya kujifunza ili muwe wajasiriamali wenye tija hivyo jengeni utayari wa kujifunza. Utayari huo utawasaidia sana kufikia malengo yenu.

## Zoezi la pili

**Jibu maswali yafuatayo**

1. Kisamafunzo ulichosoma kinahusu nini?
2. Shangazi yao Pendo na Baraka alikuwa anafanya shughuli gani?
3. Je, ni jambo gani muhimu ambalo Pendo na Baraka walitakiwa wawe nalo ili kufikia lengo lao la kuwa wajasiriamali?
4. Ni mambo gani matatu ya msingi ya kufanya kabla ya kuanzisha biashara ambayo Pendo na Baraka walidadisi kutoka kwa shangazi yao?
5. Pendo alibaini mambo gani aliyojifunza katika somo la Stadi za Kazi anayoweza kuyatumia kama fursa ya biashara?
6. Baraka aliazimia kuanzisha biashara gani kutokana na stadi alizojifunza katika somo la Stadi za Kazi? Kwa nini alichagua stadi hizo?
7. Ni uwezo gani ambao mjasiriamali anatakiwa kuwa nao ili aweze kufanikiwa?
8. Unafikiri ni mambo gani ambayo yanaweza kuzorotesha biashara au shughuli za mjasiriamali?
9. Ni dhana zipi zisizosahihi kuhusu ujasiriamali? Taja dhana nne.
10. Je, unadhani mawazo ya Baraka ya kuanzisha biashara ya sanaa za maonesho na Pendo biashara ya duka watakapomaliza Darasa la Saba ni sahihi? Kwa nini?

FOR ONLINE USE ONLY



Stadi za Kazi darasa la 6.indd 130 23/07/2021 15:12

FOR ONLINE USE ONLY
DO NOT DUPLICATE

**Kazi za kufanya namba 2**

1. Kwa kutumia stadi ulizojifunza, dadisi endapo sehemu unayoishi kuna fursa za ujasiriamali zinazoweza kutekelezeka. Mfano, upishi, utunzaji wa nyasi, maua, na mboga pamoja na sanaa za uigizaji, uimbaji, ufinyanzi, ususi au usanifu wa picha.
2. Andaa taarifa ya udadisi uliofanya na kuiwasilisha darasani.

## Wateja wa bidhaa au huduma



Fikiri

1. Wateja wa bidhaa au huduma zinazotolewa na wafanya biashara ni akina nani?
2. Je, wateja hao wanapatikanaje?

Mteja ni mtu anayekwenda kununua bidhaa au huduma mahali fulani kama vile dukani, au ofisi husika. Wateja ni kiungo muhimu sana katika shughuli yoyote ya kijasiriamali. Hakuna shughuli yoyote ya kijasiriamali inayoweza kuendelea bila kuwa na wateja. Hivyo ni muhimu kutambua na kuchanganua aina tofauti za wateja ili kuendesha shughuli kwa faida. Ni muhimu pia kujifunza namna bora ya kuwahudumia.

## Aina za wateja

Wateja wanaweza kuainishwa kwa namna tofauti. Miongoni mwa namna hizo ni kutokana na kiasi wanachonunua au tabia zao.

***Aina za wateja kutokana na kiasi cha bidhaa au huduma wanazonunua:*** Kuna aina tatu za wateja kutokana na kiasi cha bidhaa au huduma wanazonunua. Aina hizi ni wateja wakubwa, wa kati na wa rejareja.

***1. Wateja wakubwa***: Wateja hawa hununua bidhaa kwa kiasi kikubwa kutoka kwa wazalishaji na kwenda kuziuza kwa wateja wa kati.

***2. Wateja wa kati:*** Hawa ni wateja ambao hununua bidhaa kwa kiasi kikubwa ingawa si kama cha wale wakubwa ambazo huenda kuziuza kwa wateja wa rejareja.

FOR ONLINE USE ONLY

FOR ONLINE USE ONLY
DO NOT DUPLICATE

***3. Wateja wa rejareja:*** Hawa ni watumiaji wa bidhaa husika na mara nyingi hununua kiasi kidogo cha bidhaa.

***Aina za wateja kutokana na tabia zao:*** Aina za wateja kutokana na tabia zao ni kama ifuatavyo:

***1. Wateja waaminifu:*** Hawa ni wateja ambao hununua bidhaa au huduma endapo wameikubali na wameridhika nayo. Wateja hawa hurudi mara kwa mara kununua ili mradi wapate bidhaa au huduma yenye kiwango cha ubora wanaouhitaji. Mara nyingi wateja hawa ni wachache ila hufanya takribani asilimia 50 au zaidi ya mauzo ya mjasiriamali. Wateja hawa wanatakiwa kutunzwa na mjasiriamali kwa kuwapa huduma bora ambayo itawaridhisha wakati wote.

***2. Wateja wa kiasi cha gharama:*** Hawa ni wateja ambao hununua bidhaa au huduma kulingana na kiasi cha gharama au bei ya bidhaa. Wateja hawa hufanya maamuzi yao kwa kuzingatia sana punguzo la bei ya bidhaa au huduma. Wateja hawa wanaweza kutunzwa kwa kuwaelezea kuhusu thamani ya bidhaa au huduma inavyoendana na bei ili waweze kununua. Pia inatakiwa kuendelea kuwasikiliza kwa heshima hata kama hawakubaliani na bei iliyopo kwani baadaye wanaweza kuvutiwa na kubadili maamuzi yao.

***3. Wateja wenye kushawishika:*** Hawa ni wateja ambao wanakuwa na uamuzi usiopangwa wa kununua bidhaa au huduma. Mara nyingi huvutwa na hisia au kuona bidhaa. Hawa pia wanaweza hushawishika na tangazo la bidhaa husika. Wao hununua bidhaa au huduma pale wanapoiona kuwa inawavutia. Wateja hawa ni wa muhimu sana kwa sababu maamuzi yao hufanywa kutokana na hisia baada ya kuona uzuri wa bidhaa au huduma. Hivyo unatakiwa kuwapatia bidhaa au huduma bora ili iwe rahisi kwao kununua.

***4. Wateja wa mahitaji maalumu:*** Wateja hawa huwa wanaendeshwa na mahitaji maalumu. Wanapofika kwenye eneo la biashara, huangalia kama wanaweza kupata hitaji lao. Iwapo watakosa, wataondoka mara moja. Wateja hawa wanaweza pia kuwa wateja waaminifu ikiwa wanahudumiwa vizuri. Ili kuwatunza wateja hawa, inabidi ufahamu aina ya mahitaji maalumu ya wateja yanayojitokeza kwa watu wa jamii husika pamoja na wakati husika. Hii itakusaidia kuwapatia aina ya bidhaa au huduma wanayoihitaji na yenye kiwango cha ubora wanachohitaji kwa wakati.

FOR ONLINE USE ONLY



Stadi za Kazi darasa la 6.indd 132 23/07/2021 15:12

FOR ONLINE USE ONLY
DO NOT DUPLICATE

***5. Wateja wasio wa uhakika:*** Hawa ni wateja ambao hawana uhakika wa bidhaa au huduma wanayotaka kununua. Wateja hawa hawana matakwa halisi au haja maalumu ya bidhaa au huduma wanayohitaji. Badala yake, wanataka hisia ya uzoefu na mwitikio wa jamii. Ili kuwatunza wateja wa aina hii, unatakiwa kufahamu jamii husika inapendelea nini kwa wakati husika. Unatakiwa pia ujue vizuri faida za bidhaa au huduma unayotoa ili uweze kuwashawishi kununua bidhaa au huduma hiyo.

Katika somo la Stadi za Kazi umejifunza uzalishaji na utengenezaji wa bidhaa mbalimbali mfano; maua, mboga, vyakula na vinywaji, mapishi ya vyakula mbalimbali, picha, mapambo, mavazi ya kuigiza na vichezeo. Umejifunza pia stadi na sanaa mbalimbali ikiwemo ususi, ufinyanzi, uigizaji na uimbaji. Katika kuuza bidhaa au kutoa huduma yako ni lazima uzingatie aina hizi za wateja. Pia unatakiwa ukumbuke mambo matatu ya msingi yanayokuwezesha kuuza bidhaa au huduma. Mambo hayo ni endapo wateja watazihitaji, watamudu kuzinunua, na watazikubali.

Bila shaka kwa kutumia maarifa haya unaweza kubaini wateja wa bidhaa au huduma ambazo unazalisha au utakazoamua kuzalisha katika mahali husika. Hata hivyo, kukubali kwa wateja juu ya bidhaa au huduma yako inategemea pia mambo mengine kadhaa. Mfano kufahamu mahitaji ya wateja wako ili uweze kuwapatia bidhaa au huduma wanayoihitaji, kuwaelewa washindani wako katika soko na mbinu zao ili wewe uboreshe bidhaa zako zaidi yao, kuwajali wateja wako na kulenga kuwaridhisha wakati wote, pamoja na kujenga sifa ya kuaminika kwa kutimiza ahadi za kuwapatia wateja wako bidhaa au huduma kwa wakati.

### Kazi za kufanya namba 3

1. Bainisha bidhaa na huduma zote mnazozalisha wakati wa somo la Stadi za Kazi.
2. Bainisha maeneo au sehemu kila bidhaa inapouzwa na kila huduma inapotolewa.
3. Bainisha aina ya wateja wanaonunua kila bidhaa au huduma mnayozalisha.
4. Je, wapo watu wengine wasionunua bidhaa au kupata huduma hizo ambao unaweza ukawafanya wanunue? Kama wapo, utatumia mbinu gani kuwafanya wanunue bidhaa au wapate huduma hizo?



Stadi za Kazi darasa la 6.indd 133 23/07/2021 15:12

FOR ONLINE USE ONLY
DO NOT DUPLICATE

## Ufungashaji wa bidhaa na vifaa vya kupimia



Fikiri

1. Ni mambo gani huwa yanafanyika katika ufungashaji wa bidhaa na huduma zinazotolewa na wafanyabiashara?
2. Ni bidhaa gani zinazotakiwa kufungashwa?
3. Kwa nini bidhaa hufungashwa au huduma hujumuishwa?
4. Je, vifaa gani hutumika katika kupimia bidhaa hizo wakati wa kufungasha?

Ufungashaji wa bidhaa unajumuisha shughuli zote zinazohusika katika kujaza au kuweka bidhaa kwenye vifungashio kwa vipimo rasmi vya uzito, ujazo au idadi. Inashauriwa kuuza au kununua bidhaa kwa kutumia vipimo rasmi. Matumizi ya vipimo visivyo rasmi yanatakiwa kuepukwa kwani vipimo hivyo vinaweza kumpunja muuzaji au mnunuzi.

Ufungashaji unaweza kufanywa kwa namna mbalimbali na katika vipimo tofauti kulingana na aina ya bidhaa. Jedwali namba 1 linaonesha ufungashaji pamoja na vipimo vya kutumia katika kufungasha baadhi ya bidhaa ambazo unazalisha katika kazi za kufanya kwenye somo la Stadi za Kazi.

**Jedwali namba 1: Ufungashaji na vipimo vya baadhi ya bidhaa**

| Bidhaa | Kifungashio | Kipimo |
|---|---|---|
| Maua | Makasha/matenga/vikapu/chupa | Shada au idadi |
| Mboga | Makasha/matenga | Kilo au idadi |
| Matunda | Makasha/matenga | Kilo au idadi |
| Maandazi | Mifuko ya karatasi angavu | Idadi |
| Mikate | Mifuko ya karatasi angavu | Kilo au gramu |
| Kaukau | Mifuko ya karatasi angavu | Kilo, gramu au idadi |
| Bagia | Mifuko ya karatasi angavu | Kilo, gramu au idadi |
| Kababu | Mifuko ya karatasi angavu | Kilo, gramu au idadi |

FOR ONLINE USE ONLY
DO NOT DUPLICATE

| Bidhaa | Kifungashio | Kipimo |
|---|---|---|
| Keki | Makasha au mifuko ya karatasi angavu kutegemea ukubwa | Kilo au idadi |
| Samaki wa kukaanga | Makasha, Mifuko ya karatasi au kontena angavu | Idadi au kilo |
| Karanga za kukaanga | Mifuko ya karatasi au kontena angavu | Kilo au gramu |
| Chipsi au vibanzi | Kontena za aluminiamu | Kilo au gramu |
| Juisi au sharubati | Chupa, pakiti za karatasi maalumu, ndoo au vidumu | Lita au mililita |
| Maziwa | Chupa, pakiti za karatasi maalumu, ndoo au vidumu | Lita au mililita |
| Picha | Makasha angavu | Idadi |
| Mapambo | Makasha angavu | Idadi |
| Vichezeo | Makasha angavu | Idadi |
| Mavazi ya kuigizia | Mifuko ya karatasi inayoangaza | Idadi |

Unaweza kuangalia Kielelezo namba 2 kuona mifano ya ufungashaji wa bidhaa mbalimbali.

Vifungashio vinavyotumiwa kufungasha bidhaa ni lazima viwe:

(i) safi na salama ili kutunza afya ya watumiaji pamoja na mazingira;

(ii) imara na vinavyoweza kuhimili hali zote, mfano mvua na joto;

(iii) vinaendana na mazingira ya uhifadhi wa bidhaa inayohusika, mfano bidhaa ambazo hazitakiwi kupata unyevunyevu kama keki na baadhi ya mapambo, zinatakiwa kufungashwa katika kifungashio kisichoruhusu unyevunyevu kupenya;

(iv) vina umbo zuri la kumvutia mteja; na

(v) vinawiana na mahitaji ya wateja hasa katika ubora na kiasi, mfano vifungashio kwa ajili ya bidhaa za wanafunzi huwa ni vidogovidogo kwa sababu hawana uwezo wa kununua kiasi kikubwa.

FOR ONLINE USE ONLY
DO NOT DUPLICATE



*Ufungashaji kwa kutumia matenga na makasha*



*Ufungashaji kwa kutumia mifuko ya karatasi angavu*



*Ufungashaji kwa kutumia mifuko ya kitani na karatasi*



*Ufungashaji kwa kutumia gilasi zenye mfuniko*

**Kielelezo namba 2:** *Ufungashaji wa bidhaa mbalimbali*

Bidhaa iliyofungashwa hasa katika pakiti na mifuko ni vyema kuwekewa lakiri ili kuhakikisha ina ubora unaotakiwa. Hata hivyo, ili kukidhi vigezo vya ubora ni vyema bidhaa zifungashwe kwa kuzingatia sheria ya ufungashaji ya Tanzania kwa soko la ndani. Pia ufungashaji uzingatie sheria za kimataifa kwa soko la nje ya nchi. Kila bidhaa inayofungashwa ni lazima iwekewe lebo yenye taarifa muhimu. Taarifa hizo zioneshe: (a) Jina la biashara; (b) Jina la bidhaa iliyofungashwa; (c) Jina na anwani ya mtengenezaji; (d) Uzito au ujazo; (e) Orodha ya vilivyomo kufuata uzito au wingi; (f) Maelekezo ya namna ya kutumia na kuhifadhi; na (g) Tarehe ya kutegeneza au kusindika na tarehe ya mwisho wa matumizi ya bidhaa husika. Vilevile, lebo katika kifungashio zinatakiwa ziwe na rangi pamoja na mpangilio wa kuwavutia



Stadi za Kazi darasa la 6.indd 136 23/07/2021 15:12

FOR ONLINE USE ONLY

FOR ONLINE USE ONLY
DO NOT DUPLICATE

wateja. Ni dhahiri kwamba mjasiriamali akiuza bidhaa au kutoa huduma bora atawashawishi wateja warudi kununua tena. Hii itasababisha kuimarisha masoko ya bidhaa zake au huduma anayotoa.

Zifuatazo ni faida za kufungasha bidhaa kwa kutumia vifungashio bora na vipimo rasmi.

(a) Kuvutia wateja.

(b) Kutunza bidhaa kwa muda mrefu.

(c) Kuongeza thamani ya bidhaa.

(d) Kuwezesha usafirishaji wa bidhaa kuwa rahisi na salama.

(e) Kuwalinda wateja na kuwajengea imani juu ya usalama, ubora na kiasi cha bidhaa kulingana na thamani yake.

**Tanbihi:** Huduma zinazohusiana zinaweza kujumuishwa na kutolewa pamoja kama kifurushi kimoja ili kuboresha mauzo yake.

### Kazi za kufanya namba 4

1. Fanya ziara katika sehemu za wajasiriamali zilizopo karibu na eneo unaloishi kisha,
   (a) Chunguza vifungashio na vipimo vya kuuzia bidhaa mbalimbali.
   (b) Ainisha vifungashio vinavyotumika. Je, vina faida na hasara gani?
   (c) Ainisha vipimo rasmi na visivyo rasmi vinavyotumika. Onesha faida na hasara za vipimo hivyo.
   (d) Andaa taarifa ya mambo uliyofanyia uchunguzi na kisha wasilisha taarifa hiyo darasani.
2. Fungasha bidhaa mbalimbali ulizozalisha au ulizotengeneza kwa vifungashio na vipimo vinavyostahili.
3. Andaa lebo kwa kila bidhaa na kuzibandika.
4. Umepata changamoto gani katika kufanya kazi hizi? Umezitatuaje?

FOR ONLINE USE ONLY

FOR ONLINE USE ONLY
DO NOT DUPLICATE

### Udanganyifu katika biashara



Fikiri

1. Uliwahi kufanya au kufanyiwa udanganyifu katika kununua au kuuza bidhaa?
2. Ni udanganyifu gani uliofanya au kufanyiwa?
3. Ulikabiliana vipi na udanganyifu huo?

Udanganyifu ni kufanya jambo ambalo mtu anajua ni la uongo. Katika kufanya biashara kuna udanganyifu wa namna mbalimbali unaoweza kufanywa na watu unaoshirikiana nao. Mifano ya udanganyifu unaoweza kufanywa katika biashara ni mteja kudai chenji mara mbili, mtu kuiba bidhaa unapokuwa unahudumia wateja wengine na kulipa fedha pungufu. Udanganyifu wa wateja huzorotesha shughuli za mjasiriamali.

Wakati mwingine mjasiriamali anaweza kuwa mdanganyifu kwa namna mbalimbali. Mfano kuchezea mzani au kipimio cha ujazo hivyo kupima kiasi kidogo kuliko inavyostahili. Udanganyifu wa mjasiriamali mwenyewe pia huzorotesha shughuli yake kwa sababu wateja watakapobaini watakosa imani naye. Wataudhika na hawatanunua tena bidhaa au huduma yake.

Ili usidanganywe ni vema uwe makini katika kutenda shughuli za uuzaji wa bidhaa. Mhudumie mteja mmoja kwa wakati mmoja huku ukiwaambia wateja wengine wakusubiri kidogo ili nao uwahudumie. Kuwa mwangalifu kujua umepokea fedha kiasi gani kutoka kwa mteja na urudishe chenji sahihi. Ikiwa una udhaifu wa kujua hesabu chukua hatua ya kujifunza zaidi. Epuka kuwadanganya wateja kwani kwa kufanya hivyo utawaudhi na hawatarudi tena kununua bidhaa au huduma kwako. Pia, tumia lugha yenye mvuto kwa wateja wako kwa kuzingatia usemi usemwao “Biashara ni ulimi wako”.

FOR ONLINE USE ONLY

FOR ONLINE USE ONLY
DO NOT DUPLICATE

## Kazi za kufanya namba 5

1. (a) Kwa kuongozwa na mwalimu, undeni vikundi kisha kila kikundi kibuni igizo dhima linaloonesha athari za udanganyifu katika biashara na fanya igizo hilo na wenzako darasani.

   (b) Andika muhtasari wa mambo uliyojifunza katika igizo hilo.

2. Fanya ziara kwa wajasiriamali wanaofanya shughuli za ujasiriamali kwenye maeneo ya karibu na shule yako. Fanya udadisi juu ya udanganyifu unaofanywa na wajasiriamali au wateja na namna wanavyokabiliana nao. Andaa taarifa ya ziara na kuiwasilisha darasani.

## Zoezi la 3

**A. Jibu maswali yafuatayo kwa kuchagua herufi ya jibu sahihi.**

1. Stadi inayomwezesha mtu kubuni na kuanzisha miradi mbalimbali huitwa .........
   (a) Udadisi
   (b) Biashara
   (c) Ujasiriamali
   (d) Kununua na kuuuza

2. Ili mjasiriamali akubalike na wateja wake anatakiwa kufanya nini?
   (a) atambue mahitaji yao na kuwapelekea bidhaa nyumbani kwao
   (b) atambue mahitaji yao na kipato chao
   (c) atambue mahitaji yao na awakopeshe mara kwa mara
   (d) atambue mahitaji yao na awaridhishe

3. Ni udanganyifu gani unaweza kufanywa na baadhi ya wajasiriamali wasio waaminifu?
   (a) kuwazidishia chenji wateja
   (b) kuchezea vipimio
   (c) kutoa huduma wateja
   (d) kulipa kodi

FOR ONLINE USE ONLY

FOR ONLINE USE ONLY
DO NOT DUPLICATE

4. Bidhaa kama matunda, keki, samaki na mikate hufungashwa kwa kutumia vitu gani?
   (a) Makasha au mifuko ya karatasi angavu
   (b) Chupa angavu
   (c) Makopo makubwa angavu
   (d) Vitambaa angavu

5. Zifuatazo ni faida za kufungasha bidhaa isipokuwa:
   (a) Kuongeza thamani ya bidhaa
   (b) Kuwavutia wateja
   (c) Kutunza bidhaa kwa muda mfupi
   (d) Kurahisisha uchukuzi wa bidhaa

**B. Jibu maswali yafuatayo:**

1. Bainisha mambo makuu matatu yanayotakiwa ili kuwepo kwa soko la bidhaa au huduma.
2. Ainisha mambo matano ya kuzingatia katika kuchagua kifungashio cha bidhaa.
3. Taja vipimo viwili halali vya kutumia katika kufungasha bidhaa.
4. Eleza faida mbili za kutumia vipimio halali kupimia bidhaa.
5. Kwa nini ni muhimu kuweka lakiri katika bidhaa iliyofungashwa?
6. Bainisha sifa tatu za lebo ya bidhaa iliyofungashwa.

FOR ONLINE USE ONLY

FOR ONLINE USE ONLY
DO NOT DUPLICATE

# Sura ya Tisa

## Usimamizi wa fedha

### Utangulizi

*Ulipokuwa Darasa la Tano ulijifunza namna ya kutunza kumbukumbu za mapato na matumizi ya fedha. Lengo lilikuwa ni kujua mapato halisi yanayopatikana katika biashara. Katika sura hii utajifunza zaidi usimamizi wa fedha na umuhimu wa kutunza kumbukumbu za fedha. Kila siku tunatakiwa kufanya kazi ili kujipatia fedha kwa ajili ya matumizi mbalimbali. Fedha zitokanazo na kazi hizo zinatakiwa kusimamiwa vizuri ili zitumike kuendesha biashara pamoja na matumizi mengine.*

FOR ONLINE USE ONLY

## Usimamizi wa fedha



Fikiri

1. Usimamizi wa fedha ni nini?
2. Je, kuna manufaa gani yatakayotokana na usimamizi mzuri wa fedha katika biashara?

Usimamizi wa fedha ni jinsi mjasiriamali anavyoweza kufuatilia mtiririko wa uingiaji na utumiaji wa fedha. Usimamizi wa fedha unahusisha uwekaji wa kumbukumbu na ufuatiliaji wa fedha inayoingia na inayotoka. Fedha inayoingia inajulikana kama mapato na inapatikana kutokana na mauzo. Fedha inayotoka ni ile inayotumika kununua vitu vya kuuza na gharama nyingine za uendeshaji wa biashara.

Usimamizi wa fedha ni muhimu kwa mtu yeyote na hasa anayefanya biashara. Mjasiriamali anatakiwa kuwa na uwezo wa kusimamia fedha ili fedha hizo ziweze kuleta faida na kuongezeka. Yafuatayo ni manufaa yanayotokana na usimamizi mzuri wa fedha za biashara:

(a) Kujua iwapo biashara inayofanywa inazalisha faida au inaleta hasara kwa kipindi husika;



Stadi za Kazi darasa la 6.indd 141 23/07/2021 15:12

FOR ONLINE USE ONLY
DO NOT DUPLICATE

(b) Kutambua ukuaji wa mtaji wa biashara;

(c) Kufahamu iwapo thamani ya biashara inayofanywa inaongezeka; na

(d) Kujua kiasi cha kodi kinachotakiwa kulipwa.

Hivyo, usimamizi wa fedha ni muhimu katika kujenga biashara yenye kuleta faida na tija.

### Utaratibu wa usimamizi wa fedha

Fedha huhitajika na kila mtu kwa ajili ya kununua mahitaji muhimu ya nyumbani au kulipia huduma unayohitaji. Ili upate fedha kwa ajili ya mahitaji yako, unatakiwa ufanye kazi ya kuajiriwa au kujiajiri. Unaweza kujiajiri kwa shughuli za kuzalisha bidhaa kama za kilimo, kusuka mikeka, kutengeneza vyungu, kutengeneza samani, mapambo na vitu vingine vingi ambavyo umejifunza shuleni na nje ya shule. Bidhaa hizi zinaweza kuuzwa na kukupatia kipato. Ni muhimu fedha za biashara zitengwe na zile za matumizi binafsi.

Ufuatao ni utaratibu utakaomwezesha mjasiriamali kufanya usimamizi mzuri wa fedha katika biashara.

***Kupanga:*** Kupanga ni kuweka mwelekeo na utaratibu wa utekelezaji wa biashara. Mpango ni mtiririko wa kazi za kufanya unaofuatwa ili kufikia malengo ya biashara. Kabla ya kuanza biashara ni muhimu kupanga bajeti ya biashara. Bajeti ni makisio ya mapato ya fedha yanayotarajiwa kukusanywa na kutumika katika biashara ndani ya kipindi fulani.

***Kuelekeza:*** Kuelekeza ni kuongoza, kushauri, kusimamia au kuhamasisha ili kufikia mafanikio ya malengo ya biashara. Kuelekeza katika biashara ni kuweka utaratibu wa kutunza kumbukumbu za mapato na matumizi, kuainisha mapato yanayopatikana pamoja na faida.

***Kufuatilia:*** Ni kitendo cha kuhakiki maendeleo ya biashara iwapo inaendana na mipango na maelekezo yaliyopangwa. Ni muhimu kufuatilia ili kudhibiti na kuainisha matumizi ya fedha inayotokana na biashara. Ni vema kutofautisha matumizi binafsi na matumizi ya biashara.

FOR ONLINE USE ONLY

FOR ONLINE USE ONLY
DO NOT DUPLICATE

Utaratibu huu utamwezesha mjasiriamali kupangilia, kusimamia na kudhibiti matumizi ya fedha. Hivyo, mjasiriamali ataweza kufuatilia maendeleo ya biashara yake.

### Umuhimu wa kutunza kumbukumbu za biashara



Fikiri

1. Kwa nini tunatunza kumbukumbu za biashara?
2. Unafikiri kuna athari gani zinazotokana na utunzaji usio sahihi wa kumbukumbu za fedha katika biashara?

Utunzaji wa kumbukumbu za fedha ni muhimu sana kwa ustawi wa biashara yoyote. Umuhimu wa kutunza kumbukumbu za biashara ni:

(a) Kuelewa faida na hasara zinazoweza kupatikana kutokana na biashara yako;

(b) Kuelewa thamani ya biashara unayoifanya;

(c) Kupanga mipango ya uboreshaji wa shughuli za biashara unayoifanya;

(d) Kupanga matumizi ya fedha kwa usahihi; na

(e) Kujua wadaiwa na kubuni mkakati wa ufuatiliaji wake.

Zifuatazo ni baadhi ya athari za utunzaji mbaya wa kumbukumbu za fedha:

(a) Kushindwa kufahamu kiasi cha fedha kinachopatikana kila siku;

(b) Ni vigumu sana kujua ukuaji wa biashara;

(c) Mjasiriamali hatafahamu ni kwa nini anapata faida au hasara; na

(d) Mjasiriamali hatafahamu ni wateja gani wanamdai au anawadai na kiasi gani kinachodaiwa.

FOR ONLINE USE ONLY



Stadi za Kazi darasa la 6.indd 143 23/07/2021 15:12

FOR ONLINE USE ONLY
DO NOT DUPLICATE

### Soma kisamafunzo kifuatacho kwa makini

Masanja ni mjasiriamali anayefanya kazi ya utengenezaji wa samani. Siku moja Masanja alimuuzia mteja kabati kwa shilingi 1,000,000. Mteja alipochukua kabati hilo hakuwa na fedha taslimu lakini alimwahidi kulipa mwisho wa mwezi. Mwisho wa mwezi Masanja alimwendea mdaiwa wake ili amlipe fedha yake. Mteja yule alimjibu kuwa anachodaiwa ni sh.900,000 na kwamba hangelipa zaidi. Kukawa na mzozo mkali baina ya watu hawa wawili. Mwisho Masanja hakuwa na ushahidi kuonesha kuwa aliuza kabati kwa mkopo wa sh.1,000,000. Hivyo, Masanja alikuwa hana budi kukubali kulipwa sh.900,000.

#### Zoezi la kwanza

**Jibu maswali yafuatayo:**

1. Kwa nini Masanja alikubali kulipwa shilingi 900,000 badala ya sh.1,000,000?
2. Kwa nini Masanja alidanganywa?
3. Masanja alipaswa kufanya nini ili aipate fedha yake kama walivyokubaliana?
4. Je, mteja wa Masanja alionesha tabia gani?

### Namna ya kutunza kumbukumbu za fedha

Kuna namna tofauti za kutunza kumbukumbu za fedha. Kumbukumbu hizo zinaweza kutunzwa katika muundo wa rejesta. Katika muundo huu, mjasiriamali huandika kwa mkono katika vitabu vya fedha. Anaweza vilevile kutumia mfumo wa kompyuta ambao utamwezesha kutumia mojawapo ya programu za kihasibu. Zipo aina mbalimbali za rejesta zinazotumika kutunza kumbukumbu za fedha. Baadhi zipo katika muundo wa jedwali kati ya hizo ni:

(a) Rejesta ya kuandika mapato na matumizi;

(b) Rejesta ya kuandika kumbukumbu za fedha taslimu; na

(c) Rejesta ya kuandika madeni ya biashara.



Stadi za Kazi darasa la 6.indd 144 23/07/2021 15:12

FOR ONLINE USE ONLY

FOR ONLINE USE ONLY
DO NOT DUPLICATE

***Rejesta ya kuandika mapato na matumizi***: Faida ya biashara inaweza kujulikana iwapo mjasiriamali ataweka taarifa zake za mapato na matumizi vizuri. Ili Kujua faida halisi ya biashara, ni muhimu kuwa na kumbukumbu sahihi za fedha. Faida ya biashara ni fedha inayotokana na mapato au mauzo baada ya kutoa matumizi au manunuzi.

**Mfano: Faida = Mapato – Matumizi.**

Faida unayoipata unaweza kuitumia katika kuongeza mtaji wa biashara au matumizi binafsi. Kumbuka usemi usemao "fedha bila daftari hupotea bila habari"

**Soma maelezo yafuatayo kisha fuatilia namna ya kuandaa rejesta mbalimbali za kutunza kumbukumbu za fedha**

Salome huuza mbogamboga na matunda katika soko la Mjini. Kila siku anauza kabichi, machungwa, vitunguu na pilipili hoho. Baada ya kusoma mada ya usimamizi wa fedha katika somo la Stadi za Kazi, alianza kuweka kumbukumbu kwenye daftari lake. Kila siku Salome hununua bidhaa zifuatazo kwa wauzaji wa jumla:

(a) Nyanya kilo 30 @ shilingi 500 jumla shilingi 15,000;

(b) Machungwa 180 @ shilingi 50 jumla shilingi 9,000;

(c) Kabichi 6 @ shilingi 500 jumla shilingi 3,000; na

(d) Pilipili hoho 55 @ shilingi 100 jumla shilingi 5,500.

Salome huanza kuuza bidhaa zake kwa rejareja. Kwa siku Salome anaweza kupata fedha kama ifuatavyo:

(a) Shilingi 15,000 kwa kuuza nyanya kilo 20 @ shilingi 750;

(b) Shilingi 2,400 kwa kuuza kabichi 3 @ shilingi 800;

(c) Shilingi 6,000 kwa kuuza pilipili hoho 30 @ shilingi 200; na

(d) Shilingi 8,000 kwa kuuza machungwa 80 @ shilingi 100.

Matunda na mboga zinazobakia huziuza siku inayofuatia. Kabla ya kurejea nyumbani, kila siku anaandika alichopata na alichotumia. Pia anafanya hesabu ya kile anachobakia nacho mwishoni mwa siku. Jedwali namba 1 linaonesha kiasi cha fedha alichotumia Salome kununua bidhaa za kuuza.

FOR ONLINE USE ONLY

FOR ONLINE USE ONLY
DO NOT DUPLICATE

**Jedwali namba 1: Rejesta ya kuandika manunuzi au matumizi**

| Siku ya kununua | Bidhaa | Kiasi | Bei (sh) | Jumla (sh) |
|---|---|---|---|---|
| Siku ya kwanza | Nyanya (kilo) | 30 | 500.00 | 15,000.00 |
| | Machungwa | 180 | 50.00 | 9,000.00 |
| | Pilipili hoho | 55 | 100.00 | 5,500.00 |
| | Kabichi | 6 | 500.00 | 3,000.00 |
| **Jumla** | | | | **32,500.00** |

Jedwali namba 1 linaonesha kiasi cha fedha kilichotumika kununua mbogamboga na matunda kwa siku ya kwanza.

**Jedwali namba 2: Rejesta ya kuandika mauzo au mapato**

**Siku ya kwanza**

| Bidhaa | Kiasi | Bei (sh) | Jumla (sh) |
|---|---|---|---|
| Nyanya (kilo) | 20 | 750.00 | 15,000.00 |
| Machungwa | 80 | 100.00 | 8,000.00 |
| Pilipili hoho | 30 | 200.00 | 6,000.00 |
| Kabichi | 3 | 800.00 | 2,400.00 |
| **Jumla** | | | **31,400.00** |

FOR ONLINE USE ONLY

FOR ONLINE USE ONLY
DO NOT DUPLICATE

**Siku ya pili**

| Bidhaa | Kiasi | Bei (sh) | Jumla (sh) |
|---|---|---|---|
| Nyanya (kilo) | 10 | 750.00 | 7,500.00 |
| Machungwa | 100 | 100.00 | 10,000.00 |
| Pilipili hoho | 25 | 200.00 | 5,000.00 |
| Kabichi | 3 | 800.00 | 2,400.00 |
| **Jumla** | | | **24,900.00** |

Jedwali namba 2 linaonesha fedha iliyopatikana kwa kuuza mbogamboga na matunda kwa siku mbili.

Kumbukumbu za mapato na matumizi, hutumika kuandaa taarifa ya mapato na matumizi ya mwezi, miezi mitatu, miezi sita au ya mwaka. Jedwali namba 3 linaonesha taarifa ya mapato na matumizi katika biashara ya Salome mwishoni mwa mwezi Aprili.

**Jedwali namba 3: Rejesta ya kuandika mapato na matumizi - mwezi Aprili**

| Mapato | | | Matumizi | | |
|---|---|---|---|---|---|
| **Tarehe** | **Maelezo** | **Kiasi (sh)** | **Tarehe** | **Maelezo** | **Kiasi (sh)** |
| 30.04.2019 | Mauzo ya mboga na matunda | 56,300.00 | 30.04.2019 | Manunuzi ya mboga na matunda | 32,500.00 |
| | | | | | |
| | | | **Faida ghafi** | | 23,800.00 |
| **Jumla** | | **56,300.00** | **Jumla** | | **56,300.00** |



Stadi za Kazi darasa la 6.indd 147 23/07/2021 15:12

FOR ONLINE USE ONLY
DO NOT DUPLICATE

Jumla ya mapato ni sh 56,300.00 na matumizi ni sh 32,500.00. Ili kubaini faida, inatakiwa kutoa manunuzi kutoka kwenye mapato. Kumbuka kwamba, kanuni ya kukokotoa faida ni **Faida = Mapato – Matumizi.**

Jedwali namba 3 linaonesha kuwa faida ambayo ni sh 23,800.00 imewekwa upande wa kulia ili kutafuta mlinganisho wa hesabu. Angalia upande wa matumizi una kiasi kidogo kuliko mapato. Endapo kiasi cha matumizi kitakuwa kikubwa kuliko mapato, tofauti itawekwa upande kushoto wa jedwali na itakuwa ni hasara.

***Rejesta ya kuandika fedha taslimu***: Hii ni rejesta inayotumika kuandika fedha taslimu inayoingia na inayotumika. Mjasiriamali huitumia rejesta hii kwa kipindi chote anachofanya biashara yake. Rejesta hii husimamia fedha inayoingia kutokana na mauzo ya bidhaa kwa taslimu au madeni yalilyolipwa kwa kipindi fulani. Rejesta hii humwezesha mjasiriamali kusimamia fedha inayoingia na inayotumika katika maeneo mbalimbali ya biashara kwa kipindi hicho. Rejesta hii ipo katika muundo wa jedwali linaloonesha makusanyo na malipo yanayofanyika kwa kipindi kinachohusika kama inavyooneshwa katika Jedwali namba 4.

**Jedwali namba 4: Rejesta ya kuandika fedha taslimu kwa mwezi Aprili**

| Fedha iliyoingia | | Fedha iliyotumika | |
|---|---|---|---|
| **Bidhaa au huduma** | **Kiasi (sh)** | **Bidhaa au huduma** | **Kiasi (sh)** |
| Fedha ya mauzo ya mboga na matunda | 56,300.00 | Kununua mboga na matunda | 32,500.00 |
| Mteja amelipa deni | 20,000.00 | Deni la fedha ya usafiri | 500.00 |
| | | Kulipia pango | 15,000.00 |
| | | | **48,000.00** |
| | | **Faida ghafi** | **28,300.00** |
| **Jumla** | **76,300.00** | | **76,300.00** |

FOR ONLINE USE ONLY



Stadi za Kazi darasa la 6.indd 148 23/07/2021 15:12

FOR ONLINE USE ONLY
DO NOT DUPLICATE

Jedwali namba 4 linaonesha kiasi cha fedha taslimu kilichoingia na kiasi kilichotumika kuendesha biashara. Vilevile, linaonesha salio la fedha taslimu mwishoni mwa mwezi utakaokuwa umeandaa taarifa inayohusika. Kumbukumbu hizi zitamwezesha mjasiriamali kujua akiba aliyonayo. Humwezesha pia kufanya uamuzi sahihi wa matumizi ya fedha za biashara yake.

***Rejesta ya kuandika madeni ya biashara:*** Katika aina hii ya rejesta mjasiriamali huweka kumbukumbu zinazohusu fedha anazodai na anazodaiwa. Rejesta hii ipo katika muundo wa jedwali. Ndani yake mjasiriamali huandika gharama za bidhaa au huduma zilizonunuliwa kwa mkopo. Vilevile, huandika ndani yake bidhaa au huduma zilizouzwa kwa mkopo kama Jedwali namba 5 linavyoonesha.

**Jedwali namba 5: Rejesta ya kuandika madeni ya biashara**

| Aina ya bidhaa au huduma | Daiwa | Dai |
|---|---|---|
| | Kiasi (sh) | Kiasi (sh) |
| 1. Mauzo ya mboga na matunda (aliuza kwa mkopo) | | 7,000.00 |
| 2. Kulipia pango (hajalipa pango) | 9,000.00 | |
| 3. Malipo ya ushuru (hajalipa ushuru) | 2,500.00 | |
| 4. Kulipia usafiri (hajalipia usafiri) | 1,000.00 | |
| 5. Mauzo ya samani chakavu (aliuza kwa mkopo) | | 12,500.00 |
| **Jumla** | **12,500.00** | **19,500.00** |

Jedwali hili litamsaidia mjasiramali kutunza: (a) taarifa sahihi ya rasilimali au fedha zilizoko nje ya biashara; na (b) madeni ambayo mjasiriamali anatakiwa kulipa.

FOR ONLINE USE ONLY



Stadi za Kazi darasa la 6.indd 149 23/07/2021 15:12

FOR ONLINE USE ONLY
DO NOT DUPLICATE

***Kuandaa taarifa ya hesabu za fedha***: Uandaaji wa taarifa kwenye vitabu vya hesabu unategemea jinsi ambavyo mjasiriamali anavyotunza kumbukumbu za mapato na matumizi. Maelezo ya fedha zote zinazoingia na zinazotoka kwenye biashara hutumika katika kuandaa taarifa ya fedha. Taarifa za hesabu zitamwezesha mjasiriamali kujua ukuaji wa biashara yake. Kwa kujua ukuaji wa biashara, mjasiriamali anapata nafasi ya kupanga jinsi ya kudhibiti biashara kulingana na kiwango cha ukuaji. Kadiri shughuli za biashara zinavyoongezeka, ndivyo usimamizi madhubuti unavyohitajika. Iwapo mjasiriamali hatakuwa na kumbukumbu za fedha, itakuwa vigumu kufuatilia rasilimali za biashara ambazo ni muhimu katika uandaaji wa taarifa ya hesabu za fedha. Rasilimali za biashara huoneshwa kwa kutumia jedwali linaloitwa mizania.

***Mizania:*** Mizania hupatikana kwa kuwepo kwa rasilimali zinazoweza kuendesha biashara kwa kipindi husika. Mizania ni taarifa ya kifedha inayoonesha rasilimali, madeni na mtaji wa biashara. Taarifa hii hupima ukubwa au thamani ya biashara. Mizania huwa katika mpangilio wa jedwali. Jedwali hilo huonesha kiasi cha mali ambayo mjasiriamali anamiliki na kiasi cha mali na fedha ambayo mjasiriamali anadaiwa. Mizania hupima uwezo wa rasilimali kuendesha biashara kama inavyooneshwa katika kanuni ifuatayo:

**Rasilimali za biashara = Mtaji + Kiasi anachodaiwa**

## Vipengele vya Mizania

Mizania ina vipengele vitatu ambavyo ni rasilimali, mtaji wa biashara na madeni ya biashara. Vipengele hivyo vimefafanuliwa kama ifuatavyo.

***Rasilimali za biashara***: Rasilimali za biashara ni vitu vyote vya thamani ambavyo vinamilikiwa na mjasiriamali. Rasilimali huainishwa kulingana na muda wa kutumika. Kuna rasilimali za muda mfupi na za kudumu. Rasilimali za muda mfupi ni rasilimali ambazo muda wake wa kutumika hauzidi mwaka mmoja. Kwa mfano kiasi cha fedha kilichoko benki na bidhaa. Rasilimali za kudumu hutumika kwa muda mrefu zaidi ya mwaka mmoja. Mfano, ardhi, mashine, vifaa, samani, na bidhaa za kilimo kama ng'ombe. Hizi ni rasilimali ambazo zinaweza kumilikiwa na mjasiriamali kwa ajili ya kuendeshea biashara.

FOR ONLINE USE ONLY



Stadi za Kazi darasa la 6.indd 150 23/07/2021 15:12

FOR ONLINE USE ONLY
DO NOT DUPLICATE

***Mtaji wa biashara:*** Mtaji ni kiasi cha rasilimali vitu na fedha inayowekezwa kwa ajili ya kuendeshea biashara. Mtaji hujumuisha pia faida iliyobaki wakati wa matumizi katika biashara; na fedha kama vile mkopo wa benki. Matumizi hayo ni pamoja na gharama ya manunuzi ya bidhaa za biashara, na gharama nyingine za uendeshaji. Hizo zinajumuisha mishahara ya watu uliowaajiri pamoja na malipo ya kodi.

***Madeni ya biashara:*** Biashara inaweza kufanyika kwa kununua na kuuza bidhaa au huduma kwa mkopo. Hivyo, katika biashara kuna madeni ambayo mjasiriamali atakuwa anadai na mengine kudaiwa na wenye bidhaa. Madeni hayo hulazimika kulipwa katika kipindi maalumu kilichowekwa. Madeni haya yasiposimamiwa vizuri yanaweza kuyumbisha biashara inayohusika.

## Kupanga bajeti



Fikiri,

Je, kuna umuhimu gani wa kupanga bajeti kwa kila fedha inayoingia mfukoni mwako?

Bajeti hupangwa kulingana na mahitaji kwa kufanya yafuatayo:

(a) Kuainisha kiasi cha akiba ulichonacho kabla ya kutumia; na

(b) Kuweka pembeni fedha ya akiba kwa ajili ya maendeleo ya baadaye.

Ni muhimu kupanga bajeti kwa sababu husaidia kujua maeneo muhimu ya kipaumbele. Bajeti inaweza kupangwa kulingana na mahitaji ya mtu binafsi au familia kama vile:

(a) kununua mavazi;

(b) kununua chakula;

(c) kulipa ada ya shule; na

(d) kupata huduma mbalimbali kama vile huduma za afya na mawasiliano.

FOR ONLINE USE ONLY

FOR ONLINE USE ONLY
DO NOT DUPLICATE

**Zoezi la pili**

1. Toa sababu kuu tatu kwa nini tunatakiwa kutunza kumbukumbu za biashara.
2. a) Eleza maana ya mizania katika kuweka kumbukumbu za biashara.

   b) Ainisha vipengele vitatu muhimu vya kuzingatia katika mizania
3. Eleza umuhimu wa rejesta katika biashara.

## Kodi

Kodi ni chanzo kikuu cha mapato ya serikali. Serikali hutegemea makusanyo ya kodi kutoka kwa wafanyabiashara na maeneo mengine. Serikali hutumia kodi kuendesha shughuli zake kama vile kujenga madarasa, hospitali na barabara. Pia, hutumia kodi kuboresha miundombinu ya maji, umeme na kulipa mishahara ya watumishi wa umma. Kulipa kodi ni wajibu wa kila mwananchi. Hivyo, kila mtu anatakiwa kufanya kazi za kujiingizia kipato na kulipa kodi.

***Aina za kodi:*** Kodi inaweza kutolewa na mtu mmoja mmoja, kwa mfano, kodi ya mapato. Hii ni asilimia ya tozo inayotolewa baada ya kufanya kazi au biashara inayokuingizia kipato. Ni kodi ambayo kila mtu mwenye kipato hutozwa asilimia fulani kulingana na jumla ya mapato yake kwa mwaka. Mfano wa kodi hizi ni tozo inayotolewa kwa mfanyabiashara mwenye mtaji na kipato kikubwa. Pia, aina hii ya kodi hutolewa kwenye mshahara au kipato cha mfanyakazi wa umma. Vilevile, kuna kodi inayotozwa kupitia bei za bidhaa au huduma inayotolewa. Mfano wa aina hii ya kodi ni kodi ya ongezeko la thamani. Kodi hii hutozwa kwa bidhaa zinazoongezwa thamani kutoka kiwandani kulingana na asilimia ya bei ya bidhaa. Kiasi hiki kilichoongezwa kama tozo hulipwa na wateja kupitia bei ya bidhaa inayohusika.

FOR ONLINE USE ONLY



Stadi za Kazi darasa la 6.indd 152 23/07/2021 15:12

FOR ONLINE USE ONLY
DO NOT DUPLICATE

Zipo kodi zinazotegemea mali za watu. Kodi za aina hii ni kodi ya nyumba, kodi ya viwanja, kodi ya shamba na kodi ya pango la nyumba. Aina nyingine ya kodi ni ushuru wa bidhaa. Hii ni aina ya tozo ya bidhaa inayotozwa kwa kuangalia thamani ya bidhaa hiyo. Kwa mfano, katika kodi hii asilimia 5 hukatwa kama ushuru wa gunia la mkaa. Kiasi hiki kinachotozwa huitwa ushuru wa bidhaa.

**Soma kisamafunzo kifuatacho kisha jibu maswali katika zoezi la Tatu**
Kitale hufanya biashara ya kununua na kuuza mkaa. Mkaa huu huununua kijijini na kuuleta mjini ili auze kwa faida. Gunia moja la mkaa hununua shilingi 40,000.00 na kulisafirisha hadi mjini kwa shilingi 12,000.00. Njiani kuna kizuizi ambapo kila gunia la mkaa hutozwa ushuru wa asilimia 5 ya bei ya gunia.

## Zoezi la 3

**Jibu maswali yafuatayo:**

1. Kama ushuru ni asilimia 5, Je, Kitale atatoa ushuru wa shilingi ngapi kwa gunia moja?
2. Kitale akitoa ushuru wa asilimia 5 na kuongeza faida yake ya shilingi 10,000.00. Je, Kitale atauza gunia la mkaa shilingi ngapi akifikisha mjini?

## Kazi za kufanya namba 1

Tembelea maeneo ya biashara yaliyopo karibu na shule au soko au kioski na mfanye mahojiano na wauzaji kuhusu uwekaji wa kumbukumbu za fedha za biashara zao pamoja na ulipaji wa kodi. Andaeni ripoti na kuiwasilisha darasani.

FOR ONLINE USE ONLY

FOR ONLINE USE ONLY
DO NOT DUPLICATE

## Zoezi la 4

**A. Andika Ndiyo kwa sentensi iliyo sahihi na Hapana kwa sentensi isiyo sahihi.**

1. Mtaji ni kiasi cha fedha au mali inayowekezwa kwa maendeleo ya biashara ____.
2. Utunzaji wa kumbukumbu za fedha si muhimu sana kwa ustawi wa biashara yoyote _____.
3. Kodi ya nyumba na viwanja ni kodi zinazotegemea mali za watu ______.
4. Mizania ni taarifa inayohusu matumizi tu _________.
5. Kumbukumbu za kifedha zinaweza kutunzwa kwa kutumia mfumo wa kompyuta _____.
6. Rejesta ya mapato na matumizi hutumika kuandika fedha inayoingia na inayotumika na mjasiriamali katika biashara yake ________.

**B. Fanya kazi zifuatazo kwenye daftari lako la mazoezi.**

1. Taja aina za kodi zilizozungumziwa kwenye sura hii.
2. Taja faida kuu mbili (2) za kulipa kodi.
3. Taja aina mbalimbali za Rejesta za kuweka kumbukumbu za fedha katika biashara.
4. Eleza madhara yanayoweza kutokea endapo mjasiriamali hataweka kumbukumbu zake vizuri.

FOR ONLINE USE ONLY

## Msamiati

**Faida ghafi** Ziada inayopatikana katika biashara baada ya kutoa gharama za ununuzi wa bidhaa na kabla ya kutoa gharama nyingine kama vile kodi na uendeshaji wa biashara





Stadi za Kazi darasa la 6.indd 154 23/07/2021 15:12


Vitabu vingine vya Darasa la Sita
Taasisi ya Elimu Tanzania


## Darasa la Sita














ISBN 978-9987-09-039-6
9 789987 090396